# Nipashe

Jumanne Julai 30, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-


ISSN 0856 • Na. 0579983

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

ww.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

## MOI sasa kutibu uvimbe katika ubongo kupitia paja

UKURASA 3




UKURASA 13

# Membe akiri sauti yake kudukuliwa



• **Ataka** mamlaka husika kuchukua hatua, aonya kampuni za mawasiliano kuingia matatani... *Endelea ukurasa 2*


## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**OFISA NIDA MATATANI KWA MADAI YA RUSHWA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Dodoma...

UKURASA WA 26

**NCCR YATANGAZA SAFU MPYA UONGOZI**

CHAMA cha NCCR-Mageuzi kimetangaza safu mpya ya uongozi, huku...

UKURASA WA 26

**KABIGI KUPUMZISHWA NYUMBA YA MILELE LEO**

MWILI wa mwanahabari mbobezi Agnes Kabigi (53), aliyefariki dunia ghafla...




Kuhani wa Kanisa la Halisi la Mungu Baba, Jambo Jipya (kushoto), akionyesha waumini wa kanisa hilo, friji inayotumia mkaa alilolibuni, katika maonyesho ya uzalishaji yaliyoandaliwa na kanisa katika eneo la Tegeta, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Makonda awaonya wachafu SADC

UKURASA 3



## Daraja refu zaidi nchini kujengwa Ziwa Victoria

UKURASA 2


**MICHEZO** SIMBA MIPANGO AFRIKA IMEKOLEA UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Membe akiri sauti kudukuliwa

**Na Romana Mallya**

ALIYEKUWA Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bernard Membe, amezungumza kuhusu mawasiliano yake ya simu kudukuliwa, huku akikiri sauti iliyosambazwa kwenye mitandao ya kijamii hivi karibuni ni yake.

Katika mahojiano na moja ya vituo vya redio jijini Dar es Salaam jana, Membe alikiri mawasiliano yake kudukuliwa na kutoa tahadhari kwa kampuni za mawasiliano ya simu kwa kuwa changamoto hiyo huenda ikazitia hasara kubwa.

"Sauti ni za kwangu, ni mimi 100 kwa 100 na nimeifanyia kazi na ninajua imetoka wapi kwa sababu nina miiko ya kuzingatia sisemi.

"Ni sauti ya kwangu kabisa na ninaelewa kila kilichotokea. Unaweza kuingia ugonjwa wa udukuzi, kama wale wanaotoa taarifa hizi za udukuzi hawachukuliwi hatua, 'hackers' (wadukuzi) wapo duniani, wanataka fedha tu.

"Ni kosa la jinai kudukua mawasiliano ndiyo maana dunia nzima huwasikii wanadukuana waziwazi. Hapa kwetu watu wenye wajibu wa kukataza udukuzi ni TCRA (Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano) mitandao yote ipo chini yao.

"Tuna sheria zipo, sheria mpya ya mwaka 2013, sidhani kama imerekebishwa, inakataza kakatata udukuzi na dunia nzima hamuisikii ikifanya hayo kwa sababu mbili kubwa:

"Sababu ya kwanza, ukidukua yule anayedukuliwa akalalamika, utapata adhabu kubwa sana ndiyo maana dunia haigusi eneo hili, wanadukua na vyombo vya usalama wanadukua lakini haviwezi kutoa 'public' (waziwazi) 'information' (taarifa) ambazo ni 'top security' (usalama wa hali ya juu).

"Lakini, kuna baya zaidi ya hili nililolisema, kama hilo moja halitoshi, sikiliza hili la pili kwa umakini, sababu ya pili inayofanya dunia isitake kutoa taarifa za udukuzi nje nchini ni kwamba hii ni biashara.

"Mimi Membe leo nikiona nimedukuliwa na mtu mwingine yeyote yule, siyo lazima niende kwenye chombo cha sheria nikalalamike kudai fidia, hata kidogo. Dunia itakapojua wajanja, wataalamu wa IT na 'hackers' (wadukuzi) wataingia jijini Dar es Salaam."

Alipotafutwa na kituo hicho cha redio kuzungumzia suala hilo, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, alisema serikali imeandaa muswada ili kutunga sheria kulinda taarifa za mtu binafsi kudukuliwa.

"Udukuzi upo mkubwa tu, ni suala la teknolojia, vijana kwenye IT wanatengeneza mawazo mengi kwa siku, kwa hiyo wanafanya majaribio mengi.

"Nikupe mfano mmoja, ATCL (Shirika la Ndege) wakati tunaanza tulidukuliwa kwenye ukataji wa tiketi, bahati nzuri aliyekuwa anatudukua ni bwana mdogo aliyeku-

INAENDELEA UK. 8



Mwenyekiti wa Chama cha NCCR –Mageuzi Taifa, James Mbatia, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akitangaza safu mpya ya uongozi wa kitaifa wa chama hicho, waliochaguliwa katika mkutano mkuu wa chama uliofanyika wikiendi. Kulia ni Katibu Mkuu mpya, Elizabeth Mhagama na (kushoto) ni Naibu Katibu Mkuu Bara, Rehema Kahangwa. **PICHA: JOHN BADI**

## Daraja refu zaidi nchini kujengwa Ziwa Victoria

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imetia saini mkataba wa ujenzi wa daraja la Kigongo-Busisi litakalokuwa na urefu wa Km 3.2, likiunganisha mikoa ya Mwanza na Geita.

Imeelezwa kuwa ujenzi wa daraja hilo litalokuwa refu zaidi nchini, utagharimu Sh. bilioni 592 na utachukua miaka minne kukamilika.

Mkataba huo ulitiwa saini jijini Dar es Salaam jana kati ya Wakala wa Barabara (Tanroads), Kampuni za China Railway 15 na China Civil Engineering Group.

Hafla ya utiaji saini mkataba huo pia ilihudhuriwa na wabunge kutoka Kamati ya Bunge ya Miundombinu na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Seleman Jafo.

Akizungumza wakati wa utiaji saini, Mtendaji Mkuu wa Tanroads, Patrick Mfugale, alisema daraja hilo litapita juu ya mkondo wa Ziwa Victoria na litakuwa na upana wa mita 28.

Alisema daraja hilo litakuwa na njia mbili, maegesho, waenda kwa miguu,

INAENDELEA UK. 8


**UBALOZI WA MAREKANI, DENMARK, UHOLANZI, BRITISH HIGH COMMISSION, SWITZERLAND (SDC), UNICEF & SAVE THE CHILDREN DSM**

**MNADA WA HADHARA:**

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na **Ubalozi wa Marekani, Danish, Uingereza, Uholanzi, Switzerland (SDC), UNICEF na Save the Children na mradi wa Swiss** watauza kwa mnada wa hadhara Magari, Pikipiki, Generator na Funicha za nyumbani tarehe 3 August, 2019 Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street.

**Fenicha na Computer zitaanza kuuzwa kuanzia saa 4:00 asubuhi:** Sofa set, Chest drawer, Dressers, China base, Hutch, Credenza, Meza za chakula/Viti, Meza za ofisi, Book case, Meza za garden/Viti, Carpet, Vitanda, Magodoro, Fridge, Freezer, Washer, Dryer, Majiko ya umeme, A/c split units, Photocopy, Tairi za magari , TV, Mashine kubwa za kutengenezea Barafu, Solar system, Laptop, Computer set, Water pump 20HP na vingine vingi.

**Magari na Generator zitaanza kuuzwa kuanzia saa 6.00 mchana.**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Toyota Land Cruiser Prado | TX Diesel Engine | 2012 | Haujalipwa |
| 2 | Nissan Patrol Station Wagon | TD42 Diesel Engine | 2012 | Haujalipwa |
| 3 | Nissan Ranger P/Up Double Cabin | Diesel Engine | 2015 | Haujalipwa |
| 2 | Pikipiki Yamaha AG & Suzuki TF | AG IOO & TF125 Petrol | 1999 | Haujalipwa |
| 3 | Generator 20 , 22 & 130 KVA | Diesel Engine silence | 2010 | Haujalipwa |
| 3 | Air Conditioner (Central Cooling Unit) | Cooling – 19.08 KW. | - | Haujalipwa |

Mali zote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza, Lion Street kuanzia tarehe 31 July mpaka 2 August, 2019,saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.
Generator 20KVA inaweza kukaguliwa Zanzibar, mtaa wa kilimani, (Kilimani plaza) kuanzia tarehe 31 July mpaka 2 August, 2019 kuanzia saa 4.00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni – wasiliana na Mr. Musesa 0769733474 ZNZ.

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi wa Fanicha atatakiwa kulipa malipo yote kwa mweka hazina (cashier). Na mnunuzi wa Gari/Generator atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 4 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 9 August, 2019 saa 10:00 jioni, ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari au Generator litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2 Malipo kwa njia ya VISA na Master cards za CRDB bank yanakubalika.
3 Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
4 Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5 Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6 Kila mtu atatakiwa kuwa na bid namba itakayo patikana getini.

**Kwa maelezo zaidi waone:**
**UNIVERSAL AUCTION CENTRE**
**PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA**
**CELL NO: 0754 284 926, 0757 284 926**
**E-mail: universalauction@hotmail.com DAR ES SALAAM**

115346401


## Ofisa Nida matatani tuhuma za rushwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Dodoma inawashikilia watu saba kwa tuhuma mbalimbali za rushwa, Ofisa wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida), Abdulkarim Kabunga.

Mtumishi huyo wa Nida, mwenye umri wa miaka 26 ambaye ana ajira ya muda, anashikiliwa kwa madai ya rushwa ya Sh. 30,000 kutoka kwa mtu mmoja aliyekuwa akihitaji kitambulisho cha taifa ili amsaidie kukipata haraka.

Mbali na mtumishi huyo, pia wamo baba na mwanawe ambao wa-

INAENDELEA UK. 8

# MOI kutibu uvimbe ubongo kupitia paja

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa (MOI) imesema inatarajia kuanza kutumia teknolojia ya kisasa ya kuondoa uvimbe na kutibu ubongo kupitia mshipa wa paja badala ya kupasua fuvu.

Imesema upasuaji huo utafanyika kupitia mshipa mkubwa wa damu utakaopitisha vifaa vitakavyokwenda moja kwa moja sehemu yenye shida ndani ya ubongo.

Imesema upasuaji huo utafanyika katika maabara maalum ya upasuaji wa ubongo itakayokuwa na vifaa vyenye kamera zinazoonyesha eneo linalofanyiwa upasuaji.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, alipofungua kongamano la kimataifa la mafunzo ya upasuaji wa ubongo kwa mbinu za kisasa kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Colorado, Marekani.

Alisema tayari serikali imetenga Sh. bilioni 2.9 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kisasa vya upasuaji kwa kutumia mshipa wa paja na huduma hiyo inatarajiwa kuanza kutolewa nchini mwishoni mwa mwaka huu.

"Miezi miwili iliyopita, serikali ilitenga Sh. bilioni 2.9 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kisasa vya upasuaji wa ubongo kwa kutumia mshipa wa paja badala ya kuchana fuvu la kichwa, lengo ni Watanzania wapate huduma za matibabu bora kwa njia ya kisasa badala ya kusafiri kwenda nje ya nchi," alisema.

Dk. Ndugulile alisema serikali pia imeshawapeleka China wataalamu watano kwa muda wa miezi mitatu kujifunza upasuaji huo.

Aliongeza kuwa serikali inaendelea kuboresha huduma za matibabu nchini kwa kuleta wataalamu kutoka nje ya nchi kuja kubadilisha uzoefu na wataalamu wa ndani katika kuhakikisha wanaboresha huduma za matibabu ya mfumo wa fahamu na ubongo kwa njia ya kisasa.

Sambamba na hilo, kiongozi huyo alisema serikali imetenga Sh. bilioni 16.5 kwa ajili ya kukamilisha jengo jipya la MOI na kuweka vifaa vya kisasa kwa ajili ya upasuaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Respicious Boniface, alisema matibabu hayo yatasaidia kuokoa muda wa matibabu na gharama ambao kwa sasa zinafika Sh. milioni tano hadi sita nchini na hadi Sh. milioni 40 kwa matibabu ya nje ya nchi.

Alisema matibabu yanayotolewa sasa ni kuchana fuvu la kichwa na kutibu tatizo lililoko ndani ya ubongo, huduma ambayo inatumia muda mrefu na gharama kubwa.

"Duniani kote wanatumia huduma hii ya kutibu ubongo kwa kutumia mshipa wa paja na hivyo MOI tayari tumejipanga kwa ajili ya kuanza kutoa huduma hii muhimu," alisema.

# Makonda aonya wachafu SADC


**Na Mary Geofrey**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, ameibua gumzo kwenye mitandao ya kijamii baada ya jana kutangaza kupiga marufuku mtu yeyote kuingia jijini humo kama hajafanya usafi wa mwili wake kwa kuoga, kufua na kupiga pasi nguo zake.

Makonda ametoa kauli hiyo ikiwa leo zimebaki siku tisa Tanzania kupokea ugeni mzito wa viongozi wakuu wa nchi 16 zinazounda Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Africa (SADC). Mkuu huyo wa mkoa amesema ni muhimu wakazi wa jiji hilo kuchukua tahadhari mapema kuhakikisha wanakuwa wasafi ili kuepuka kukamatwa na vyombo vya dola.

Makonda alitoa angalizo hilo jana wakati wa uzinduzi wa kampeni ya usafi katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini (Terminal I) yenye lengo la kuendeleza usafi kwenye jiji hilo ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya kupokea ugeni wa marais, makatibu wakuu na

INAENDELEA UK.8

TANGAZO

# BENKI YA STANBIC TANZANIA

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa | Robo Mwaka/Mwaka uliopita |
|---|---|---|---|
| | | 30-Jun-19 | 31-Mar-19 |
| | **A. MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 12,790 | 9,964 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 144,127 | 152,498 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 70,122 | 71,357 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 19,054 | 61,833 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 39,759 | 22,354 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 149,076 | 184,569 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 161,559 | 151,350 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 801,023 | 810,242 |
| 12 | Mali Nyingine | 52,581 | 50,113 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 52,655 | 54,334 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **1,502,746** | **1,568,614** |
| | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 159,406 | 214,917 |
| 18 | Amana za Wateja | 905,807 | 903,165 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 25,274 | 36,173 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 1,159 | 2,477 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 26 | 26 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 42,562 | 36,652 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 39,759 | 22,354 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 3,410 | 908 |
| 27 | Dhima Nyingine | 30,030 | 59,161 |
| 28 | Madeni | 18,396 | 18,941 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **1,225,830** | **1,294,775** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **276,916** | **273,840** |
| | **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 8,400 | 8,400 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 112,396 | 112,396 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 125,054 | 137,761 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 10,996 | 6,307 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 20,069 | 8,975 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **276,916** | **273,840** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 706,005 | 574,742 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 68,786 | 62,159 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 41,424 | 38,816 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Madeni | 18.4% | 17.5% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 8.1% | 7.3% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 91.4% | 90.4% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 58.7% | 55.6% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 81.3% | 79.0% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -0.9% | 4.2% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -4.2% | 11.7% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi |
|---|---|---|---|---|---|
| | TAARIFA | 30-Jun-19 | 30-Jun-18 | 30-Jun-19 | 30-Jun-18 |
| 1 | Mapato ya Riba | 27,351 | 23,254 | 51,772 | 46,392 |
| 2 | Gharama za Riba | 4,169 | 2,324 | 8,014 | 5,186 |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **23,182** | **20,930** | **43,758** | **41,207** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | -208 | 2,425 | 222 | 3,858 |
| | **Mapato baada ya tengo katika mikopo** | 23,390 | 18,505 | 43,536 | 37,349 |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba** | **12,356** | **12,435** | **28,326** | **27,591** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 6,533 | 5,869 | 16,390 | 14,338 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 5,785 | 6,369 | 11,850 | 12,857 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 38 | 197 | 86 | 395 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba** | **28,208** | **27,185** | **54,790** | **55,168** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 13,825 | 14,442 | 27,603 | 28,392 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 3,792 | 3,847 | 7,097 | 8,301 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 10,591 | 8,896 | 20,090 | 18,476 |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **7,538** | **3,755** | **17,072** | **9,771** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 2,849 | 1,295 | 6,076 | 3,461 |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **4,690** | **2,460** | **10,996** | **6,310** |
| **11** | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| | i) Mabadiliko ya thamani katika amana zinazouzika | -666 | -2,575 | -635 | 111 |
| | ii) Kodi ya mabadiliko ya thamani katika amana zinazouzika | 200 | 773 | 190 | -33 |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **4,224** | **657** | **10,552** | **6,388** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 522 | 555 | 522 | 555 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 0.6 | 0.3 | 1.3 | 0.9 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 9 | 9 | 9 | 9 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.3% | 0.2% | 0.7% | 0.5% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 1.7% | 1.1% | 4.2% | 2.9% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 71.0% | 76.2% | 68.4% | 74.6% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 1.9% | 2.1% | 3.5% | 4.0% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa | Robo Mwaka iliyopita | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|---|
| | TAARIFA | 30-Jun-19 | 31-Mar-19 | 30-Jun-19 | 30-Jun-18 |
| **I:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **4,690** | **6,307** | **10,996** | 6,310 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 3,282 | 3,260 | 6,542 | 3,863 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | -8,187 | -123,955 | -132,141 | -91,477 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | 23 | 24 | 48 | -3 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | -46,363 | 79,223 | 32,860 | 40,579 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | -8,973 | 39,830 | 30,857 | 61,413 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | -17,389 | 43,044 | 25,655 | 13,563 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | -2,758 | -16,085 | -18,894 | -4,449 |
| | - Kodi Iliyolipwa | -4,648 | -3,590 | -8,238 | -6,703 |
| | - Mengineyo (bainisha) | 2,589 | -2,715 | -76 | - |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **-77,734** | **25,344** | **-52,390** | **23,095** |
| **II:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | -1,362 | -1,448 | -2,810 | -1,901 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 26 | 33 | 59 | 84 |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **-1,336** | **-1,415** | **-2,751** | **-1,817** |
| **III:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | 37,920 | 37,920 | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | -545 | 439 | -105 | 18,216 |
| | Mengineyo (bainisha) | -1,613 | 988 | -625 | -10,841 |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | **-2,158** | **39,348** | **37,190** | **7,376** |
| **IV:** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | -81,228 | 63,277 | -17,951 | 28,654 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 335,651 | 272,375 | 272,375 | 170,472 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 254,424 | 335,651 | 254,424 | 199,126 |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI 2019

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mabadiliko thamani katika amana zinazouzika | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 7,390 | 75,487 | 137,761 | 0 | 5,719 | 2,267 | 228,624 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 10,996 | - | - | - | 10,996 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | -444 | -444 |
| Miamala na wanahisa | 1,010 | 36,910 | - | - | - | - | 37,920 |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | -12,707 | 12,707 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | -1,414 | - | 1,414 | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | -180 | -180 |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,400** | **112,396** | **134,637** | **12,707** | **7,133** | **1,643** | **276,916** |
| " **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 7,390 | 75,487 | 131,372 | 2,496 | 4,648 | 4,463 | 225,855 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 16,221 | - | - | - | 16,221 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | -2,448 | -2,448 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 1,424 | -2,496 | 1,072 | - | 0 |
| Mengineyo | - | - | -11,256 | - | - | 253 | -11,003 |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **7,390** | **75,487** | **137,761** | **0** | **5,719** | **2,267** | **228,624** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2019

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

| ***Jina na Cheo*** | ***Saini*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|
| Ken Cockerill **(Ofisa Mtendaji Mkuu)** | | 26-Jul-19 |
| Lydia Kokugonza **(Mkuu wa Fedha)** | | 26-Jul-19 |
| Jonathan Ngoma **(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)** | | 26-Jul-19 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| ***Jina*** | ***Saini*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|
| 1. Prof. Marck Mwandosya **(Mwenyekiti wa bodi)** | | 26-Jul-19 |
| 2. Nada Margwe **(Mjumbe wa bodi)** | | 26-Jul-19 |

TANGAZO

# STANBIC BANK TANZANIA LIMITED

## DISCLOSURE MADE UNDER REGULATION 11 OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATION, 2015

## MINIMUM DISCLOSURE OF BANK CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)

| No. | Item/Transaction | Charges/Fees TZS | Charges/Fees USD |
|---|---|---|---|
| **1.0** | **Current Accounts** | | |
| a) | Required Minimum balance | 0 | 0 |
| b) | Monthly Service/Management Uhuru Banking | FREE | FREE |
| c) | Monthly Service/Management Private banking PAYT | 29,500 | 17.70 |
| d) | Monthly Service/Management Fees Private banking Bundle | 53,100 | 31.86 |
| e) | Monthly Service/Management Fees Biashara Direct segment | 15,000.01 | 10.62 |
| g) | Monthly Service/Management Fees SME banking segment | 35,400 | 21.24 |
| h) | Monthly Service/Management Fees Commercial banking segment | 64,900 | 38.94 |
| i) | Monthly Service/Management Fees Non commercial Entities | FREE | FREE |
| j) | Monthly Service/Management Fees Corparate Banking | 48,000 | 20.00 |
| k) | Over the counter withdrawal fee(per segment and price option) | TZS 4 088 for amounts below 20M, 0.15% of value for amount above 20M max 125,000 | For FCY withdrawals - 1% min 8 |
| l) | ATM withdrawal fee own ATM | 950.01 | 0.96 |
| m) | ATM withdrawal fee other banks (local) | 1,000 - 400,000 =2,800<br>400,001-above=4,000 | 1,000 - 400,000 =2.8<br>400,001-above=4 |
| n) | ATM withdrawal fee International | 8,000.01 | TZS EQV |
| o) | ATM Mini Statement | 900.01 | 0.91 |
| p) | Interim Statement per page | 5,000 | 5.00 |
| q) | Periodic schedule statement | FREE | FREE |
| r) | Issue of cheque book | 450 per leaf | 0.46 per leaf |
| s) | Returned updaid Cheque( insuficient fund) | 100,000.01 | 100.01 |
| t) | Cheque payment to other bank | 950.01 | 0.96 |
| u) | Counter Cheque | 15,000 | 15.00 |
| v) | Stop Payment | FREE | FREE |
| aa) | Salary processing to staff banking with other bank(EFT) | 5,000 | 5.00 |
| ab) | Salary processing to staff banking with other bank(TISS) | 10,000 | Equivalent of 10 000 |
| ac) | Standing Order to 3rd partywithin stanbic | FREE | FREE |
| ad) | Standing Order to other banks local | 40,000.01 | 40.00 |
| ae) | Standing Order own account | FREE | FREE |
| af) | Balance enquiry (Over the counter) | 1,000 | 1.00 |
| ag) | ATM card issuance | FREE | FREE |
| ah) | ATM card replacement/Renewal | 25,000 | 25.00 |
| ai) | Unarranged Overdraft | 100,000 | 60.00 |
| aj) | Overdrawn Account interest charge | 36% | 21% |
| ak) | Interbank Transfer Normal | 5,000 | 5.00 |
| al) | Interbank Transfer Express (TISS) | 10,000 | Equivalent of 10 000 |
| am) | Interbank Transfer with stanbic | 5,000 | 5.00 |
| an) | Bill Payments through non branch channels( E channel) | FREE | FREE |
| ao) | Deposit fee | FREE | FREE |
| **2.0** | **Savings Accounts** | | |
| a) | Required minimum opening balance | 50,000 | 100.00 |
| b) | Monthly service fee (if balance breach minimum balance required) | 2,000 | 1.18 |
| c) | Interim statement | FREE | FREE |
| d) | Account closure | FREE | FREE |
| **3.0** | **Electronic banking** | | |
| a) | Internet banking monthly fee | FREE | FREE |
| b) | Internet transfers within own accounts STB | FREE | FREE |
| c) | Internet transfers 3rd party transfer STB | FREE | FREE |
| d) | Internet transfers other banks normal(EFT) | 2,000.01 | 2.01 |
| e) | Internet transfers other banks express(TISS) | 8,000.01 | Equivalent of 8 000.01 |
| g) | Bank to wallet | 1,000 - 50,000 =1,500<br>50,001 - 200,000 = 2,250<br>100,001 -250,000=3,000<br>250,001 - 400,000 = 3,7500<br>500,000 - 1,000,000=4,500 | N/A |
| h) | Balance and statement | FREE | FREE |
| i) | Air time top up | FREE | FREE |
| j) | SMS Banking | FREE | FREE |
| k) | Till to bank | 1.8% of the amount | 1.8% of the amount |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowlwdge and information

Signed by:

| | | |
|---|---|---|
| **Chief Executive Officer** | **K. Cockerill** | ............................................. |
| **Head, Personal and Business Banking** | **Ndadzungira, Brian B** | ............................................. |
| **Head, Corporate and Investment Banking** | **Manzi Rwegasira** | ............................................. |

| No. | Item/Transaction | Charges/Fees TZS | Charges/Fees USD |
|---|---|---|---|
| **4.0** | **Foreign Exchange Transactions** | | |
| a) | Purchase/Sale of TC's ttransactions over the counter | N/A | 1.475% min 43.66 |
| b) | Purchase of foreign cheque | 1.18% of the amount min 100 000, | 1.18% of the amount min 59, Max 236 |
| c) | Telegraphic transfer Inward | N/A | $10 |
| d) | Telegraphic transfer Outward | 0.3%. Min $50, Max 150 | 0.3%. Min $50, Max 150 |
| e) | TISS outward | 10,000 | 10 000 Equivalent |
| f) | TISS inward | FREE | FREE |
| g) | Cancellation of TT/Recall of funds | N/A | $75 |
| **5.0** | **Personal Loan** | | |
| a) | Processing/ Arrangement/ Appraisal fee | | |
| | (i) Personal Loans | 2.00% | 2.00% |
| | (ii) Overdrafts | 2% of the facility min 100 000. | 2% of the facility min $100 |
| | (iii) Mortgage Finance | 1.18% | 1.18% |
| | (iv) Asset Finance | 1.18% | 1.18% |
| b) | Early repayment | 3.0% | 3.0% |
| | Valuation fees | As per valuer | As per valuer |
| **6.0** | **Other Disclosures (Viambatanisho Vinginevyo)** | | |
| | Base/Prime Lending Rate | 21% | 10% |
| | Maximu spread over Base/Prime lending rate | 4.5% | 2% |
| **7.0** | **Deposit Rate (*subject to change from time to time*)** | | |
| | a) Fixed Deposits | | |
| | **TZS** | **+1BN** | **+1M** |
| | 1month | 3.00% | 1.20% |
| | 3months | 4.00% | 1.60% |
| | 6months | 5.00% | 1.80% |
| | 9months | 5.20% | 2.20% |
| | 12months | 5.50% | 2.50% |
| | b) Savings Account | 3.00% | 0.20% |
| | c) Current Account | Nil | Nil |
| **8.0** | **Trade Finance** | | |
| | a) Letters of Credit/Guarantee | | |
| | Establishment Fee - per quarter | Nil | 1% on establishment per quarter and part thereoff min $300 |
| | b) Documentary collection( clean bill) | Nil | $150 |

Stanbic Bank Moving Forward™

A member of Standard Bank Group

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Ongezeko la utalii lilete hamasa kuutangaza*

**ONGEZEKO** la idadi ya watalii wanaoingia nchini kama ilivyotangazwa na serikali ni habari njema kutokana na kuongezeka kwa pato la ndani la taifa na kukua kwa sekta ya utalii.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na serikali, watalii wanaoingia nchini wameongezeka toka milioni 1.3 hadi milioni 1.5 katika kipindi cha mwaka 2017/18.

Ongezeko hilo limesaidia taifa kupata pato la ndani la Dola za Kimarekani bilioni 2.4 (Sh. trilioni 4.5).

Kuingia kwa wingi kwa watalii nchini kunatokana na juhudi mbalimbali zinazofanywa na serikali na wadau wake kutangaza vivutio vya utalii wa Tanzania kupitia fursa mbalimbali wanazozipata wanapokuwa nje ya nchi na hata ndani ya nchi.

Tanzania imejaliwa kuwa na vivutio vingi vya utalii vinavyoweza kuwafanya watalii kujionea maajabu ambayo nchi nyingine duniani hayawezi kupatikana.

Siku za hivi karibuni Tanzania imeshuhudia watu maarufu mbalimbali wakiwamo wasanii wa filamu, marais wastaafu kutoka nchi kubwa duniani, wakija kushuhudia maajabu hayo kwa kujionea wenyewe badala ya kuangalia kwenye picha au sinema.

Utajiri wa vivutio vya utalii vilivyomo nchini umefanya hata nchi jirani kutumia ujanja na kuvitangaza ni vya kwao ili tu kuwavutia watalii waingie nchini mwao.

Fursa hii ya kipekee ya kuwa na wanyama, mimea, wadudu mbalimbali na vivutio vya kipee vilivyoumbwa na Mwenyezi Mungu, havina budi kutangazwa kwa nguvu zote ili mapato yanayotokana na utalii yaendelee kukua siku hadi siku.

Kwa mujibu wa Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Khamis Kigwangala, sekta ya utalii nchini inachangia asilimia 17.6 ya pato la taifa. Utalii wa wanyamapori umeelezwa kuendelea kuwa kitovu cha kivutio na hivyo kuifanya sekta hiyo kuongoza kuchangia pato la taifa.

Katibu Mkuu, Wizara ya Maliasili na Utalii, Profesa Adolf Mkenda, wakati akitoa taarifa ya takwimu za utalii ameeleza kuwa ukuaji wa watalii wanaoingia nchini ni mara mbili ya watalii wanaofanya utalii duniani.

Mwaka 2018, wizara hiyo kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Kamisheni ya Utalii ya Zanzibar na Idara ya Uhamiaji, ilifanya utafiti wa watalii wanaondoka nchini kwa lengo la kupata taarifa zitakazosaidia kuandaa akaunti za taifa na takwimu za mizania ya malipo ya nje.

Mapato yatokanayo na utalii yameongezeka kwa asilimia 7.2 hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 2.4 kutoka bilioni 2.3 zilizopatikana mwaka 2017.

Watalii waliokuja kwa ajili ya likizo na burudani walikuwa asilimia 62.6 na wameendelea kuwa na wastani mkubwa wa matumizi wa Dola 394.0 kwa siku.

Watanzania pia wamekuwa wakihamasishwa kujenga utamaduni wa kufanya utalii wa ndani kwa kutembelea mbuga za wanyama na vivutio mbalimbali vilivyomo nchini ili kujionea na kushawishi wengine kwenda.

Wageni kutoka nje wanajiwekea akiba hata kwa miaka miwili kwa lengo la kuja Tanzania kujionea vivutio, lakini Watanzania wenyewe wanashindwa hata kwa siku moja kutembelea vivutio hivyo.

Kwenda kujionea mwenyewe ni njia nzuri ya kuhamasisha mtu mwingine kwenda na kwa uhamasishaji huo utasaidia kuongeza mapato kwenye sekta ya utalii.

Inaelezwa kuwa watalii waliotembelea Tanzania walikaa kwa wastani wa siku 10 katika mwaka 2018, waliokuja kutembelea ndugu na jamaa walikaa kwa wastani wa siku 11.

Katika juhudi za kuitangaza sekta ya utalii, serikali inatarajia kuongeza matangazo ili kuvutia zaidi watalii na kufikia idadi ya watalii milioni tano kwa mwaka.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



## *Ugeni wa Rais Magufuli Nanenane Simiyu uchagize ununuzi wa pamba*

Na Raphael Kibiriti

**TAARIFA** za hivi karibuni kutoka kwa vyombo vya habari kwamba Rais John Magufuli anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye kilele cha Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima (Nanenane) mkoani Simiyu, zimemvutia Muungwana pia.

Kwa mujibu wa Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, maadhimisho ya sikukuu hiyo yanayoanza Agosti Mosi katika kanda zote nane nchini yakiwa ni maadhimisho ya 26 tangu kuanzishwa kwake, yatafunguliwa na Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Aidha, kwa mujibu wa taarifa hiyo, maadhimisho hayo yanayofanyika katika viwanja vya Nyakabindi, Bariadi, vilevile yatatembelewa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Agosti 3, ambaye atapata fursa ya kuona shughuli mbalimbali za wadau.

Muungwana anasema amevutiwa na taarifa hizo kwa sababu Rais Magufuli anakuwa mgeni rasmi katika kilele cha sikukuu hiyo ya wakulima mkoani Simiyu, katika kipindi ambacho wakulima wa zao la pamba bado wana kilio.

Wana kilio kwa sababu wengi wao wanaendelea kukabiliwa na changamoto ya kutonunuliwa kwa pamba yao takribani miezi mitatu sasa tangu msimu wa ununuzi wa zao hilo ulipozinduliwa Mei 2 mwaka huu.

Taarifa kutoka maeneo kunakolimwa pamba na hasa Kanda ya Ziwa, ukiwamo mkoa wa Simiyu ambako Rais Magufuli atakuwa mgeni rasmi katika kilele cha Nanenane zinaonyesha kwamba wanunuzi wa pamba ni kama 'wanapiga chenga.'

Kwamba pamoja na serikali kutoa kauli rasmi kupitia kwa Waziri Mkuu katikati ya mwezi huu kwamba kufikia Julai 30 pamba yote iliyoko katika mikoa inayolima zao hilo itakuwa imenunuliwa na wakulima wote kulipwa fedha zao, bado uhalisia wake hauko hivyo.

Muungwana anasema hivyo kwa sababu kwa mujibu wa taarifa kutoka maeneo mbalimbali, pamba bado imejaa kwenye bohari za Vyama vya Msingi vya Ushirika (AMCOS), kiasi kwamba nyingine ilikuwa inahifadhiwa nje.

Hata hivyo, pamba hiyo iliyoko kwenye bohari za AMCOS ni chache ikilinganishwa na ile ambayo bado iko majumbani kwa wakulima.

Ni kweli kwamba baada ya kauli ya serikali, baadhi ya kampuni zinazonunua zao hilo zimekuwa zikipeleka fedha kwenye vyama vya msingi, lakini kiasi kinachopelekwa ni kidogo, ikilinganishwa na pamba iliyokusanywa ambayo bado haijalipiwa.

Baadhi ya viongozi wa AMCOS wamemtaarifu Muungwana kwamba wanunuzi wanapeleka fedha kulingana na kiasi cha pamba ambayo tayari wameisafirisha kuipeleka kwenye viwanda vya kuchambua pamba kutoka AMCOS.

Na ndiyo maana hadi sasa vyama vingi vya msingi vinadaiwa na wakulima waliopeleka pamba yao kwenye bohari za vyama hivyo, huku wanunuzi wakiendelea kupeleka kiasi kidogo cha fedha kwa sababu ambazo hazijabainika.

Hili linatokea wakati ambapo Mwenyekiti wa Chama cha Wanunuzi Binafsi wa Pamba akiwa ameahidi mbele ya Waziri Mkuu kwamba baada ya serikali kukubali kuwadhamini wanunuzi ili wapate mikopo kutoka benki, wangenunua pamba yote ya wakulima.

Aidha, kuna taarifa kwamba kwenye baadhi ya vijiji, wanunuzi hawajafika kabisa hadi sasa na hivyo kufanya wakulima waendelee kubaki na pamba yao majumbani hadi sasa.

Na kutokana na kwamba siku zimeendelea kukatika bila ufumbuzi hadi sasa, baadhi ya wakulima walikuwa wameamua kupeleka pamba yao kwenye bohari za AMCOS, walau ikakae huko hadi pale fedha zitakapopelekwa.

Hatua hiyo ndiyo iliyosababisha baadhi ya bohari kujaa, na hivyo pamba nyingine kuhifadhiwa nje. Ni vizuri kwamba baadhi ya wakuu wa wilaya akiwamo wa Maswa, waliingilia na kuzuia wakulima kupeleka pamba kwenye bohari za Amcos, wakati hakuna fedha za kuwalipa.

Wakati Rais Magufuli akiwa mgeni rasmi kwenye kilele cha Maadhimisho ya Sikukuu hii ya Wakulima, Muungwana anatoa rai kwake kutatua sintofahamu hii, ili pamba yote ya wakulima inunuliwe.

Anatoa rai kwake akichukulia ukweli kwamba yeye ni mtu wa vitendo na mtetezi wa wanyonge wakiwamo wakulima wa pamba, kama alivyo kwisha jibainisha.

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
*benki kwa maendeleo yako*

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30.06.2019
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka Mwaka wa sasa 30-Jun-19 | Robo Mwaka Mwaka uliopita 31-Mar-19 |
|---|---|---|---|
| **A. MALI** | | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 12,455 | 11,596 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 12,491 | 17,668 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 22,920 | 19,715 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 384 | 111 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 112 | 18 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 0 | 0 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 89,971 | 82,623 |
| 12 | Mali Nyingine | 14,467 | 14,095 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 20 | 20 |
| 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 3,079 | 3,364 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **155,899** | **149,210** |
| **B. DHIMA** | | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 1,167 | 711 |
| 18 | Amana za Wateja | 110,887 | 112,647 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana Maalumu | 0 | 0 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 23 | 18 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 4,122 | 3,794 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 15 | 47 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 1,173 | 912 |
| 27 | Dhima Nyingine | 1,182 | 1,007 |
| 28 | Madeni | 15,023 | 8,000 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **133,591** | **127,136** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **22,308** | **22,074** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 8,607 | 8,607 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 7,400 | 6,778 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 371 | 217 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 5,930 | 6,472 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **22,308** | **22,074** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 490 | 978 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 21,313 | 20,752 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 14,849 | 15,728 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 1,459 | 1,459 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 14.3% | 14.8% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 20.1% | 20.7% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 92.8% | 86.5% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 68.0% | 67.1% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 72.7% | 68.7% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -1.2% | -4.5% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 4.5% | -3.9% |

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.06.2019
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka sasa 30-Jun-19 | Robo ya mwaka Linganishi 30-Jun-18 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-19 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30-Jun-18 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 7,246 | 6,997 | 14,205 | 14,967 |
| 2 Gharama za Riba | (1,295) | (1,416) | (2,478) | (3,073) |
| 3 **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **5,951** | **5,581** | **11,727** | **11,894** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (468) | (1,052) | (608) | (4,089) |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **1,894** | **1,842** | **3,767** | **3,897** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 109 | 59 | 157 | 56 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 1,435 | 1,649 | 2,967 | 3,394 |
| 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 6.4 Mapato Mengine | 350 | 135 | 643 | 448 |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | **(7,065)** | **(8,574)** | **(14,356)** | **(16,707)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (3,575) | (3,745) | (7,336) | (7,497) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 7.3 Gharama Nyingine | (3,490) | (4,830) | (7,020) | (9,210) |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **313** | **(2,202)** | **530** | **(5,006)** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | (159) | 0 | (159) | 0 |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **154** | **(2,202)** | **371** | **(5,006)** |
| 11 **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **154** | **(2,202)** | **371** | **(5,006)** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 448 | 466 | 448 | 466 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 18 | (256) | 43 | (582) |
| 15 **Idadi ya Matawi** | **18** | **18** | **18** | **18** |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.4% | -5% | 0.5% | -6% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 2.8% | -41% | 3.3% | -46% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 90.1% | 115% | 92.7% | 106% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 22.1% | 19% | 21.7% | 20% |

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30.06.2019
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Jun-19 | Robo Mwaka iliyopita 31-Mar-19 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-19 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30-Jun-18 |
|---|---|---|---|---|---|
| **I:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 313 | 217 | 530 | (2,202) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | - Hasara Katika Mali | 383 | 418 | 801 | 397 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (7,347) | 372 | (5,513) | 3,844 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | 0 | (5) | (5) | 4 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (1,304) | (5,400) | (6,705) | (7,900) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (3,205) | 6,855 | 3,945 | 1,235 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 7,759 | (895) | 6,865 | 2,031 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (373) | (697) | (2,827) | (1,153) |
| | - Kodi Iliyolipwa | 144 | 0 | 144 | 0 |
| | - Mengineyo (bainisha) | 321 | 58 | 379 | 769 |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | **(3,310)** | **924** | **(2,386)** | **(2,975)** |
| **II:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (320) | (186) | (506) | (158) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 0 | 5 | 6 | 0 |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mengineyo (bainisha) | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | **(320)** | **(181)** | **(501)** | **(158)** |
| **III:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mengineyo (bainisha) | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **IV:** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (3,630) | 743 | (2,887) | (3,133) |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 20,327 | 19,584 | 19,584 | 21,001 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **16,698** | **20,327** | **16,698** | **17,868** |

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30.06.2019
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2019** | **8,607,136** | **2,431,917** | **7,546,745** | **2,537,257** | **779,217** | **21,902,272** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 371,234 | 0 | 0 | 371,234 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | (114,812) | 149,646 | 0 | 34,834 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | (31,841) | 0 | 31,841 | - |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka 30.06.2019** | **8,607,136** | **2,431,917** | **7,771,325** | **2,686,904** | **811,058** | **22,308,339** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2018** | **8,607,136** | **2,431,917** | **12,981,019** | **694,193** | **843,314** | **25,557,579** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | (5,005,956) | 0 | 0 | (5,005,956) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | 662,715 | (694,193) | 0 | (31,478) |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 117,422 | 0 | (117,422) | 0 |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Salio la mwisho wa mwaka 30.06.2018** | **8,607,136** | **2,431,917** | **8,755,200** | **0** | **725,892** | **20,520,145** |

**BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.06.2019**

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

| ***Jina na Cheo*** | ***Saini*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|
| Augustine Akowuah **(Mtendaji Mkuu)** | | |
| Bertha Simon **(Mkuu wa Fedha)** | | |
| Chemo Mutani **(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)** | | |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| ***Jina*** | ***Saini*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|
| 1. Ernest Massawe | | |
| 2. Dr. Josephat Daniel Lotto | | |




215345502

# Membe akiri sauti

INATOKA UK. 2

wa anaifanya hiyo kazi, amesoma IT (teknolojia ya habari) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

"Tukamtafuta na kumkamata, kwa hiyo udukuzi si kwamba upo Tanzania tu, hata duniani upo, siyo sisi tu huku," alisema.

Siku chache baada ya makatibu wakuu wastaafu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abdulrahman Kinana na Yusuf Makamba kutoa waraka wakilalama kudhalilishwa na mtu anayejiita mwanaharakati huru, mawasiliano ya simu yenye sauti zinazodaiwa zao, yalisambaa kwenye mitandao ya kijamii.

Baadaye mawasiliano ya simu ya Membe yalisambazwa kwenye mitandao hiyo.

# Makonda aonya wachafu SADC

INATOKA UK. 3

wafanyabiashara kutoka SADC.

"Tabia ya kuja mjini hujafua, hujaoga usitutie aibu," Makonda alisema, "kama umezoea kuja mjini hujaoga wala kufua nguo, baki nyumbani walau huu mwezi wa nane uishe.

"Tunataka siyo usafi tu wa mazingira, usafi pia wa wananchi wetu, watu wamejaa chawa tu hapa."

Makonda pia aliwaonya wananchi wenye tabia ya kutupa taka ovyo wakiwa kwenye vyombo vya usafiri husussani daladala kuwa watashushwa chini na kupewa adhabu kali ikiwa ni pamoja na kufanyishwa usafi.

"Ule utaratibu wetu wa Lugalo tunauanza rasmi leo, haiwezekani wawe na nidhamu kwenye kile kipande cha kukaribia mita 200, 300.

"Kwa hiyo ule utaratibu wa mtu kwenye gari kutupa taka ovyo, mshusheni akikataa, chukueni namba yake ya gari tutamkamata ili aje apige deki," Makonda alisema.

Makonda alisema amewaandaa vijana wa jeshi na mgambo zaidi ya 430 watakaokuwa katika kila kona ya jiji hilo kwa ajili ya kufanya usafi na kuwachukulia hatua za kisheria wachafuzi wa mazingira.



Alisema kuweka jiji hilo katika hali ya usafi ni kuonyesha ubora wa wananchi wa jiji hilo na kuitaka mikoa mingine kuiga mfano huo.

Alisema ifikapo Agosti 5, jiji hilo linapaswa liwe safi kwa ajili ya mapokezi ya wageni na akawataka maofisa mazingira kuhakikisha miti yote inayopandwa inaota kwa sababu serikali imekuwa ikitenga bajeti kubwa na pesa hizo hazionyeshi matunda na mazingira chanya kama inavyokusudiwa.

Makonda pia aliwataka vijana wa usafishaji kuhakikisha dereva wa gari akitupa taka ovyo, anapigishwa deki kwa kupewa kipande cha barabara badala ya kuwapiga faini za pesa na watendaji wa mitaa husika kuhakikisha maeneo yao yanakuwa safi vinginevyo watapoteza ajira zao.

# Daraja refu zaidi kujengwa

INATOKA UK. 2

magari 10,200 kupita kwa siku na litapunguza urefu wa Km 183 za barabara zilizokuwa zinatumiwa na waendesha magari kwenda nchi za Uganda, Rwanda, Burundi.

Alisema kukamilika kwa daraja hilo kutawezesha magari kutumia muda wa dakika nne kuvuka, kulinganisha na sasa ambapo wananchi wanatumia muda wa saa mbili kusubiri kivuko.

"Kukamilika kwa daraja hili kutachochea shughuli nyingi za uchumi, shughuli za utalii zitapanuka, litadumu kwa muda wa miaka 120, litakuwa na uwezo wa kubeba tani 180 kwa wakati mmoja, litakuwa na nguzo 67 na umbali kutoka nguzo moja hadi nyingine ni mita 60," Mfugale alisema.

Alisema zabuni ya ujenzi wa daraja hilo ilitangazwa Desemba mwaka jana na Kampuni za CCE na Railway15 zilishinda.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Robert Gabriel, alisema kukamilika kwa daraja hilo kutakuwa ukombozi kwa wakazi wa Kanda ya Ziwa, litaokoa maisha ya wakazi wa Geita na litaleta manufaa ya kiuchumi na kiusalama kwa wakazi wa Geita.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongela, alisema mkoa huo ni kiungo cha nchi za Afrika Mashariki, hivyo kukamilika kwa daraja hilo kutaleta maendeleo chanya kwa wakazi wa Afrika Mashariki.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Hawa Mchafu, alisema kamati itaendelea kumuunga mkono Rais John Magufuli katika ujenzi wa miundombinu.

Naye Mbunge wa Misungwi, Charles Kitwaga, alisema: "Tunamshukuru Rais Magufuli kwa kuamua kutujengea daraja hili, daraja hili litatoa fursa kwa wananchi wote wa Afrika Mashariki na kati," alisema.

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isaac Kamwelwe, alisema ujenzi wa daraja hilo unatarajiwa kutoa ajira za kudumu 1,000 na za muda 10,000.

Alisema wakazi wa mikoa ya Geita, Kagera na Shinyanga watakuwa wanavuka kwa urahisi kwenda kupata huduma mkoani Mwanza.

# Shahidi adai mtoto alichapwa na kunyong'onyea

**Na Hellen Mwango**

SHAHIDI wa utetezi Jaqline Kesi (25), ambaye ni mtoto wa mshtakiwa amedai mahakamani katika kesi ya mauaji ya Naomi John (7), kwamba siku ya tukio mtoto huyo kabla ya kuchapwa na mshtakiwa, alikuwa amelegea na alipomchapa alinyong'onyea zaidi.

Kadhalika alidai kuwa baada ya Naomi kuishiwa nguvu zaidi alimwona mama yake (mshtakiwa) akimmwagia maji ya moto katika vidonda, hali iliyomfanya aishiwe nguvu zaidi.

Ushahidi huo ulitolewa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyopewa mamlaka ya kusikiliza kesi za mauaji iliyoketi chini ya Naibu Msajili, Pamela Mazengo.

"Mama yetu alikuwa mkali sana na alikuwa akimfanyia ukatili sana Naomi," alidai shahidi kupitia maelezo yake ya onyo aliyoyatoa kituo cha polisi Maturubai Mbagala, mkoa wa kipolisi Temeke.

Jaqline alitoa ushahidi huo wakati upande wa Jamhuri ulipopewa nafasi ya kumhoji shahidi huyo wa pili wa utetezi na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Cecilia Mkonongo.

Shahidi huyo ambaye pia ni mtoto wa mshtakiwa alidai kuwa baada ya mama yake kumchapa Naomi alikwenda duka la dawa, lakini akashauriwa ampeleke hospitali.

Alidai kuwa alimbeba mgongoni wakaomba msaada wa gari kwa jirani na wakiwa njiani alimsikia Naomi akishusha pumzi kwa nguvu na kisha akatulia.

Katika utetezi wake, Ester Lyimo (41), alidai kuwa alimchapa mtoto huyo (wakati wa uhai wake) na fimbo ya mparachichi, lakini alimwachia na kumlaza barazani baada ya kuona mwili wake umelegea.

Vile vile, alidai kuwa alipoona mwili wa Naomi umelegea alimlaza barazani na alikwenda duka la dawa kununua glucose kwa ajili ya kumnywesha mjukuu wake.

Akiongozwa na Wakili wa Utetezi Wilson Mafie, shahidi huyo alidai kuwa siku ya tukio alirudi nyumbani majira ya asubuhi akitokea kufanya usafi wa mtaa.

Alidai kuwa alipofika alipokea mashtaka kutoka kwa Andrew John (9), kwamba Naomi amejikojolea, tangu ameamka amekaa na hajafanyakazi yoyote.

"Kila mtu alikuwa na eneo lake la kufanya usafi, Andrew na Naomi, lakini siku hiyo Naomi hakufanya usafi nilimkuta amekaa nikamsalimia akanyamaza nikaingia ndani nikasema nikitoka nje nikute amepiga mswaki," alidai na kuongeza:

"Nilipotoka nilimkuta anachezea maji nikakata fimbo kwenye mti wa mparachichi nikamchapa kumwonya kama mzazi, lakini nilishangaa kumwona analegea nikajua anatania au anafanya jeuri nilipoona anazidi kunyong'onyea nikamlaza barazani nikaenda dukani kununua glucose, nikaona amezidi kulegea nikampeleka hospitali Temeke," alidai mshtakiwa huyo.

# Ofisa Nida matatani

INATOKA UK. 2

nadaiwa kutaka kumhonga Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, Sh. milioni 1.2 ili asitekeleze majukumu yake.

Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa Kabunga baada ya kuhojiwa, amekiri kuhusika na kitendo hicho na hatimaye kufikishwa mahakamani.

Pia alisema mfanyabiashara Bahadur Hijri (68) na mtoto wake, Nahid Hijri (33) ambaye ni mhasibu wa Victory Bookshop Ltd ya jijini hapa, wamefikishwa mahakamani kwa tuhuma za kutaka kumhonga mkuu wa wilaya.

Alisema watuhumiwa hao walinaswa Jumamosi iliyopita majira ya saa 11 jioni katika Hoteli ya Royal Village. Kibwengo alisema watuhumiwa hao waliahidi na kutoa hongo ya kiasi hicho cha fedha kwa Katambi ili asifuatilie upungufu katika utekelezaji wa amri ya Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya juu ya kukazia hukumu iliyowasilishwa kwa mfanyabiashara huyo na dada yake.

"Baada ya kupata taarifa ya watuhumiwa kuahidi kutoa fedha hizo kama kishawishi kwa mkuu wa wilaya, tulianza kufuatilia na kufanikiwa kuwakamata baada ya mtuhumiwa Nahid kumkabidhi Katambi huyo rushwa hiyo," alisema.

Alisema watuhumiwa hao wametenda kosa hilo kinyume na kifungu cha 15(1)(a) na (b) vya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007.

**WALIMU NAO WANASWA**

Mkuu huyo wa Takukuru alisema walimu wawili wa Shule ya Sekondari Viwandani, Venance Mayo (34) na Sulaith Rusheke (33) wamefikishwa mahakamani kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 20,000 ili wampatie cheti cha utambulisho wa kumaliza shule mtoa taarifa aliyekuwa mwanafunzi wa shule hiyo.

Alisema mwanafunzi huyo (jina linahifadhiwa), alipotaka kuomba kozi fupi katika taasisi fulani, alitakiwa awasilishe cheti hicho, hivyo akaenda shuleni hapo na ndipo watuhumiwa wakamtaka awape rushwa.

"Watuhumiwa wanajua kabisa ni kinyume cha utaratibu lakini walitaka rushwa ili wampatie cheti hicho na ndipo akatoa taarifa kwetu. Tulipofuatilia tuliwakamata majira ya 4:30 asubuhi Julai 26, mwaka huu," alisema.

Alibainisha kuwa mtuhumiwa Mayo alikamatwa akiwa kwenye bajaj yenye namba ya usajili MC686 BHK iliyoegeshwa nje ya uzio wa shule baada ya kupokea hongo hiyo na kumkabidhi mhusika cheti.

"Mtuhumiwa alikwenda katika eneo hilo akiwa na muhuri wa Mkuu wa Shule na cheti husika na alikigonga muhuri na kumpatia mtoa taarifa wetu baada ya kupokea fedha hiyo. Baada ya hapo tulimkamata pia Rusheke kwani alishiriki katika kushawishi hongo hiyo," alisema.

**MAOFISA WATENDAJI**

Pia alisema Takukuru inamshikilia msaidizi wa Mtendaji wa Kata ya Makutupora, Omary Mtauka, kwa kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 110,000 kutoka kwa Mzee Paulo Mawope (78) ili amalize tuhuma dhidi yake za kugombana na jirani, zilizowasilishwa kwa mtendaji wa mtaa na ofisi ya kata.

"Tulipokea taarifa kutoka kwa mjukuu wa mzee huyo kwamba alipigiwa simu na 'mtendaji wa kata ya Makutupora' akitakiwa kutoa fedha hizo ili babu yake aliyekuwa ameshtakiwa katika ofisi ya kata aachiwe," alisema.

Kibwengo alisema uchunguzi wao ulithibitisha uwapo wa suala la mzee huyo kushtakiwa na jirani yake, kushikiliwa na kutakiwa kutoa fedha ili suala hilo limalizwe.

"Tulifanikiwa kumnasa mtuhumiwa baada ya kupokea hongo hiyo Julai 25 katika baa ya Mama Lilly iliyoko Makutupora na tulibaini mtuhumiwa ni msaidizi wa mtendaji wa kata ya Makutupora na alikamilisha uhalifu wake kwa kujifanya ni mtendaji wa kata," alisema.

# Wazee walalamikia uhaba wa dawa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAZEE wanaoishi Wilaya ya Shinyanga Vijijini mkoani hapa, wamelalamikia uhaba wa dawa kwenye zahanati na vituo vya afya wilayani humo hali inayowafanya kukosa huduma bora za matibabu.

Hayo yalibainishwa juzi na Katibu wa Baraza la Wazee wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini, Boniface Boaz, wakati akisoma taarifa ya wazee hao kwenye kikao cha Shirika la Kutetea Haki za Wazee mkoani Shinyanga (TAWLAE), kilichohusisha pia maofisa wa ustawi jamii, maendeleo, mganga wa halmashauri hiyo na mkurugenzi.

Alisema changamoto kubwa wanayokabilia nayo ni ukosefu wa matibabu bora kwa kuwa wanapokwenda kupatiwa matibabu kwenye zahanati na vituo vya afya huambiwa hakuna dawa bali wakanunue huku wakiwa hawana uwezo huo na kuamua kujitibu kienyeji.

"Tunaomba serikali itutatulie tatizo hili la uhaba wa dawa kwenye zahanati na vituo vya afya Shinyanga Vijijini, ikiwa sisi wazee tunapata tabu sana na ikizingatiwa hatuna uwezo wa kifedha kwenda kununua dawa kwenye maduka ya watu binafsi, pia tutengewe na madirisha yetu maalumu pamoja na madaktari bingwa wa magonjwa ya wazee," alisema Boaz.

"Pia tunaomba tupatiwe na vitambulisho vya matibabu bure kwa wazee, kwenye halmashauri yetu ya Shinyanga Vijijini tuna jumla ya wazee 12,922, lakini wenye vitambulisho ni 5,563 na waliosalia hawana, hivyo imekuwa ikiwapatia ugumu wa kupata matibabu kutokana na kutokuwa na vitambulisho," aliongeza.

Naye Mganga Mkuu wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Amosi Mwenda, alitoa ufafanuzi wa suala hilo, kuwa kuna baadhi ya dawa haziruhusiwi kuwapo kwenye zahanati na vituo vya afya, hivyo wazee wanapoambiwa wakanunue au waende hospitali ya wilaya na mkoa mahali zilipo ndipo hudai hakuna dawa.

Pia alitoa ufafanuzi suala la utengwaji madirisha ya wazee kuwa linatokana na uhaba wa watumishi na kwenye halmashauri hiyo kuna uhaba wa watumishi wa afya asilimia 68 wakiwamo na madaktari bingwa kwa magonjwa ya wazee, walichokifanya ni kuandika vibao vya mzee apewe kipaumbele kwenye matibabu.

Vile vile, Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo ya Shinyanga Vijijini, Hoja Mahimba, alisema changamoto zote hizo za wazee atazifanyia kazi ikiwamo kuwapatia vitambulisho vya matibabu bure, kwa mwaka huu wa fedha (2019-20) zimeshatengwa Sh. 4,750,000 kwa ajili ya ukamilishaji wa vitambulisho 7,359.

# Miradi ya bilioni 12/- kukaguliwa Kisarawe

**Na Beatrice Shayo**

MKUU wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo, amesema miradi minne yenye thamani ya Sh. bilioni 11.6 itakaguliwa wakati wa mbio za Mwenge wa Uhuru katika wilaya hiyo.

Mwegelo aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati alipokuwa akipokea Mwenge huo na kusema katika Wilaya ya Kisarawe utakimbizwa umbali wa kilometa 103.1

"Mwenge wa Uhuru utaweka jiwe la msingi katika miradi miwili, kukagua miradi miwili na kuzindua miradi miwili. Pia katika eneo la mkesha Mwenge wetu utatembelea mabanda ya Ukimwi, malaria, dawa za kulevya na rushwa," alisema.

Alisema jumla ya miradi hiyo imegharimu kiasi cha Sh. bilioni 11.67 katika fedha hizo wananchi wamechangia Sh. milioni 10.82, halmashauri Sh. milioni 2.4, Serikali Kuu imechangia Sh. bilioni 10.6 na sekta binafsi imechangia Sh. milioni 996.

**Ripoti ya ubora wa nondo ilikosekana, kiongozi wa mbio za Mwenge ametuagiza tulifuatilie jambo hilo na pia kuna majengo ambayo hayajakamilika.**

Vile vile, alisema maji ni haki kwa kila mtu, hivyo ni muhimu kutunza vyanzo vyake na wakumbuke kushiriki katika uchaguzi wa serikali za mtaa.

"Lengo la ujumbe huu ni kuelimisha, kuhimiza na kusisitiza umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji kuendeleza utoaji wa huduma za maji, kuendeleza vyanzo vya maji, kuongeza maeneo ya utoaji wa maji katika vyanzo vya maji, kuibua vyanzo vipya vya maji, kutekeleza miradi mipya ya maji na kuendelea kuhamasisha wananchi kushiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa," alisema.

Vile vile, alisema Mwenge wa Uhuru unaendelea kuwakumbusha wananchi mapambano dhidi ya ugonjwa wa Ukimwi, rushwa pamoja na dawa za kulevya.

Alisema wataendelea kuwahamasisha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo katika maeneo yao bila kujali dini, kabila, rangi au mlengo wa chama cha siasa ili kuendana na dhana ya ushirikishwaji. Mkuu wa Wilaya ya Mafia, Shaibu Nntunduma, akikabidhi Mwenge huo, alisema walifanikiwa kukagua miradi minane na miwili ilikuwa ina shida.

"Miradi miwili haikuweza kufunguliwa kwa sababu thamani ya hela haina uhalisia kwa kuwa fedha iliyotumika ni nyingi, kiongozi wa mbio za Mwenge aliagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), kufanyia kazi suala hilo," alisema.

Alisema katika mradi wa barabara ulioibuliwa na wananchi Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (Tarura) walikwenda kutengeneza karavati ambalo walitakiwa kuonyesha taarifa ya ubora wa nondo walizotumia, lakini hawakuonyesha hiyo ripoti.

"Ripoti ya ubora wa nondo ilikosekana, kiongozi wa mbio za Mwenge ametuagiza tulifuatilie jambo hilo na pia kuna majengo ambayo hayajakamilika," alisema.



Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania Plc, Hisham Hendi, akieleza jambo kwa baadhi ya washiriki wa kongamano la Corporate Unwind lililoandaliwa na Smart Codes. Kongamano hilo lilikutanisha wadau mbalimbali kutoka sekta ya biashara na uvumbuzi pamoja na wafanyabiashara, taasisi na kampuni mashuhuri nchini Tanzania. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Makinda awaasa madiwani wanawake

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

SPIKA mstaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Anne Makinda, amewataka wabunge na madiwani wa viti maalum nchini kusimamia kikamilifu rasilimali za umma ili ziwanufaishe wananchi wote.

Akizungumza jijini Mwanza mwishoni mwa wiki katika semina ya kujenga uwezo kwa viongozi wanawake wa Serikali za Mitaa (WASEMI), iliyoandaliwa na Shirika la TGNP Mtandao, Makinda, alisema, mchango wa wabunge na madiwani wa viti maalum umekuwa hauonekani vizuri au kutambuliwa na jamii kutokana na wao wenyewe kuwa na hofu au kutokujiamini kitu ambacho kimechangia kuwarudisha nyuma na kushindwa kuendelea mbele.

"Tatizo letu sisi viongozi wanawake, tunajenga hofu, tunaogopa sana kujitokeza na kuwajibika vizuri kwa wananchi, eti kwa sababu ni viti maalum. Sisi tulianzia pia viti maalum, lakini tulipata nafasi ya kwenda jimboni kwa sababu tulijiamini, tuliwajibika kikamilifu na tulihakikisha uwezo wetu unaonekana na kila mmoja. Jitokeze, kwa wananchi, watumikie kwa uadilifu na watakuona na kutambua mchango wako," alisema Makinda.

Aliwaasa wanawake viongozi wa serikali za mitaa, kuhakikisha wanasimamia ubora wa huduma za jamii kwenye halmashauri zao na kila kinachofanyika kwenye halmashauri wanakielewa vizuri na kutoa taarifa kwa wananchi wote.

Awali, akizungumza Mwenyekiti wa WASEMI, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, Kibena Kingo, alisema WASEMI itahakikisha wenyeviti wa halmashauri wanawake wanaonyesha mfano bora wa utendaji uliotukuka kwenye halmashauri zao hasa kutokomeza rushwa, ubadhirifu wa mali za umma na kuhakikisha kila senti iliyopangwa kwa ajili ya kuboresha maisha ya wananchi inatumika vizuri.

Mkutano huu pia ulihudhuriwa na Mwenyekiti wa Umoja wa Serikali za Mitaa (ALAT), Gulamhafeez Mukadam na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Makazi, Anjelina Mabula ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Ilemela jijini Mwanza.

Tanzani ina Halmashauri 185, kati ya hizo, wanawake wanaoongoza halmashauri ni watano pekee.

# HHRD yaipatia Ruangwa vifaa tiba vya mil. 250/-

**Na Said Hamdani,** RUANGWA

SHIRIKA lisilo la Kiserikali la Helping Hand for Relief and Development (HHRD) la nchini Marekani limeipatia Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi, vifaa tiba vya Sh. milioni 250.

Vifaa hivyo vimekabidhiwa kwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ambaye pia ni Mbunge wa Ruangwa.

Msaada huo ni pamoja na vitanda vya kujifungulia, mashine za matibabu, magodoro na vifaa vingine vya huduma za afya.

Mwenyekiti wa Bodi wa Shirika hilo, Yassir Awadhi, alisema kwa kutambua juhudi zinazofanywa na serikali, uongozi umeamua kuunga mkono kwa kuchangia kile kidogo walichonacho, ili kiweze kusaidia kuboresha masuala ya afya kwa wananchi.

**Msaada huo utakaogaiwa kwa vituo vyote vya afya na zahanati, utapunguza usumbufu kwa wananchi wenye matatizo kutafuta huduma za matibabu mbali na maeneo wanayoishi.**

"Sisi HHRD ni wadau wa maendeleo na ni mashuhuda wa namna ambavyo ina mkakati kuibadilisha Tanzania na inasonga mbele katika sekta zote, viwanda, afya na elimu," alisema.

Alisema msaada huo utasaidia kuboresha huduma za afya kwa wananchi wa Wilaya ya Ruangwa na Tanzania kwa ujumla bila ya kujali itikadi za vyama, huku akisisitiza kuendelea kushirikiana na serikali kwenye mambo ya maendeleo.

Pia, alisema shirika hilo linafanyakazi katika nchi 16 za Afrika, ofisi ndogo ikiwa jijini Nairobi, nchini Kenya na inajishughulisha zaidi kupunguza changamoto za kijamii, ikiwamo watoto yatima, sekta ya afya, elimu na matukio ya dharura.

Alisema kwa Tanzania, Shirika hilo linajihusisha katika miradi mbalimbali, ikiwamo msimu wa ugawaji nyama na chakula kwa jamii kipindi cha mafuriko na cha mahujaji wanaoenda hija.

Awadhi alisema HHRD kwa sasa linahudumia yatima 250 kwa Wilaya ya Kisarawe, mkoani Pwani kwa kuwapatia mahitaji muhimu, ikiwamo kulipiwa gharama za shule, vifaa, sare, vitabu, makazi, chakula na nguo, upimaji afya, mafunzo na malezi kwa wazazi na walimu.

Waziri Mkuu, alilipongeza shirika hilo kwa msaada huo, huku akiendelea kuwaomba wadau wengine kujitokeza kuunga mkono jitihada zinazofanywa na serikali katika kuhudumia Watanzania.

Alisema msaada huo utakaogaiwa kwa vituo vyote vya afya na zahanati, utapunguza usumbufu kwa wananchi wenye matatizo kutafuta huduma za matibabu mbali na maeneo wanayoishi.

Waziri Mkuu Majaliwa yupo jimboni kwake Ruangwa kwa mapumziko mafupi.




Naibu Waziri wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mhandisi Stella Manyanya (kushoto), akishikana mikono na Ofisa Huduma kwa Wateja wa Benki ya NBC, Hilaria Mhagama alipotembelea banda la Benki ya NBC wakati wa Maonyesho ya Viwanda na Kongamano la Uwekezaji Ruvuma, ambapo NBC ilikuwa ni mmoja ya wadhamini. Wa pili kushoto ni Meneja wa Benki ya NBC Tawi la Songea, Simon Ntwale na Ofisa Mauzo wa benki hiyo, Jennifer Peter. **NAMPIGAPICHA WETU**

# EPZA yataka Ruvuma kuweka mazingira wezeshi

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Ukanda Maalum wa Uwekezaji nchini (EPZA) imeuhimiza Mkoa wa Ruvuma kuweka mazingira wezeshi ili kuwavutia wawekezaji kuchangamkia fursa zinazoweza kuufanya mkoa huo kuwa moja ya maeneo yenye viwanda vingi nchini.

Kauli hiyo ilitolewa jana mkoani hapa na Mkurugenzi Mkuu wa EPZA, Kanali mstaafu Joseph Simbakalia, wakati akiwasilisha mada wakati wa uzinduzi wa mwongozo wa uwekezaji mwishoni mwa wiki.

Alisema kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda ikiwa pamoja na miundombinu muhimu kama barabara, umeme na maji, ni hitaji muhimu kwa kuwa kila mwekezaji hupenda kujua kabla ya kufanya uamuzi wa kuwekeza.

"Mkoa wa Ruvuma kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2016, ulikuwa kati ya mikoa 11 iliyokuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa.

"Mkoa huu umebarikiwa kuwa na vivutio na fursa nyingi kitu ambacho kinafanya Mkurugenzi Mkuu wa EPZA kusisitiza umuhimu wa mkoa kuweka mazingira wezeshi ili kuwavutia kwa wingi wawekezaji wazawa na wanaotoka nje," alisema.

Simbakalia alisema kuwa moja ya jukumu la msingi la mamlaka ni kuainisha maeneo ya uwekezaji, kumilikishwa kwa niaba ya serikali na kuwavutia wawekezaji.

"Jukumu hili halipaswi kutekelezwa na EPZA peke yake bali tunahimiza serikali za mikoa na wilaya kushirikiana kwa karibu katika kutenga maeneo na kuboresha mazingira ya biashara ili kusudio la ujenzi wa uchumi wa viwanda liende kwa kasi zaidi," alisema.

Alisema mwongozo huo uliozinduliwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, umelenga kuainisha fursa kubwa za uzalishaji na kupunguza utoaji habari za uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na wa nje.

# 'Tumieni maonyesho Nanenane kusajili biashara'

**Na Sabato Kasika**

WATANZANIA wametakiwa kutumia maonyesho ya Nanenane ya mwaka huu wa 2019 kusajili majina ya biashara, kampuni, alama za biashara, leseni za viwanda na za biashara ili waweze kufanya shughuli zao kwa ufanisi.

Wito huo ulitolewa juzi jijini Dar es Salaam na Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (Brela), Emmanuel Kakwezi, wakati akielezea jinsi Brela itakavyoshiriki katika maonyesho hayo. Kakwezi alisema, katika maonyesho hayo ambayo kitaifa yanafanyika mkoani Siminyu, Brela itasajili pia leseni za usafirishaji wa mifugo na mazao ya chakula ndani na nje ya nchi.

"Hii ni habari njema kwa wakazi wa mikoa ya Kanda ya Ziwa, ewe mwananchi njoo sasa usajili majina ya biashara, usajili kampuni, usajili alama za biashara na huduma za usajili wa hataza, usajili leseni za viwanda, usajili leseni za biashara," alisema Kakwezi.

Alisema Brela ina banda lake katika maonyesho hayo, hivyo Watanzania watumie Nanenane kusajili majina ya biashara, kampuni, alama za biashara, leseni za viwanda na za biashara ili waweze kufanya shughuli zao kwa ufanisi.

Vile vile alisema, Brela imejipanga kutoa elimu kuhusu shughuli zinazofanywa na wakala na watawashashiwi washiriki na raia watakaotembelea maonyesho hayo kuhusu umuhimu wa kurasimisha shughuli zao.

"Watanzania kurasimisha shughuli zao ambazo mara nyingi zimekuwa ni kwa matumizi ya nyumbani ni la muhimu na inawezekana baada ya kuwapa elimu watabadilika na kusajili shughuli zao ili ziweze kuwanufaisha," alisema.

Alisema Brela inataka kuona shughuli za kilimo, ufugaji na uvuvi zisiwe za kukidhi mahitaji ya nyumbani pekee bali ziwe za kibiashara na itaelekeza jinsi wanavyoweza kusajili kampuni na kuwasaidia namna ya kupata masoko.

"Kwa ujumla ni kwamba Brela tumejipanga vizuri, kwa kuwa tayari tuna mfumo wa kuuza bidhaa nje ya nchi, na tutatoa elimu hiyo ili Watanzania wajue ni jinsi gani wanaweza kuuza bidhaa zao nje ya nchi," alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, alisema taasisi, mashirika zaidi ya 300 yakiwamo ya umma na binafsi yamethibitisha katika maonyesho hayo yatakayofunguliwa na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan.

"Maonyesho ya Nanenane kitaifa mwaka 2019, yatakayofanyika viwanja vya Nyakabindi mjini Bariadi kuanzia Julai 29 hadi Agosti 8, wajasiriamali wataanza kuonyesha teknolojia, huduma na bidhaa zao," alisema Mtaka.

Aliwataka wajasiriamali, wafanyabiashara, wakulima, wavuvi, wafugaji kujitokeza kwa wingi kwa vile maonyesho hayo yenye kaulimbiu usemayo 'kilimo, mifugo na uvuvi katika ukuaji wa uchumi wa nchi' yameboreshwa.

# Watakiwa kuthamini na kuenzi utamaduni

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

WATANZANIA wametakiwa kuendelea kuthamini na kuzienzi mila, desturi na utamaduni uliopo katika jamii ili kuendelea kuzirithisha kwa vizazi vijavyo.

Ofisa Utamaduni wa Mkoa wa Arusha, Irene Ngao, alisema hayo juzi wakati akizungumza katika Siku ya Tamasha la Kanono la wanaumoja wenye asili ya Karagwe na Kyelwa, mkoani Kagera waishio Arusha.

Ngao alisema serikali inatambua uwapo wa mila na desturi mbalimbali zilizoko katika jamii, hivyo wanategemea zirithishwe zaidi kwa vizazi vilivyopo na vinavyokuja ili waendeleze na utaratibu huo na hatimaye zisahaulike katika jamii.

"Nasisitiza kila kabila liendelee kuenzi utamaduni na mila zake na tuhakikishe zinatuunganisha badala ya kutugombanisha kwani serikali nayo kwa upande wake inaendelea kufundisha somo la utamaduni shuleni ili kuhakikisha watoto wetu wanazitambua mila na desturi zilizopo," alisema Ngao.

Naye Mwenyekiti wa Umoja huo, Wilibald Ngambeki, alisema wamekuwa na utamaduni wa kufanya tamasha hilo kila mwaka na hilo ni tamasha la 23 kufanyika mkoani hapa.

Alisema lengo la kufanya tamasha hilo ni kuhakikisha watoto wanaozaliwa mjini wanazijua mila na desturi zao na kuhakikisha hazipotei.

Ngambeki alisema kila mwaka wamekuwa wakikutana na kuonyesha tamaduni zinazofanywa na jamii hizo na kuwapa fursa watoto wao kujionea masuala mbalimbali na kujifunza na kupitia tamasha hilo, wataendelea kuwarithisha watoto wao mila hizo.

"Kwa kweli utamaduni ni kitu muhimu sana kwani unasaidia kupunguza makali ya utandawazi, hivyo jamii kuendelea kujikita katika utamaduni wake na kuacha kuiga mambo ya utandawazi. Kila kabila liendelee kuenzi ili mila na desturi zisipotee," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya tamasha hilo, Barungo Augostino, alisema wamekuwa wakikutana kwa lengo la kutunza mila, desturi na utamaduni wao kwa kuwa asilimia kubwa ya watoto waliozaliwa mijini hawazijui na bila kufanya hivyo, hawatazitambua na badala yake zitaendelea kupotea.

# RC ataka biashara kufanywa saa 24

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, amewashauri wafanyabiashara wa Babati kufanya kazi saa 24 ili kuendana na kasi ya maendeleo yanayoletwa na serikali ya awamu ya tano.

Mnyeti alitoa ushauri huo juzi wakati akizungumza na wafanyabiashara kwenye mkutano ulioandaliwa kwa ajili ya kuzindua kitabu kinachoonyesha fursa za uwekezaji mkoani Manyara.

Alisema mkoa huo unabadilika ambaye haoni mabadiliko basi ni kipofu wa akili, kama si kipofu wa macho kwa sababu mbali na Arusha, Dar es Salaam na Mwanza, hakuna mji mwingine wenye taa za barabarani zinazowaka usiku kama ilivyo Babati.

"Wafanyabiashara kufanya biashara zenu saa 24 ni ruksa. Wewe nenda umpe taarifa Kamanda wa Polisi wa Mkoa, ili awaambie askari wake wakiwa doria wawe wanakulinda," alisema Mnyeti na kuongeza:

**Na mimi tukikutana huko mitaani usiku usiniambie vipi mkuu wa mkoa we chukua 50 zako na mimi nichukue 50 zangu, maana mimi kuwa RC si Yesu, mwingine tukikutana ananisalimia hataki kuniachia.**

"Na mimi tukikutana huko mitaani usiku usiniambie vipi mkuu wa mkoa we chukua 50 zako na mimi nichukue 50 zangu, maana mimi kuwa RC si Yesu, mwingine tukikutana ananisalimia hataki kuniachia," alisema.

Aidha, alisema kuna watu wengine wakimwona anatembea usiku wanashangaa, hivyo aliwataka kuacha kumshangaa sababu hana ukoo na Yesu, wamwache afanye hivyo kwa sababu mchana anakuwa kazini.

"Kinachonisikitisha sana ni kupanda cheo mapema sana. Kwa miaka hii 35 nimewahi mno, sasa hivi nikifukuzwa kazi au nikastaafu nitarudi kijijini na kuzeeka haraka," alisema.

Alisema hajui akifukuzwa kazi atarudi kufundisha na uzee na kama atarudi kufundisha, alidai wanafunzi watamcheka maana atakapokuwa anaandika ubaoni wengine watasema huyu aliwahi kuwa mkuu wa mkoa.

Pia alisema cheo kinachomfaa kwa miaka yake aliyo nayo ni ukuu wa wilaya ili aje apande taratibu huku akiwachekesha kuwa kilichomfanya apewe nafasi hiyo ni kuongeza makusanyo ya mapato alipokuwa Arumeru.

Alitumia fursa hiyo kuwataka wafanyabiashara kulipa kodi huku akitangaza Wilaya ya Simanjiro kuongoza kwa kulipa kodi, hivyo kumtangaza mkuu wa wilaya hiyo, Mhandisi Zephania Chaula kuwa mkuu wa wilaya bora ndani ya mkoa.

Mfanyabiashara Musa Machinga kutoka Simanjiro, alisema mazingira ni mazuri ya kufanyia biashara kwa kuwa hakuna utitiri wa kodi lakini shida ya wafanyabiashara ni kutotimiza wajibu wao.



Ofisa Madini Mkazi wa Mirerani, wilayani Simanjiro, Mkoa wa Manyara, Daudi Ntalima, akisoma hadidu za rejea za kamati ya kupitia mipaka na mitobozano ya machimbo ya madini ya Tanzanite juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wauzaji wa mbegu waweka mkakati

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

WAJASIRIAMALI wa mbegu nchini wameanza mkakati wa kuzalisha mbegu zinazokabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi na zinazoweza kuhimili ukame na kuleta mazao mengi.

Akizungumza jana katika Maonyesho ya Kilimo Teknolojia yaliyofanyika katika Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (Tari) Seliani, Meneja Mauzo wa Kampuni ya Seedco, Daniel Ulimboka, alisema wamefanya utafiti na kuja na mbegu bora ambazo zinahimili hali ya ukame licha ya uhaba wa mvua na bado zinaleta mavuno ya kutosha kwa mkulima.

"Tuna mbegu aina ya 'Tumbili 419' ambayo inafanya vizuri sana hasa katika kipindi hiki ambacho hakuna mvua za kutosha na wakulima bado wamekuwa wakipata mavuno na kufurahia kilimo," alisema Daniel.

Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Melchiory Temu, aliwataka watafiti kubuni teknolojia zinazoendana na mabadiliko ya tabia ya nchi ili kuwawezesha wakulima kupata mazao badala ya kupata hasara kutokana na mabadiliko ambayo yamekuwa yakisababisha athari na kushuka kwa uzalishaji.

Aidha, aliwataka wakulima kuondokana na kilimo cha mazoea ili kufanya kilimo chenye tija na kuwaletea manufaa wao na taifa kwa ujumla.

Mkurugenzi wa Baraza la Nafaka Afrika Mashariki, Gerald Masila, alisema wanafanya juhudi za kuwaunganisha wakulima na masoko ili kupata faida kutokana na kilimo chao na kujikwamua kiuchumi.

# Mfanyabiashara mbaroni kwa tuhuma wizi nondo

**Na Paul William,** MOSHI

JESHI la Polisi mkoani Kilimanjaro linamshikilia mfanyabiashara Daudi Audifas (48), mkazi wa Rau katika Manispaa ya Moshi, kwa tuhuma za kukutwa na nondo 270 nyumbani kwake.

Nondo hizo zinadaiwa kuibwa kutoka eneo la mradi wa ujenzi wa stendi ya mabasi ya Ngangamfumuni katika manispaa hiyo.

Kamanda wa Polisi mkoani Kilimanjaro, Hamisi Issah, alisema jeshi hilo pia linamhoji Meneja wa Kampuni ya Ulinzi inayolinda eneo hilo la mradi, Michael Jonas kwa kutokutunza kumbukumbu za wafanyakazi wake.

Serikali imetoa Sh. bilioni tisa kwa ajili ya ujenzi wa stendi hiyo ya mabasi yaendayo mikoani, unaotekelezwa na Kampuni ya Ujenzi ya Kimataifa ya CRJE (East Africa) Ltd, kwa mkataba wa miezi 24.

**Ni aibu serikali kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo halafu wanajitokeza wachache na kuihujumu.**

"Uchunguzi unaonyesha nondo zilizoibwa ni nondo za milimita 10 ziko 157, milimita 12 ziko 123, na milimita 16 ziko 106 ambazo ni mali ya kampuni ya ujenzi inayoitwa CRJE Company. Yuko mtuhumiwa ambaye tumemkamata ambaye anatuhumiwa kutoboa ukuta wa uzio kwa chini," alisema

Kwa mujibu wa Kamanda Issah, timu ya makachero pia imefanikiwa kumkamata mtuhumiwa Hubert Chandu maarufu kama Masumbuko, mkazi wa Rau Kalikacha.

Kwa mujibu wa Kamanda Issah, kampuni ya ujenzi iliyopewa zabuni ya kulinda eneo hilo, iliajiri walinzi watatu ambao bado wanatafutwa kutokana na kutoroka baada ya tukio hilo.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipotembelea na kukagua mradi huo wa kimkakati Julai 18, mwaka huu, aliagiza Jeshi la Polisi kuwasaka na kuwakamata watu hao ambao wanakwamisha ujenzi wa mradi huo.

Majaliwa akiwa katika eneo hilo la mradi alisema: "Ni aibu serikali kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo halafu wanajitokeza wachache na kuihujumu.

"Kama walinzi hao hawatapatikana, viongozi wa kampuni husika wakamatwe ili kutoa ushirikiano wa sehemu walipo wafanyakazi wao. Wananchi wa Moshi mmetukatisha tamaa, naagiza wasakwe popote walipo."

Manispaa hiyo ni miongoni mwa halmashauri bora za Tanzania 17 ambazo zimetia saini mkataba na serikali wa kupewa kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya kuanza miradi ya kimkakati.



Mtaalamu wa uhaulishaji wa migomba kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Tari-Tengeru, Dk. Ally Mbwana (kushoto), akitoa maelezo kwa Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Agness Hokororo (aliyevaa koti jeusi), kuhusu upandaji wa migomba kisasa alipotembelea shamba darasa la mradi wa migomba katika Kijiji cha Mengeni, Wilaya ya Rombo juzi. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Mbunge Chadema aipongeza serikali

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MBUNGE wa Viti Maalum, Lucy Owenya (Chadema), amesema uamuzi wa serikali wa kuanza kuijenga kwa awamu barabara ya Kiborloni-Old Moshi-Kikarara-Tsuduni kwa kiwango cha lami, utapunguza mateso wanayopata wananchi wa Old Moshi kutokana na ubovu wa barabara hiyo tangu uhuru.

Ujenzi wa barabara hiyo ambayo ni utekelezaji wa ahadi ya Rais John Magufuli, kwa sasa umesimama baada ya kutengenezwa kwa kiwango cha lami umbali wa kilomita moja.

Kutokana na umuhimu wa barabara hiyo kwa wakazi wa ukanda wa mlimani wa Old Moshi, Owenya jana aliiomba Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) kuangalia uwezekano wa kumalizia kipande kilichobaki katika bajeti mpya ya mwaka 2019/2020, ili kukamilisha kipande cha Km 10 ambacho ndiyo kero kubwa kwa wananchi hao.

"Kwanza niishukuru serikali kwa hatua iliyochukua ya kuijenga kwa lami, nimekuwa nikiisemea mara nyingi barabara hii tangu wakati wa serikali ya Rais mstaafu Jakaya Kikwete na nikaendelea kuipigia kelele hadi Rais John Magufuli aliposikia kilio cha wananchi wa Old Moshi na kuahidi kuijenga.

"Niiombe serikali imalizie kipande hicho kilichobakia ili kufungua fursa za utalii pamoja na uchumi kwa wenzetu wa Old Moshi ambao hawana kabisa barabara ya lami," alisema.

Mbunge huyo pia alisema ujenzi wa barabara ya Getifonga-Mabogini-Kahe katika eneo la Moshi Vijijini ambayo inatarajia kujengwa kwa kiwango cha lami hivi karibuni, ni faraja kubwa kwa wananchi wa Moshi Vijijini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa hivi karibuni na Mhandisi wa Tarura, Loisheyi Mollel, barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami kuanzia eneo la Getifonga/Mabogini hadi Chekereni kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 22.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Tarura itatumia zaidi ya Sh. bilioni 1.1 katika ujenzi wa barabara zenye urefu wa Km 674.52.

# Ataja siri kuongezeka tija uzalishaji maziwa

**Na Mary Mosha,** HAI

UBORA wa uhifadhi wa malisho mabichi ya mahindi kwa ajili ya chakula cha mifugo (sailage) ambao huruhusu kuhifadhi karibu viinilishe vyote vilivyo kwenye mimea, unatajwa kuongeza tija ya maziwa kwa asilimia 15.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Match Maker inayofanya kazi kwa karibu na Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV) linaloendesha mradi wa faida maziwa kwa wafugaji wa Wilaya za Hai na Siha mkoani Kilimanjaro, Peniel Uliwa, alisema jana kuwa teknolojia ya uhifadhi wa malisho mabichi yanayotokana na zao la mahindi inapunguza gharama kwa asilimia 100.

Uliwa alikuwa akizungumza wakati wa makabidhiano ya mitambo ya kuchakata malisho ya mifugo yenye thamani ya Sh. milioni 150 kwa vikundi sita vya vijana.

"Tunafikiri hii ni teknolojia sahihi ya kwenda nayo na si kitu kipya duniani, sehemu zote duniani inatumika. Mradi huu wa faida ya maziwa una lengo la kuhamasisha matumizi ya uchakataji wa vyakula vya mifugo hasa sailage za mahindi ambazo zitawasaidia vijana na kinamama katika kuongeza mnyororo wa thamani," alisema.

Alisema mitambo hiyo ina uwezo wa kuchakata tani 16 za malisho kwa shamba la ekari moja kwa saa na ambazo kitaalamu hulisha ng'ombe wawili au watatu kwa mwaka mzima.

Alisema mradi huu utawasaidia vijana wapatao 60 na asilimia 60 wakiwa ni vijana wa kike ambao waliopita kwenye mchujo wa kupata washiriki wa mafunzo hayo.

Awali, Mkuu wa Idara ya Mifugo ya Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Elia Machange, akizungumza na vikundi hivyo vya wafugaji wa ng'ombe wa maziwa alisema kama zoezi hilo litatekelezwa kwa mafanikio, linaweza kutoa fursa ya ajira kwa vijana na kina mama kujikwamua kiuchumi kutokana na mradi huo.

Mkurugenzi wa Shirika la SNV, Tomy Olesika, alisema katika jitihada zao za kuboresha biashara ya maziwa mkoani Kilimanjaro, wameweka mikakati ya pamoja na kutafuta ng'ombe bora na malisho bora.

"Tumeungana pamoja ili kuleta tija kwenye tasnia ya maziwa kwa kuboresha malisho na usafi, kwa sasa ng'ombe mmoja ana uwezo wa kutoa lita nane mpaka 10 kwa siku wakati awali ng'ombe wao wa kawaida walikuwa wakitoa lita moja au mbili kwa siku," Olesika alibainisha.

Akizindua mashine hizo, Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, aliwataka wataalamu hao kuhakikisha wanatoa elimu ya kutosha kwa wakulima na wafugaji kabla ya kuanza mchakato wa utengenezaji wa malisho hayo ili wasije wakakata mahindi shambani na kusababisha baa la njaa.

"Wataalamu hakikikisheni mashine hizi zinafanya kazi iliyokusudiwa, pia angalieni ujio huu wa teknolojia mpya usije ukasababisha baa la njaa kwa watu kukata mahindi yao," Sabaya alitahadharisha.

Nipashe
# TESA
Jumanne Julai 30, 2019
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Ukurasa 15



## Elimu ya Kujitegemea na Mwalimu Julius K. Nyerere

## JE, WAJUA?



Ukurasa 18

## Mradi UNICEF vitabu vya kidijitali fursa watoto wenye ulemavu Kenya




# ELIMU KUNUFAISHA WAFUGAJI MSALALA

Ukurasa 16

# ELIMU KUTOKA POLISI

## NAMNA INTERPOL INAVYOKUTANISHA POLISI DUNIANI



Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Robert Boaz. **PICHA: MTANDAO**

INTERPOL ni Shirikisho la Polisi Duniani lilioundwa mwaka 1923.

Shirikisho hili lina nchi wanachama 192 ikiwamo Tanzania, ambayo ilijiunga mwaka 1962.

Mwezi Septemba 2017, Visiwa vya St. Solomon na taifa la Palestina waliomba uanachama wa Interpol, pia wako mbioni kuanza kushirikiana na majeshi mengine ya polisi kama wanachama wengine wa shirikisho hilo.

Makao Makuu ya Shirikisho la Interpol, yapo Lyon nchini Ufaransa.

Dhumuni la kuanzishwa kwa Interpol ni kuyaunganisha majeshi ya polisi dunia nzima kushirikiana kupambana na uhalifu wa kitaifa na kimataifa ikiwamo uhalifu wa kuvuka mipaka.

Ofisi za Interpol Duniani zimegawanyika katika kanda na kwa Afrika, kanda hizo ni pamoja na Kanda ya Mashariki mwa Afrika, ambapo ofisi zake zipo Nairobi nchini Kenya.

Aidha, kuna Kanda ya Kusini mwa Afrika ambapo ofisi zake zipo Harare nchini Zimbabwe na Kanda ya Kati ya Afrika ambapo ofisi zake zipo Yaounde nchini Cameroon.

Vilevile kuna Kanda ya Magharibi ambayo ofisi zake zipo Abidjan nchini Cote d'Ivoire. Makao makuu ya kanda yanajulikana kama Regional Bureau "RBs".

Kwa upande wa nchi wanachama, ofisi hizi huunganisha nchi mwanachama wa shirikisho la polisi duniani ambazo zinajulikana kwa jina la NCBs na Makao Makuu ya Interpol Ufaransa.

Makao Makuu ya Interpol Tanzania yapo Dar es Salaam kwenye Jengo la Makao Makuu ya Polisi.

Kwa kawaida kitengo cha Interpol huwa ndani ya Jeshi la Polisi chini ya Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai.

Mkuu wa kitengo hiki huwa ni Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai na husaidiwa na Mkuu wa NCB ambaye ndiye mtendaji wa shughuli za kila siku za kitengo hiki na ambaye kwa sasa ni Naibu Kamishna wa Polisi (DCP) Daniel Nyambabe.

Tanzania ni mwanachama wa Interpol, pia kutokana na sababu za kijiografia na kihistoria Tanzania ni mwanachama wa kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Kazi kubwa ya Interpol ni kupokea na kutuma taarifa za uhalifu na wahalifu wanaotafutwa ndani na nje ya nchi. Pia inapobidi Interpol hufanya upelelezi kwa kushirikiana na askari wa ndani na nje ya nchi.

Katika kukamilisha shughuli zake, Interpol hujikita katika makosa mbalimbali ambayo yamepewa kipaumbele.

Makosa hayo ni ya usafirishaji haramu wa binadamu, Ugaidi, Uhalifu dhidi ya mazingira na wanyamapori, uhalalishaji na utakatishaji wa fedha haramu.

Vilevile, wizi wa magari, wizi wa hakimiliki na kazi za sanaa, hati za kusafiria zilizopotea au kuibwa, silaha haramu pamoja na dawa za kulevya.

Nchi wanachama wa shirikisho hili la polisi duniani zinafaidika kwa kutafutiwa ndugu/mtu aliyepotea nje ya nchi, kujua uhalali wa gari analotaka kununua kutoka ndani na nje ya nchi na Kujua uhalali wa kampuni anayotaka kuingia mkataba nayo nje ya nchi.

Aidha, kumpata mtuhumiwa aliyetorokea nje ya nchi (wanted fugitives), kupata mali yake iliyoibwa/kutapeliwa nje ya nchi na kusaidia kurejeshwa kwa mwili wa raia wa Tanzania aliyefariki nje ya nchi.

Ufanisi wa shughuli za Interpol hutegemea sana mawasiliano ili kuziunganisha nchi zote duniani ambazo ni wanachama wake.

Kwa kulitambua hilo Interpol Makao Makuu Lyon, Ufaransa ilianzisha mtambo ujulikanao kama I-24/7 (Interpol saa 24 kwa siku saba) ambao unayaunganisha majeshi ya polisi duniani kote.

Mtambo huu hufanya kazi kwa haraka zaidi na kwa ufanisi mkubwa.

Huu ndio mfumo pekee wa kimawasiliano ambao haujawahi kudukuliwa kutokana na utaalamu mkubwa unaotumika kuuimarisha.

Ni vema wananchi wakafahamu kuwa kitengo cha Interpol pekee hakiwezi kupambana na uhalifu na wahalifu wa kitaifa na kimataifa kwa ufanisi mkubwa bila ya ushirikiano baina yao na Jeshi la Polisi.

***Imetolewa na Kitengo cha Uhusiano, Makao Makuu ya Jeshi la Polisi.***

# TUJIFUNZE KISWAHILI



**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

## Asiyeangalia huishia ningalijua

MTU asiyeangalia aendako huishia kusema 'laiti ningejua' baada ya kufikwa na jambo. Methali hii yatushauri tuwe watu wa kukanyika au wanaofuata ushauri tunaopewa na wanaotutangulia kwa maarifa au ujuzi kama vile wazee.

'Kanya' maana yake ni kataza mtu kutofanya jambo linaloweza kumletea hasara au madhara; kanyana, kanyia, kanyika, kanywa.

'Ushauri' ni maoni anayopewa mtu ili yamsaidie kufikia mapatano fulani na wengine. Maelekezo kama vile ya kiufundi anayotoa mtaalamu kuhusu namna ya kufanikisha jambo.

Wahenga walisema "Asiyeonywa huona (kwa) macho yake." Mtu anayekanywa kisha akayapuuza maonyo yale huishia kufikwa na madhara. Methali hii hutumiwa kumtajia au kumwelezea mtu anayepewa ushauri na kuupuuza, kuwa atakuja kupatwa na madhara.

Kuna wanaonibeza (kitendo cha kupuuza kitu, mtu au jambo; kitendo cha kuonesha hisia ya kejeli kwa mtu). Baadhi ya wanaonifahamu huniambia: "Ah! tangu lini Mmasai/Mchaga akajua Kiswahili?"

Wengine hunambia: "Rudi kwenu masaini na uchagani ukawafunze nduguzo Kiswahili fasaha. Kwenu mbuzi mwaita 'mbusi', nazi mwaita 'nasi', viatu mwasema 'fiatu.' Utatufundisha nini wewe? Sisi ndiwo wa kukufunza wewe."

Hata hivyo, wapo wanaounga mkono safu yangu ya "Tujifunze Kiswahili" kila Jumanne katika gazeti hili unalosoma sasa - Nipashe. Ukisema hutaki, kuna wanaotaka.

"Habari za leo. Shukrani kwa juhudi yako ya kutuelimisha matumizi mazuri ya lugha yetu, Kiswahili. Waandishi wa habari za michezo wana kawaida ya kutokamilisha sentensi. Hebu angalia mfano huu:

" ... ni timu kubwa na tunaiheshimu, lakini tumejiandaa kupata matokeo," alisema kocha wa timu. Hapa nashindwa kuelewa ni matokeo ya aina gani. Je, neno 'matokeo' lina maana sawa na ushindi? Naitwa Kissiwa, niko Zanzibar (+255 0713 768 335).

Siku iliyofuata akanitumia ujumbe mwingine: "Asalaam aleykum. Matumizi mabaya ya neno 'lakini.' Waandishi/wazungumzaji huandiika/husema, 'lakini pia ...' na kuendelea na maelezo yao. "'Lakini' huonesha hitilafu wakati 'pia' ni ziada. Iweje maneno haya yaunganishwe? Kwa nini lisitumike moja tu kati ya hayo?" Kissiwa.

Neno 'lakini' hutumiwa sana na viongozi wetu na ingawa nimelitolea maana yake mara nyingi, bado laendelea kutumiwa tofauti kabisa na maana yake. Kama alivyoandika Bw. Kissiwa, maana ya 'lakini' ni tamko la kuonesha kasoro ya jambo; neno linaloonesha upungufu, kasoro au hitilafu; isipokuwa, ila.

Mfano: "Alitaka kwenda kwa mwafulani (jina linalotumika kumtaja mtu ambaye yupo ila jina lake linafichwa) lakini alikatazwa na wazazi wake kutokana na tabia chafu ya huyo mwafulani.

Neno 'Pia' lina maana tano: i) Kitu chenye umbo la koni cha kuchezea watoto kwa kukizungusha wakati kimesimama ncha; ii) Mfupa unaochezacheza ulio juu ya goti; iii) Omo ya chombo cha majini yenye umbo la duara; iv) vilevile; na v) Bila ya kubaki, pamoja na.

Msomaji mwingine alinitumia ujumbe ufuatao: "Mzee Maro (yeye aliandika Malo) umefundisha vitu vya msingi sana. Hata mimi nimefurahi sana. Nakutakia kazi njema. Ni mimi Mustafa nikiwa Mtwara." 0684 307 081.

Nawashukuru wote walionitumia maoni yao. Mimi si mwalimu kama waniitavyo wengine ila ni mwanafunzi wa Kiswahili. Kidogo nipatacho huwashirikisha na kuwagawia wenzangu. Karibuni hata kwa kunikosoa kwani akuambiaye usikombe mboga ataka ushibe.

Sasa soma jinsi Kiswahili kinavyopelekwa arijojo (hali ya kupotea; kupoteza mwelekeo).

"Mnyalu buana, yaani juzi wenzako walikuwa wanakuangalia halafu wakacheeka ila mimi sikucheka, niliwaza ikitokea itakuwaje?"

"Ndugai buana, yaani unamtaja mke wa mwenzako kuwa ni mzuri, hee si unajua wagogo wa Dodoma kuamua huwa wanaamua kwa haraka mara moja. Sawa lakini mmh!"

"Spika buana, eti wabunge wanapiga kelele kama vilabuni!"

"Lakini kikubwa alichowaacha hoi wabunge na kutaka wampigie makofi mkongwe huyo wa siasa za Tanzania, ni pale aliposema ndiyo mwalimu wake kwa kila kitu. Nyoka wa makengeza buana!" Neno buana halimo kwenye msamiati (maneno yote yanayotumika katika lugha) wa lugha ya Kiswahili ila yanaingizwa na waandishi wetu baada ya kusikia maneno ya vijiweni na mitaani! Eti buana ndio bwana! Twaipeleka'pi lugha yetu?

Sasa hata wazungumzaji kutamka au waandishi kuandika maneno ya Kiswahili kwa ufasaha wanashindwa! Ndo maana wahenga walisema "Kuchamba (ashaakum) kwingi mwisho huondoa mavi."

Methali hii hutumiwa kupigia mfano jambo ambalo limeonesha dalili fulani ambazo zimepuuzwa kisha likaishia kuharibika. Tusiyadharau mambo madogo; huweza yakawa makubwa baadaye.

Mambo madogo kuwa makubwa ni kama haya: "Yale maji ya mjengoni yanayorukaruka yamekauka ama vepee?" Eti waandishi wameona neno vipi halifai ila linalofaa ni vepee! Haya ndio matokeo ya kuchamba kwingi ....!

"Mwenyewe anajiitaga mawe matatu. Ndo lugha ya wenzetu wa Kanda ya Ziwa kusema nakulaga, nakwendaga, nasemaga n.k. badala ya hula, huenda, husema, n.k.

Hata wasomi sasa wameathirika kwa matumizi mabaya ya maneno kama ilivyo hapa:

***Methali: Kila mlango na ufunguo wake.***

***marobarnabas@yahoo.com, 0715/0784 334 096***

## UCHAMBUZI WA KITABU;

# Elimu ya Kujitegemea na Mwalimu Julius K. Nyerere

KARIBU msomaji wangu kuendelea kujifunza vitabu ili kujenga ustawi wa maisha yetu.

Leo kitabu chetu ni 'Elimu ya Kujitegemea,' hivyo basi soma kwa utulivu namna Mwalimu Nyerere alikuwa na fikra pana kwa ajili ya taifa hili.

Mbali na kushika nafasi ya juu ya uongozi nchini, Mwalimu Nyerere pia alikuwa ni mwandishi hodari na msomaji wa vitabu.

Katika maisha yake, inakadiriwa alisoma vitabu vipatavyo 6,000. Ni wazi hekima zake nyingi zilizotokana na mapenzi yake ya kusoma vitabu.

Kama ilivyo kwa wasomaji wengi wa vitabu huishia kuwa waandishi, ndivyo na kwake ilikuwa hivyo.

Elimu ya Kujitegemea ni moja ya vitabu vyake vya mkusanyiko wa hotuba na mitizamo yake ya kina kuhusu elimu.

Tunaelekea takriban miaka 20 toka kifo chake kulichotokea Oktoba 14, mwaka 1999, lakini hazina alioiacha itaendelea kudumu hasa maandiko na hotuba zake.

Kila nchi hutofautiana katika mipangilio ya elimu na uendeshwaji wake, japo shabaha kuu huwa ni moja ambayo ni kuwa kama njia ya kurithisha maarifa, mila za taifa, ujuzi kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Na kwa namna hii kuwaandaa vijana ili kuchukua nafasi na kuziendeleza zaidi kwa ajili ya taifa lao.

Elimu hii haishii tu darasani. Ikumbukwe kabla ya uhuru wa nchi za kiafrika, bado kulikuwa na elimu iliyokuwa si rasmi ya kufundisha mafunzo kwa vijana wao kwa njia ya masimulizi jioni, jando na unyago juu ya kukabiliana na changamoto za kimaisha.

Pia vijana walifundishwa ujuzi wa aina za dawa zitokanazo na mizizi ya miti. Walifundishwa kwa kutenda na pia wakaishi kwa kurithisha kwa kurithisha ujuzi uliokuwa na tija kwa kizazi kingine.

Ikiwa taifa lolote litashindwa kufikia shabaha ya kuwaandaa vijana juu ya ujuzi, maarifa, busara na mila za taifa katika kizazi kimoja na kingine ni wazi kuwa maendeleo ya nchi hiyo yatalegalega sana. La sivyo elimu itazalisha minong'ong'ono ya watu baada ya kugundua kwamba elimu walioyonayo imewaandaa na kuwapa maisha yasiyo ya matarajio yao.

Elimu ni kama dira ya taifa lolote, inapoanza kuyumbayumba isitarajiwe kuwa taifa laweza kuwa salama.

Kwa hali hiyo, ni vyema basi mipango na ndoto za nchi yoyote ile ijue inataka nini. Kwamba mfumo wa elimu uendane na shabaha ya mwelekeo wa taifa.

Ni wazi kuwa bado maeneo la vijijini hayajapewa kipaumbele kwenye suala la huduma za kijamii tofauti na ya miji.

Kuimarishwa kwa vijiji kunawawajibisha pia wanavijiji wenyewe kuchangia mawazo na fedha ili kuinua kiwango cha maisha yao kielimu, kiuchumi na katika masuala ya afya.

Mwalimu Nyerere alisisitiza kuwa elimu kiwe chombo cha kupanda mbegu ya watu kuishi pamoja na kufanya kazi pamoja kwa faida ya wote.

Kwamba elimu isiwe chombo cha kukandamiza na kudharau waliokosa fursa ya kusoma au kusomeshwa.

Elimu ikumbuke kuwa vijana waliosoma hawana budi kutimiza wajibu wao katika kuendeleza vijiji vyao, jamii zao na kipimo cha maisha bora ndio yawe matokeo ya kupimwa.

Aidha, elimu iwafundishe vijana kujiona ni sehemu ya jamii, rafiki na ndugu katika kushirikiana. Na angalizo ni kwamba isiwe chanzo cha majivuno kwa wengine.

Rai ya Mwalimu Nyerere ni kwamba elimu inayotolewa iwe mosi ya udadisi, pili inayojenga uwezo wa kujifunza na tatu yenye kujenga imani katika nafsi ya mtu kwamba yeye ni raia katika jamii husika kama walivyo wengine pia.

Haya mambo matatu ni muhimu kwa upande wa elimu ya mafunzo ya kazi na maadili ya maisha.

Mwalimu Nyerere alisema: "Hata kijana akijifunza utaalamu wa kulima namna gani, hatapata kitabu kitakachompa majibu ya matatizo yote atakayoyakuta katika shamba lake mwenyewe."

Ni muhimu kujifunza bila kuchoka. Aidha, wananchi huru wa Tanzania watapaswa kujiamulia wenyewe yote yanayohusu maisha yao.

Hakuna msahafu wa siasa, wala mwingine wowote utakaoshuka na kutoa majawabu ya matatizo yote yatakayotokea katika nchi hii siku za usoni.




Mwalimu Julius Nyerere. **PICHA: MTANDAO**

**HEKIMA ZA WAZEE**

Si kweli kuwa elimu ya darasani au ya vitabuni itatosha kuwa suluhisho, ikiwa ujuzi na hekima za wazee zitapuuzwa au kudharauliwa.

Ni muhimu kwa kijana msomi na mtu msomi kutopuuza hekima za wakulima wazee kwa mfano na wengine wote walio na ujuzi wa kikale. Hitaji la kuheshimu na kujifunza mengi kutoka kwao ni la msingi. - Haishii kusoma tu pasipo kujifunza stadi zingine za maisha yao mfano namna ya upishi kiasili, kazi za nyumbani, miiko ya jamii. Ni aibu kwa kijana kuishia kusoma tu na akashindwa kujua hata historia ya jamii yake.

Usomi si kujiepusha na kazi za kusaidia jamii hata pasipo malipo yoyote yale, mfano kusafisha mazingira, kuchimba mifereji na kazi zote katika jamii zao.

Mwisho mwalimu Nyerere anashauri pawepo na kambi za vijana ambazo zitapelekea pawe na chachu ya kuinuana kiuchumi na kutumia fursa za elimu zao na ujuzi kutatua matatizo yaliyo katika jamii.

Vitabu vingine vya Mwalimu Nyerere ni pamoja na Tujisahihishe. Wakati mwingine tutajifunza hekima zake na maarifa aliotuachia kizazi hiki na vijavyo.

***Mchambuzi ni Dk. Raymond Nusura Mgeni, raymondpoet@yahoo.com***

***+255 676 559 211.***

ELIMU

NA SHABAN NJIA, KAHAMA

# Elimu kunufaisha wafugaji Msalala

• Ni ya kuwakinga ng'ombe dhidi ya majanga wakati wa ukame •Inatolewa na Shirika la TAPO



Ofisa Mifugo wa Kata ya Bulige, Halmashauri ya Msalala, Devid Chiloleth (aliyenyanyua chupa), akiweka dawa ya minyoo kwenye silinji kabla ya kutoa tiba kwenye mifugo.

TANZANIA ni moja kati ya nchi zinazoongoza kwa kuwa na mifugo mingi barani Afrika, ikitanguliwa na nchi za Ethiopia na Sudani ambazo ni kinara katika sekta ya mifugo hadi sasa.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Ufugaji ya Wizara ya Mifugo ya mwaka 2013, Tanzania ina idadi ya ng'ombe zaidi ya milioni 22.8, mbuzi milioni 15.5, kondoo milioni 6.9 na nguruwe milioni 2.1.

Aidha, kwa mujibu wa Shirika la Chakula Duniani (FAO), wakati Brazil ikiongoza duniani kwa kuwa na ng'ombe milioni 211, Tanzania inashika nafasi ya 11 duniani.

Kwa Afrika Tanzania ni ya tatu, ikitanguliwa na Ethiopia yenye ng'ombe milioni 54, wanaoifanya nchi hiyo ishike nafasi ya tano duniani.

Sudan yenye ng'ombe milioni 41.9 inashika nafasi ya pili Afrika na ya saba ulimwenguni.

Na katika ngazi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Tanzania inafuatiwa na Kenya yenye ng'ombe milioni 18.1, Uganda ng'ombe milioni 13, Sudan Kusini ng'ombe milioni 12, Rwanda ng'ombe milioni 1.4 na Burundi, ng'ombe 777,786.

Pamoja na Tanzania kuwa na wingi huo wa mifugo, ni nchi ya Ethiopia ndiyo yenye viwanda vingi vitokanavyo na malighafi za mifugo hasa ng'ombe, ikizalisha bidhaa aina ya ngozi kwa kiwango cha juu barani Afrika kwa kipindi hiki.

Ufugaji nchini kwa kiwango kikubwa unafanyika kwenye maeneo ya vijijini. Hata hivyo, pamoja na faida zake bado wafugaji wengi wanaishi maisha duni.

Lakini hata kwa upande wa serikali pia, bado haijafaidika kwa upeo na matunda ya uwepo wa rasilimali hiyo nchini.

Kimsingi wafugaji wanapatikana katika mikoa yenye mifugo kama Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Tabora, Geita, Mara na Singida.

Lakini pia Dodoma, Pwani, Morogoro, Katavi, Arusha, Manyara, Tanga, Songwe, Mbeya na Rukwa.

Hata hivyo, faida ya mifugo hii kwa wafugaji ni ya kiwango cha chini.

Na inatokana na mauzo ya mazao kama nyama, ngozi na kwato zinazowapatia kipato ambacho kinawawezesha pamoja na mambo mengine kuhudumia familia zao ikiwa ni pamoja na kusomesha watoto wao.


Mifugo aina ya ng'ombe na punda wakila mashudu na pumba zilizotolewa na Shirika lisilo la Kiserikali la Haki na Ustawi wa Wanyama Tanzania. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA**

Na kwa mujibu wa ripoti ya ufugaji ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ya mwaka 2012, zaidi ya kaya milioni 2.3 zinategemea ufugaji kama chanzo kikuu cha mapato.

Pamoja na hayo ripoti hiyo inasema mchango wa sekta hiyo katika ustawi wa kaya hizo na katika pato la Taifa ni mdogo sana.

Kuna sababu kadhaa zinazosababisha hali hiyo. Bado wafugaji nchini wanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na ukosefu wa maeneo ya malisho hali inayosababisha wafugaji kuvamia maeneo ya wakulima, pia mapori ya hifadhi ya taifa.


Ofisa Mifugo wa Kata ya Bulige, Devid Chiloleth (kulia), akimchoma punda sindano ya kukinga ngozi isishambuliwe.

Kwa mfano nyakati za ukame, wafugaji wamekuwa wakiingiza mifugo katika maeneo ya hifadhi za serikali na hivyo kuzua migogoro, huku wengine wakikamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Kimsingi migogoro inayosababishwa na wafugaji inachangiwa na mambo mengi, lakini kubwa ni kukosekana kwa elimu ya ufugaji wenye tija.

Elimu ambayo itawapatia maarifa ya namna ya kuhudumia mifugo yao ikiwa ni pamoja na kuwa na malisho bora, tiba dhidi ya magonjwa ya mifugo na namna bora ya kuiweka mifugo katika hali ya usafi.

**MKURUGENZI WA TAPO**

Yohana Kashilillah ni Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la Haki na Ustawi wa Wanyama nchini (TAPO).

Anasema elimu inahitajika kwa wafugaji kuwawezesha kuwa na maarifa ya kuendesha ufugaji wenye tija.

> "Wafugaji wengi hawana uelewa wa nini cha kufanya na hasa kunapokuwa na ukame katika maeneo ya malisho, hali inayochangia mifugo mingi kudhoofika na kufa wakati mwingine," anasema na kuongeza:

"Wafugaji wengi hawana uelewa wa nini cha kufanya na hasa kunapokuwa na ukame katika maeneo ya malisho, hali inayochangia mifugo mingi kudhoofika na kufa wakati mwingine," anasema na kuongeza:

"Na ndiyo maana shirika letu limeamua kutoa elimu kwa wafugaji ya nini cha kufanya wakati wa ukame na pale yanapotokea majanga mengine kama ya magonjwa ya mifugo."

Anasema wameanzia na Wilaya ya Kahama, katika Halmashauri ya Msalala kwenye kata za Bulige, Mwendakulima, Kagongwa na Segese.

**MWENYEKITI WA WAFUGAJI BULIGE**

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji katika Kata ya Bulige, Daudi Yona anasema hali ya maeneo ya malisho huwa mbaya hasa katika kipindi cha kiangazi kama sasa na kwamba wafugaji mara nyingi hujikuta katika mgogoro na wakulima.

"Tunajikuta tukitembea na mifugo hadi umbali wa kilometa nane kila siku kutafuta malisho... na kwa kuwa tunategemea mashamba ya watu yaliyokwishavunwa mazao, nyakati zingine tunakumbana na tatizo la wamiliki wake kutukataza kuchungia kwenye mashamba yao," anasema.

Anabainishwa kwamba kutokana na changamoto ya malisho, kila inapofika mwezi wa nane hulazimika kuhama na mifugo yao kwa ajili ya kutafuta malisho sehemu zingine kwa kipindi cha miezi mitatu.

"Huwa tunarudi baada ya miezi hiyo kwani mvua za masika zinakuwa zimeanza na majani yanakuwa yamekwishachipua, hivyo mifugo inapata chakula," anasema na kuongeza.

"Tunashukuru kwamba katika kipindi hiki cha miezi yenye changamoto za malisho, Shirika la Tapo hutuletea misaada

Inaendelea Uk. 18

JIELIMISHE

## JOTO LA KUPINDUKIA LATAMALAKI BARANI ULAYA NA MAREKANI


Mtoto akicheza kwenye maji wakati wa msimu wa joto kali. **PICHA: MTANDAO**

VIWANGO vya joto barani Ulaya, Marekani na baadhi ya maeneo ya Kaskazini mwa Afrika, ni vya juu na vinatishia afya ya binadamu, kilimo na mazingira.

Joto la kupindukia linaendelea kulikumba bara la Ulaya kwa wiki nyingine, huku kiwango cha joto kikivunja rekodi, linasema Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO).

Kwa mujibu wa WMO, kwa takribani wiki mbili zilizopita, joto lilikuwa kali kupita ada, huku sehemu nyingi za Ulaya zikishuhudia viwango vya juu vya joto, jua kali la kupita kiasi na fukuto la hali ya juu.

Mathalani Ujerumani na Benelux, zilishuhudia rekodi mpya ya joto lililofikia nyuzi joto 40°C.

WMO inasema hata siku ya Jumatatu wiki iliyopita viwango vya juu vya joto vilirekodiwa nchini Ufaransa ambako iliripotiwa kuwa na viwango vipya vya chini vya joto hususani kwenye maeneo ya Kusini Magharibi ambako mji kama Bordeaux ulikuwa na kiwango cha chini cha nyuzi joto 24.8°C na Toulouse nyuzi joto za chini ni 24.6°C .

Sehemu kubwa ya Ufaransa na Uswis imewekwa katika tahadhari ya joto kali daraja la 3 kwa siku nne mfululizo, ikimaanisha kwamba watapata kiwango kikubwa kabisa cha joto kuwahi kushuhudiwa katika miaka ya hivi karibuni.

> Shirika hilo la utabiri wa hali ya hewa duniani limeongeza kuwa mbali ya Ulaya baadhi ya sehemu za Mashariki mwa Marekani zimeshuhudia joto la kupindukia mwishoni mwa wiki na maeneo mengi yakijiwekea rekodi mpya ya joto lililofikia nyuzi 100°F sawa na nyuzi joto 37.8°C.

Shirika hilo la utabiri wa hali ya hewa duniani limeongeza kuwa mbali ya Ulaya baadhi ya sehemu za Mashariki mwa Marekani zimeshuhudia joto la kupindukia mwishoni mwa wiki na maeneo mengi yakijiwekea rekodi mpya ya joto lililofikia nyuzi 100°F sawa na nyuzi joto 37.8°C.

Maeneo yaliyoathirika zaidi ni pamoja na Atlantic City, New jersey na uwanja wa ndege wa kimataifa wa JFK New york.

Aidha, kituo cha kitaifa cha huduma za hali ya hewa Marekani mjini Omaha kilifanya majaribio ya kuoka biskuti kwenye gari ili kupima kiwango cha joto na baada ya saa 8 juani, biskuti ilikuwa imeiva ikidhihirisha joto na jua lilikuwa kali kiasi gani.

Pia WMO inasema jaribio hilo linadhihirisha hatari iliyopo dhidi ya kuacha watoto au wanyama wafugwao kwenye gari katika kipindi hiki, hata kama ni kwa muda mfupi.

**UN**

# Elimu kunufaisha wafugaji

Inatoka Uk. 17

vya vyakula kuwanusuru wanyama wetu hususani ng'ombe na punda ambao huathirika zaidi kiafya kulinganisha na wengine."

Mbali na vyakula vya mifugo, Yona anasema shirika hilo huja katika kata hiyo kila baada ya miezi miwili kwa ajili ya kuangalia afya za wanyama, kutoa tiba na mafunzo kwa wafugaji ya namna bora ya kuendesha ufugaji wenye tija.

**OFISA MIFUGO KATA BULIGE**

Kwa upande wake Ofisa Mifugo wa kata hiyo, Devid Chiloleth, anasema wafugaji wamekuwa wakifuga kiasili zaidi kwa kutumia njia ya kuwatoa ng'ombe kwenda katika malisho na kuwarudisha wakati wa jioni, huku changamoto ikiwa ni mapori ya kuchungia.

Chiloleth anasema, wakati wa kiangazi wafugaji hutegemea chakula cha wanyama kitokanacho na mabaki ya mavuno ya wakulima pindi wanapomaliza kuvuna.

"Mabaki hayo yanakuwa si mengi na hivyo kunufaisha wafugaji wachache," anasema.

Anabainisha kwamba kipindi cha masika ng'ombe wengi huwa wanakonda, lakini pia huwa ni kipindi cha magonjwa kwa sababu ya wingi wa wadudu aina ya kupe wanaoshambulia mifugo.

"Sasa ukijumuisha na maji yaliyotuama, magonjwa ya minyoo huwa hayaepukiki kwa mifugo," anasema.

Ofisa Mifugo huyo anabainisha kuwa kwa sasa TAPO ndilo shirika linalosaidia kwa kiasi kikubwa wafugaji wa kata hiyo kutibu wanyama wao kama vile ng'ombe na punda.

Anasema shirila hilo linatoa msaada wa huduma za vitamini, vyakula vya mifugo na dawa za minyoo ili kuhakikisha mifugo na hasa ng'ombe hawashambuliwi maeneo ya mkiani, sikioni na sehemu za siri, hivyo kuzuia vifo.

**WITO**

Mratibu wa huduma hiyo kutoka TAPO, Master George, anasema ni bora wafugaji kujitokeza kwa wingi kunapokuwa na

## JE, WAJUA?



Wanafunzi wakitumia kompyuta mpakato katika mradi wa shule wa (INS) kwenye kambi ya wakimbizi ya Kakuma nchini Kenya. Mradi wa INS ni wa ushirikiano baina ya UNHCR na wakfu wa Vodafone. **PICHA: MTANDAO**

# Mradi UNICEF vitabu vya kidijitali fursa watoto wenye ulemavu Kenya

"Mfumo wa kidijitali wa kusoma ni mzuri sana kwa viziwi, ni wazo zuri ambalo tunalitekeleza kwa sababu wanafunzi hawa wanatumia uwezo wao wa kuona wakati wanasoma na vitabu vya kidijitali vina picha, ishara na rangi kwa hiyo inawatia moyo sana."

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) na wadau wake wamezindua jaribio la kitabu cha kidijitali katika shule 25 za msingi nchini Kenya.

Lengo ni kuimarisha elimu ya kidijitali hususan kwa watoto walio hatarini au maeneo ya vijijini ama mitaa ya mabanda na wanaoishi na ulemavu.

Kupitia video ya UNICEF tunakutana na mwanafunzi wa shule ya msingi akiwa darasani amevalia sare ya shule ambayo ni sweta ya kijani na shati jeupe.

Kwenye dawati ana kompyuta ndogo kwa makini kabisa anafuata maelekezo kupitia lugha ya ishara.

UNICEF inasema, watoto wengi walio na ulemavu wa viungo mara nyingi wanakosa elimu kwa sababu ya kukosa vifaa elimu, lakini vitabu mtandaoni ni habari njema.

Vitabu hivi vinahakikisha kwamba watoto walio na ulemavu wa kuona wanapata vitabu hivyo kwa njia ya sauti, na lugha nyepesi kwa walio na ulemavu wa upungufu wa kuelewa pia lugha ya ishara kwa viziwi.

Mfumo huu unakaribishwa pia na walimu kama anavyosema mwalimu Martha Mwango kutoka Shule ya Msingi ya Aga Khan ambaye anaonekana na wanafunzi wake darasani.

"Mfumo wa kidijitali wa kusoma ni mzuri sana kwa viziwi, ni wazo zuri ambalo tunalitekeleza kwa sababu wanafunzi hawa wanatumia uwezo wao wa kuona wakati wanasoma na vitabu vya kidijitali vina picha, ishara na rangi kwa hiyo inawatia moyo sana."

Mfumo huu umetajwa kuwa muhimu katika kuhakikisha kwamba wanafunzi wanakwenda sambamba na wenzao wasio na ulemavu wa viungo, kwani katika zama za sasa teknolojia inatumika katika mambo mbalimbali.

Kwa upande wao wanafunzi ambao walikuwa wamezoea mfumo wa kizamani wa mafunzo sasa wanapata taswira kamili kwani wanajifunza kupitia picha na video. Mwanafunzi Keith kupitia lugha ya ishara anasema:

"Nimependa sana kitabu hiki, ninafurahi kukisoma, ninapenda picha na kusoma hadithi zilizomo."

# UTAFITI


## KUPANDA MITI KUTAPUNGUZA MABADILIKO YA TABIANCHI

NJIA bora zaidi ya kupambana na ongezeko la joto duniani ni kupanda miti mingi, kadiri iwezekanavyo.
Hiyo ni kwa mujibu wa utafiti uliotolewa na mwanasayansi mmoja kutoka nchini Uswisi.
Mwanasayansi huyo anasema katika utafiti wake kuwa tunahitajika kupanda takriban miti trilioni moja, au zaidi ya hapo.
Habari nzuri ni kwamba tunaweza kusaidia kuzuia mabadiliko ya tabianchi kwa kufanya kampeni kabambe ya kupanda miti, kwa mujibu wa utafiti mpya uliochapishwa hivi karibuni.
Lakini kuna habari mbaya pia, kwa sababu tunahitajika kupanda miti katika eneo linalofikia ukubwa wa nchi kama Marekani ama nusu hivi ya Bara la Afrika.
Hata hivyo, baadhi ya wanasayansi wanatia shaka juu ya hitimisho la utafiti wa waraka huo.
Misitu inaweza kuhifadhi gesi nyingi ya kaboni.
Juhudi kama hizo zitaweza kuhifadhi theluthi mbili ya gesi za kaboni zinazozalishwa na binadamu na kupunguza viwango vya jumla katika anga hadi katika kiwango cha chini katika karibu karne moja, kwa mujibu wa utafiti ambao ulifanywa na Eth Zurich na kuchapishwa katika jarida la sayansi.
Utafiti huo ni wa kwanza kujaribu kuelezea ni miti mingapi inaweza kusaidia dunia, wapi pa kupandwa miti hiyo na ni kiasi gani cha kaboni kinaweza kuhifadhiwa na miti hiyo.
Misitu ni muhimu kufyonza gesi chafu za kaboni zinazohifadhi joto angani

**NAFASI YA KUPANDA MITI**

Na kuna nafasi ya kutosha, anasema mtafiti huyo mwanasayansi kutoka Uswisi.
Hata kwa kuwa na miji iliyopo hivi sasa na eneo la mashamba, kuna nafasi ya kutosha kupandwa miti mipya kuweza kuenea katika kilometa za mraba milioni tisa, eneo hilo ni takriban eneo sawa na Marekani.
Utafiti huo umepiga hesabu kwamba kwa muda wa miongo kadhaa, miti hiyo mipya inaweza kufyonza karibu tani za ujazo milioni 830 za gesi ya kaboni dioxide ambayo huhifadhi joto kutoka katika anga.
Hii ni kiasi ya uchafuzi mkubwa wa kaboni kama ilivyotolewa na binadamu katika kipindi cha miaka 25 iliyopita.
Manufaa makubwa yatakuja haraka kwasababu miti inaondoa kaboni zaidi kutoka katika hewa wakati ikiwa michanga, waandishi wa utafiti huo wanasema.
Uwezekano wa kuondoa kaboni nyingi zaidi uko katika maeneo ya tropiki.
Mataifa sita ambayo yana nafasi kubwa kwa kupanda miti mipya ni Urusi, Marekani, Canada, Australia, Brazil na China.

**DW**



Baadhi ya misitu ya kupandwa ambayo utafiti unaonyesha inanyonya hewa ukaa ambayo sasa inaongezeka kutokana na mabadiliko ya tabianchi. **PICHA: MTANDAO**

# ji Msalala

fursa kama hiyo ya matibabu kwa mifugo ili kuiwezesha kuwa na afya njema.

"Watumie majosho yaliyojengwa na Serikali katika maeneo yao na maofisa mifugo ili kuwa na elimu ya njia sahihi ya kutibu mifugo yao na kwa kipindi muafaka," anasema.

George anabainisha baadhi ya maeneo ambapo shirika hilo linafanya kazi ya kutoa elimu kwa wafugaji juu ya kuwakinga wanyama wao dhidi ya majanga ya ukame katika Wilaya ya Kahama ni pamoja na kata za Bulige, Mwendakulima, Kagongwa na Segese katika Halmashauri ya Msalala.

> Sasa ukijumuisha na maji yaliyotuama, magonjwa ya minyoo huwa hayaepukiki kwa mifugo," anasema.



Na Michael Eneza

# Nyuma ya mapito ya Laetoli kuna shujaa wa Kimasai?

WAKATI fani za sayansi zina kanuni za kupima vitu kwa urefu, upana, kina au uzito, fani za masuala ya jamii zinaongeza nyenzo za ziada katika utafiti, kwa kanuni ambayo mshairi na mtunzi Shaaban Robert angeiita Kusadikika.

Ndicho tunachokiona katika utafiti wa wataalamu wanne waliovinjari miongoni mwa jamii ya Kimasai eneo la hifadhi ya Ngorongoro yenye hazina ya mambo ya kale.

Liligunduliwa fuvu la kichwa la binadamu au mtu wa awali kabisa likapewa jina la kitaaluma la Zinjanthropus, halafu zikagunduliwa alama za miguu eneo la Laetoli.

Ziko alama kadhaa maeneo tofauti, mstari mmoja wa alama ukiwa wa jitu kubwa zaidi.

Wataalamu hao wakiongozwa na mwenyeji wao aliyeko Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Elgidius Ichumbaki, walisema katika makala iliyochapishwa na kufuatiliwa maeneo mengi, kuwa wakati sayansi ya mambo ya kale ni muhimu, ni jambo la lazima kujua watu wanaokaa eneo la Laetoli wanavyoelewa alama hizo za miguu.

Wanadhani alama hizo zinawakilisha nini? Yeye na wenzake watatu waliwauliza wanajamii za Kimasai ambao walikuwa wakifanya kazi pamoja nao hapo Laetoli, halafu pia wakaandaa majadiliano ya vikundi kati yao na wanavijiji wengine.

Hata wa vijiji vya karibu kama Essere, Enduleni na Kakesiyo walishiriki majadiliano hayo.

Kimsingi jamii ya Kimasai inayokaa eneo hilo inaunganisha alama za miguu za Laetoli na hadithi ya Lakalanga, shujaa mwenye nguvu aliyewasaidia Wamasai kushinda mpambano dhidi ya jamii fulani ya karibu.

Kwa mujibu wa hadithi hiyo, ambayo ni sehemu mahsusi ya mapokeo katika eneo hilo, Lakalanga alikuwa mkubwa kiasi ambacho popote alipokwenda aliacha alama zinazoonekana wazi ardhini.

Wataalamu hao wanasema licha ya kuwa hakuna mpangilio halisi wa nyakati katika hadithi hiyo, maelezo hayo yameingia kwa kina katika ufahamu wa watu hao.

Wakijitahidi kuonyesha umuhimu wa maelezo hayo katika uelewa wa kisanyansi wa alama za mapito ya Laetoli, wanasema kuwa Lakalanga anayo nafasi maalum katika hisia za jamii ya Wamasai na ni muhimu kuna hadithi inayomuunganisha na waliyoleta alama za miguu.



Ugunduzi mpya wa nyao za binadamu eneo la Laetoli lililoko ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), ambazo ni za watu wanaodaiwa kuishi miaka milioni 3.7 iliyopita. **PICHA: MTANDAO**

Kwa maana hiyo kuna haja ya kuunganisha hisia hizi katika tafsiri na hifadhi ya alama hizo za miguu, kwani kufanya hivyo kutapunguza uwezekano wa watu kuziharibu alama hizo, na kuongeza uhusiano kati ya jamii ya watu na historia yao. Yaani hadithi hiyo inakuwa sehemu ya uhifadhi.

Kilichofanyika hapo ni kuongezea kinachozungumzwa katika vijiji vya karibu kuhusu alama za miguu ambazo zinaonekana katika udongo ulioganda wa volcano (tope la moto kutokana na kulipuka ncha ya mlima na kusukuma mafuriko ya kilicho katika 'tumbo' la dunia kutokana na tetemeko, pale ambako kuna mpasuko ulioenda kina sana chini ya ardhi). Msukumo huo wa kutupa tope la moto, maji yaliyochanganyika na udongo kutoka kina cha dunia, ulizusha milima.

Swali ambalo wanafunzi na watu wa kawaida wanaosoma maelezo hayo katika magazeti hapa nchini na pia katika mitandao ya kitaaluma au ya kijamii ni kama mapokeo hayo ya jamii iliyo karibu na mapito ya miguu eneo hilo, ni sehemu ya sayansi au ni fasihi.

Wanataaluma hao wanasisitiza kuwa maelezo hayo ni sehemu ya uelewa wa kisayansi wa uwepo wa mapito hayo, hasa yenye alama za mtu ambaye ukilinganisha na alama nyingine zilizoundwa wakati huo huo, wakati tope hilo bado ni laini linabonyea likikanyagwa, hakuwa mtu wa kawaida.

Wanaweka pembeni suala la mpangilio wa muda katika maelezo hayo, wakiona uwepo wa hisia hizo na jinsi zilivyojengeka katika jamii hizo ni sababu tosha ya kuzingatia maelezo hayo katika...sayansi.

Wanasayansi katika maelezo rasmi ya kitaaluma wanasema kuwa alama hizo za miguu zinatokea kipindi cha kuwekwa marundo au mitiririko ya volcano kipindi cha Pliocene, kinachodhaniwa na wanasayansi kuwa kilidumu miaka milioni 5.3 iliyopita hadi miaka milioni 2.5 iliyopita.

Alama hizo za miguu zinasemekana kuwa zimewekwa na kundi la viumbe wanaofanana zaidi na sokwe ambao ni hatua ya kufikia umbile halisi la binadamu (au mtu), zilipogunduliwa zikaitwa kwa jina la kisayansi Australopithecus. Fuvu moja (la mwanamke) lililoonekana likaitwa 'Lucy.'

Kwa maana hiyo alama hizo za miguu ni za 'Austrapolithecus afarensis' walioishi zama za kale, na siyo kale hii ya kusambaa kwa makabila na kuanza kutenga maeneo ya kila ukoo au kabila kwa njia ya vita.

Kimsingi kinachotokea hapa ni wanasayansi kujaribu kutaifisha alama hizo ziwe za Kitanzania, zinazotokana na jamii inayozunguka eneo hilo, kwa kupigia debe maelezo yao kimapokeo ambayo hayawezi kwa hali yoyote ile kuoanishwa na maelezo ya kitaaluma.

Hizi koo ambazo zimekuwa makabila zilianza kusambaa maeneo tofauti hasa kuanzia mwaka 1500 – takriban miaka 500 kurudi nyuma kuanzia hapa tulipo. Sasa jamii hizo ni 'Australopithecus'?

Katika maelezo yao ya jumla, jopo hilo la wanasayansi wanne linaunda taswira ya suala hilo inayoacha maswali mengi zaidi kuliko inavyojibu, au tuseme inaunda taswira inayopendeza machoni, halafu wanadengulia tofauti kati ya taswira hiyo na sayansi halisi.

Ni kile ambacho Wafaransa wanaita 'un tour de passe passe,' yaani kila kinacholetwa unasema acha kipite, bila mchujo na bila kuhoji usahihi wa kinachozungumzwa.

Kwa Kiswahili ni kucheza ngoma ya 'gombe sugu' na kuacha ieleweke kuwa kinachozungumzwa nacho ni sehemu ya sayansi halisi.

Wanasema mwaka 1976 na 2014 wanasayansi walitaarifu kuwa kuna alama za miguu za binadamu katika mabaki ya kivolkano ya Pliocene pale Laetoli, Kaskazini Mashariki ya Tanzania.

Walijenga fikra kuwa alama hizo za miguu zinatokana na aina kale ya mtu, Australopithecus afarensis.

Siyo tu kwamba alama hizo za miguu zimechangia sana uelewa wa wanasayansi kuhusu hatua za kufikia kujengeka maumbile ya binadamu ila pia zimeweka Laetoli na Tanzania katika ramani ya dunia ya utafiti wa mambokale.

Hata hivyo, kuna tafsiri tofauti nani aliyeweka alama hizo, ambako hisia za wanasayansi zinafahamika kwa mapana yake, lakini mapokeo ya Wamasai (wanaoishi karibu na eneo hilo) hayajawahi kuchunguzwa.

Mada hii inadadavua hisia za Wamasai hizo alama ni nini, ni za nani. Tunaarifu kuwa dhana zinazohusiana na undani wa maumbile na chanzo cha alama hizo na nani aliyezifanya ni sehemu ya historia ya Wamasai.

Mwisho tunatoa rai kuwa kwa uhifadhi endelevu wa alama hizo, maelezo ya wenyeji yaingizwe katika tafsiri za kisayansi za eneo hilo. Hapo kuna tofauti gani na kusadikika, kuita ni sayansi?



# WADAU SABATO KASIKA

## BAADHI ya wazazi na walezi wanadaiwa kukumbatia mila zilizopitwa na wakati ikiwamo ya kuficha watoto wenye ulemavu na kusababisha wasipate elimu. Wadau wana maoni gani?



**MICKDADI MCHILA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

ELIMU ni haki ya kila mtu, awe mweusi mweupe, mlemavu na asiye mlemavu, hivyo wale wasiopeleka watoto wao shule hawawatendei haki. Nasema hivyo kwa sababu si walemavu tu, bado kuna watu wasiojua maana ya elimu na hawaoni kwa nini wapeleke watoto wao shule. Ndiyo maana nikasema elimu ni haki ya mtu awe mweusi, mweupe na hata mlemavu. Sidhani kwamba mtu anayejua umuhimu wa elimu anaweza kubagua watoto kwamba aliyekamilika viungo ndio aende shule na mlemavu abaki nyumbani. Hii ni dhana ambayo imepitwa na wakati kwani watoto wote ni sawa na wana haki sawa katika elimu. Bila elimu mtu hawezi kufanya shughuli zake kwa uhakika ama kujiamini. Ndiyo maana serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali wamejitahidi kuhamasisha jamii kuona umuhimu wa elimu. Wanaoendelea kuwaficha watoto wao wakiwamo walemavu na kutowapeleka shule ni wakaidi. Wanatakiwa kuelimishwa zaidi ili watambue makosa yao, kwani wasiopelekwa shule waweza kuwa msaada mkubwa kwao wakipata elimu. Mtu akielimika anaweza kupata kazi nzuri, kufanya biashara nzuri na kuendesha maisha yake vizuri. Ndiyo maana jamii inahamasishwa kupeleka watoto shule, wawe walemavu na hata wasio walemavu kwa lengo moja kwamba baadaye waweze kutumia elimu yao kujitegemea.



**ESTHER NHAMBU (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

Mimi ni mlemavu, napinga kwa nguvu zote wale wanaoficha au kutopeleka shule watoto walemavu, kwani kitendo hicho kinawanyima haki yao ya msingi ya kupata elimu. Elimu ni haki ya kila mtoto awe mlemavu ama ana viungo kamili, wote wanatakiwa kupewa elimu. Kwa maana hiyo wanaowaficha wachukuliwe hatua za kisheria kwani ni haki ya msingi na kisheria mtoto kupata elimu bila kujali maumbile yake, awe wa maskini ama tajiri. Wito wangu ni kwa walimu, mashirika yasiyo ya kiserikali yanayopambana na ukiukwaji wa haki za binadamu serikali iyashirikishe kazi hii ya kupambana na wale wanaondekeza tabia hiyo. Natambua kwamba bado wapo wanaowaficha walemavu, hivyo kwa kutimiza wajibu wetu tushirikiane kupunguza idadi ya walemavu wasiosoma ambao wako mitaani. Tukumbuke kwamba serikali ina mambo mengi ya kufanya, hivyo haiwezi kufanya kila kitu, ni wajibu wetu kufanya sehemu yetu ili kuisaidia serikali kupambana na hali hii. Wengi wa wale wanaowaficha wana imani potofu kwamba kuzaa mlemavu ni aibu ama laana. Wakumbuke kuwa suala la uzazi anajua Mungu, hivyo wakubali kile ambacho wanakipata kwenye uzazi wao na si kukitenga.



**CHRISTINA LAZARO (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

KASI ya kuhamasisha jamii kuona umuhimu wa elimu kwa kila mtu inatakiwa iongezwe ili kusaidia walemavu wote waweze kupelekwa shule. Mambo ya mila zilizopitwa na wakati hayana budi kuachwa. Tuko karne nyingine hii ya sayansi na teknolojia, ambayo inakwenda sambamba na elimu. Kwa muda mrefu walemavu wamekuwa wakiachwa nyuma kutokana na baadhi ya wazazi na walezi kuwanyima elimu kwa kufichwa nyumbani. Ninashukuru serikali kuendelea kukemea tatizo hili na pia kuhamasisha jamii kuachana na tabia hii ambayo ni sawa na kunyanyapaa. Lakini pia kasi ya uhamasishaji ni bora iongezwe, kwani kila mtu ana haki sawa na mwingine, awe mlemavu au aliyekamilika viungo. Sioni sababu yoyote ya mzazi kumtompeleka shule mwanaye mwenye mlemavu, huyu naye ana haki ya kupata elimu na anaweza kujitegemea na hata kuisaidia jamii. Uwezeshwaji mkubwa katika maisha ni elimu, hii ndio inaweza kumfanya mtu akamudu mazingira yanayomzunguka. Kwa wale, ambao hawakubahatika kupelekwa shule kutokana na imani hiyo mbaya, wasaidiwe kwa namna yoyote ikiwamo hata kupewa mitaji wafanye biashara ili nao waishi maisha mazuri kama watu wengine. Pia ningewashauri wazazi wenye watoto walemavu wasiwafiche nyumbani na wasiwaone kana kwamba ni mkosi. Wawapeleke shule wapate elimu, kwa kuzingatia kwamba bila elimu ni sawa na bure, wanaokaidi wachukuliwe hatua za kisheria haraka.



**JACKSON NACKSON (MKAZU WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

JAMII itambue kwamba mlemavu ni mtu wa kawaida kama mwingine, awe mlemavu macho kama mimi, viungo hata ngozi, wote hawa wana haki sawa kama walivyo wengine. Nina uhakika wakiwezeshwa kwa kupata elimu wanaweza kufanya makubwa, katika nchi hii. Dhana ya kusema kwamba walemavu hawawezi chochote ni potofu kabisa. Mbona mimi sioni lakini ninafundisha na wanafunzi wananielewa vizuri na wananikubali? Hivyo ninatoa wito kwa wazazi ambao bado wana tabia ya kutopeleka shule watoto wao wenye ulemavu waachane na tabia hiyo, wawasomeshe kwani wanaweza kuwa msaada mkubwa kwao kwa siku za baadaye. Kwanza kabisa ninawaomba wazazi na walezi wote wenye watoto walemavu wawasaidie kupata elimu na kama hawana uwezo wa kuwasomesha, wawe wazi ili wasaidiwe. Na pia walemavu ambao wanasoma waongeze bidii katika masomo ili baadaye wafaidike na elimu waliopata. Ninaiomba serikali itukumbuke na sisi ambao tuko kazini kwa kutupa vifaa mbalimbali ambavyo vitasaidia kufanikisha kazi. Kwa mfano mimi ninahitaji kupata fimbo, mashine ya kuandikia na vitu vingine vingi ambavyo vinalingana na hali yangu.



**NURU DIKO ( MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

HII ni kasumba iliyojengeka miongoni mwa jamii kwamba walemavu ni watu ambao hawafai na wala hawastahili kupelekwa shule na pia kuwa na matarajio chanya ya kuzaa mtoto asiye na ulemavu, lakini inapotokea kwa walivyotarajia sivyo wamepata mtoto mlemavu wanakata tamaa na kuamua kufanya yale, ambayo hayafai ikiwa ni pamoja na kuwaficha na hata kutowapeleka shule. Mimi nadhani cha kufanya hapa ili kuachana na mila hizo ni kuwapo kwa semina elekezi kwa wazazi na jamii ambayo bado inawatenga walemavu na kuwapa ukweli kwamba wale ni watu kama wengine ambao pia wana haki ya kupata elimu. Pia serikali iwe tayari kuwaunga mkono walemavu wanapolalamikia haki zao, yaani wasaidiwe haraka ikiwamo elimu kuanzia ya msingi na kuendelea na pia wapewe kipaumbele kwenye ajira za moja kwa moja ili kuwapa moyo wazazi wao na hata wa wale wanaowaficha na kuwanyima elimu. Suala la kutowapeleka shule watoto wenye ulemavu si la serikali. Jamii ndio inayojua kwamba ni mzazi gani au mlezi gani mwenye mtoto mlemavu ambaye hataki kumpeleka mtoto shule, kama yupo aelimishwe ili atambue kuwa mlemavu anastahili kupata elimu na kama amekuwa mgumu kuelewa, taarifa zifike serikalini ili hatua zaidi zichukulie ili kumwokoa mtoto mwenye ulemavu.

# Wapewa elimu uvuvi wa kisasa

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

VIJANA 978 katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, wamepatiwa elimu ya ufugaji bora wa samaki kupitia Shirika la TechnoServe ili kuwawezesha kuvua kwa kuzingatia kanuni na taratibu.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Dk. Hunter Mwakifuna, alisema juzi kuwa elimu ya ufugaji bora wa samaki ambayo ilitolewa kwa vijana ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya kuwakwamua na umaskini lakini kunufaika na fursa mbalimbali zinazowazunguka.

Dk. Mwakifuna alisema wanufaika wengi wa elimu hiyo ni wale wanaofanya kazi yao ndani ya Ziwa Nyasa na kupitia mafunzo hayo, wamejifunza namna bora ya kuvua samaki kwa teknolojia ya kisasa.

"Halmashauri imejitahidi kulikomboa kundi kubwa la vijana ambao walikuwa hawana ajira. Kwa umuhimu huo, tuliamua kutoa mafunzo kwa vijana wanaojishughulisha na uvuvi pamoja na wale wanaotamani.

Wote hao wamepewa maarifa juu ya kuendesha shughuli hiyo. Hii imesaidia vijana kutumia vyema fursa ya Ziwa Nyasa kwa kujiingiza kipato kupitia uvuvi," alisema Dk. Mwakifuna.

Pia alisema katika mwaka 2018/2019, Idara ya Mifugo na Uvivu ya Halmashauri, imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali kama uhimilishaji wa ng'ombe wa asili na kutokana na kazi hiyo, ng'ombe 765 walihimilishwa kati yao ndama wakiwa 417, majike 160 na madume 257.

Aliongeza kuwa katika kuimarisha idara hiyo, halmashauri ilinunua chanjo za kuku hivyo kuwezesha kuku 581, 725 kupatiwa chanjo ya kideri.

Mmoja wa wanufaika wa mafunzo hayo, Jacob Mwakyusa, alisema amejifunza teknolojia mpya ya uvuaji na sasa anavua samaki wengi kulinganisha na awali.

Alisema awali alikuwa anatumia uvivu haramu ambao umepigwa marufuku na serikali lakini baada ya kupata elimu, ameanza kutumia njia za kisasa zinazokubalika na anapata samaki wengi.

**Awali alikuwa anatumia uvivu haramu ambao umepigwa marufuku na serikali lakini baada ya kupata elimu, ameanza kutumia njia za kisasa zinazokubalika na anapata samaki wengi.**

# Watia saini kuwalinda mjamzito na mtoto

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

WATENDAJI wa kata 20 katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wametia saini mkataba wa kulinda afya ya mama mjamzito, anayenyonyesha na mtoto mwenye umri wa chini ya miaka mitano kwa nia ya kukabiliana na utapiamlo na udumavu.

Akizungumza jana wakati wa hafla ya utiaji saini iliyofanyika kwenye ofisi za wilaya ya Mbarali, Mkuu wa Wilaya, Reuben Mfune, alisema mkataba huo unalenga kukabiliana na changamoto ya utapiamlo na udumavu ambayo imekuwa ikiharibu maendeleo ya ukuaji wa mtoto.

Alisema ili kufanikisha jukumu hilo, viongozi walikubaliana jambo hilo lisimamiwe na watendaji wa kata kwa sababu wako karibu zaidi na wananchi na kusimamiwa ipasavyo.

**Pamoja na jitihada zinazochukuliwa na serikali pamoja na wadau, bado kuna changamoto ya lishe hususani katika makundi maalumu ya watu.**

Mfune alisema pamoja na jitihada zinazochukuliwa na serikali pamoja na wadau, bado kuna changamoto ya lishe hususani katika makundi maalumu ya watu.

"Tumeamua kutiana saini na watendaji wa kata zote 20 za wilaya ya Mbarali ili kwenda kusimamia kikamilifu zoezi la kulinda afya ya mama mjamzito, anayenyonyesha na mtoto mwenye umri chini ya miaka mitano. Lengo ni kuhamasisha jamii kuzingatia lishe bora ili kuepukana na hali ya utapiamlo na udumavu," alisema Mfune.

Alisema kazi ya kutoa elimu kwa jamii juu ya suala hilo ilianzia kwenye ngazi ya taifa, mikoa, wilaya na sasa linatekelezwa katika kata na vijiji.

Aliwahimiza kinamama kuhakikisha siku za mwanzo ambazo ni siku 1,000 tangu kutunga mimba, kuzingatia mlo kamili kwa ajili ya kumtengeneza mtoto ili kuepukana na matatizo ya utapiamlo na udumavu.

"Kwenye mikutano yote ya waheshimiwa madiwani, suala ya lishe liwe ajenda ya kwanza. Hakikisheni mnawaalika wataalamu wa lishe watoe elimu angalau muda wa dakika 10. Hii itasaidia jamii kufahamu namna bora ya kuwahudumia watoto," alisema Mfune.

Diwani wa Itamboleo, Lwitiko Mwangosi, alipongeza jitihada hizo na kushauri jukumu hilo liwashirikishe wananchi wote ili kufanikiwa kwa haraka.



Wananchi wakitoa nondo baada ya kituo cha mafuta Mbezi Mwisho, Barabara ya Morogoro, kuvunjwa jijini Dar es Salaam jana, ili kupisha upanuzi wa barabara unaoendelea. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Aonya vurugu uchaguzi wa mitaa

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

MWENYEKITI wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Samwel Jeremiah, amesema atawachukulia hatua za kisheria watu wote watakaosababisha vurugu kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa.

Jeremiah aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Songwe na kusema kama kuna kundi la watu au mtu aliyejiandaa kuvuruga uchaguzi huo, ajisalimishe mapema kwa sababu wamejipanga kuwashughulikia.

Alisema Kamati ya Ulinzi na Usalama ikiongozwa na yeye, imejipanga kufanya doria kwenye maeneo yote ya wilaya na kuwasisitiza wananchi kutoa taarifa pindi wanapobaini kuna viashiria vya uvunjifu wa amani.

"Tumejipanga kuhakikisha uchaguzi wa serikali za mitaa unafanyika kwa uhuru na amani ili wananchi watimize haki yao ya kikatiba ya kumchagua kiongozi wanayemtaka ambaye wanaamini atawaletea maendeleo," alisema Jeremiah.

Aliongeza kuwa kipindi cha uchaguzi vitendo vya uhalifu huongezeka ikiwamo mauaji ya watu wenye ualbino na watoto, hivyo wamejipanga kuwalinda ili wasidhuriwe na watu wanaoamini kwenye mambo hayo.

Jeremiah alisema wameandaa utaratibu mathubuti wa ulinzi dhidi ya watu wenye ualbino na watoto huku akiishauri jamii kuwa makini na wageni wanaowapokea katika maeneo yao hasa kipindi hiki.

Nao wananchi wa Kata ya Mkwajuni wilayani Songwe, walisema suala la kuimarisha doria kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa ni muhimu kwa kuwa litasaidia kuchagua viongozi wanaowataka.

Mmoja wa wananchi hao, George Anthony, alisema alilishauri Jeshi la Polisi kutopuuza taarifa za matukio ya mauaji ya watu wenye ualbino na watoto ambayo huibuka nyakati za uchaguzi yakihusishwa na imani za kishirikina.



HABARI DODOMA

# Miradi ya maji Bahi sasa kufuatiliwa na wananchi

**Na Renatha Msungu,** BAHI

KUTOKANA na changamoto mbalimbali kwenye utekelezaji wa miradi ya maji katika Wilaya ya Bahi, wananchi wametakiwa kuhakikisha wanafuatilia kwa karibu utekelezaji wake ili ukamilika kwa wakati.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa kutambulisha mradi wa uwezo wa jamii na asasi katika kufuatilia rasilimali za umma (PETS) kwenye miradi mbalimbali ya maji wilayani humo, Mratibu wa Mtandao wa Asasi za Kiraia mkoani Dodoma (Ngonedo), Edward Mbogo, alisema wanatarajia kutekeleza mradi huo ili wananchi wafuatilie kwa ukaribu kwenye maeneo yao.

Alisema mradi huo unatarajiwa kutekelezwa katika kata nne za wilaya hiyo ambazo ni Bahi, Mpamatwa, Mundemu na Ibugule.

**Mfano mradi wa maji unaotekelezwa katika Kijiji cha Nguji lakini hakuna wataalam na wasimamizi wa kutosha PETS imekuja wakati muafaka kwa sababu jamii itanufaika.**

Alisema unalenga kuijengea uwezo jamii katika kusimamia rasilimali za umma kwenye sekta ya maji na iweze kuwa na tija kwao.

"Tunalenga kuishirikisha jamii katika upatikanaji wa huduma bora za maji hususani kwenye maeneo ya mradi na utekelezaji wake utafanywa na wananchi na viongozi wa serikali kuanzia ngazi ya vijiji hadi wilaya," alisema.

Mbogo alisema mradi huo utatekelezwa kwa muda wa miezi sita na utaanzia Julai mwaka huu na kiasi cha Sh. milioni 50 kitagharamia mradi huo.

Alieleza kuwa mradi huo utajenga matokeo mazuri kwa wananchi kwa sababu watakuwa wamepata uelewa mzuri baada ya kukamilika.

Aidha alisema utoaji, upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo ya mradi, afya za watumiaji maji zitaimarika.

"Ukitatua tatizo la maji kwa wananchi kunasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza magonjwa ya mlipuko katika maeneo ya vijijini na mijini," alisema.

Naye, Diwani wa Kata ya Mundemu, Golden Senyegalo, alisema kuna changamoto nyingi katika miradi ya maji inayotekelezwa hivyo jamii ikipata uelewa itasaidia kuzitatua.

"Mfano mradi wa maji unaotekelezwa katika Kijiji cha Nguji lakini hakuna wataalamu na wasimamizi wa kutosha PETS imekuja wakati muafaka kwa sababu jamii itanufaika," alisema.

Kwa upande wake, Diwani wa Kata ya Bahi, Augustine Ndonu, alisema jamii ikielimishwa itakuwa ikiwabaini wahujumu wa miradi ya maji jambo ambalo litasaidia kuondoa kero ya ucheleweshaji wa miradi.

Kwa upande wake, Katibu Tawala Wilaya ya Bahi, Jeremia Mafogo, alisema mafunzo hayo yatawapa upeo wananchi jinsi ya kusimamia miradi ya maji itakayotekelezwa kwenye maeneo yao.

## Mhagama awa mbogo mafunzo ujasiriamali kwa vijana

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu, Jenista Mhagama, amewaonya vijana wanaoshiriki mafunzo ya ujasiriamali kuacha mtindo wa kuyapuuza mafunzo wanayopewa huku akitaka hatua zichukuliwe kwa waratibu wa madawati ya vijana walioshindwa kupeleka wawakilishi.

Agizo hilo alilitoa jana na alipokuwa akizindua mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara kwa vijana yaliyofanyika jijini hapa.

Alisema kumekuwa na kawaida ya vijana kutotilia mkazo mafunzo wanayopewa, huku wakitambua kuwa serikali imewekeza fedha nyingi kwa ajili yao ili kuweza kuleta tija kwa taifa.

"Ole wake kijana ambaye atapewa mafunzo na kwenda kulala bila kufanya shughuli iliyokusudiwa maana mmekuwa na kawaida ya kuchukulia poa tu, hapa mmekuja mmepewa mafunzo ambayo tumeyagharamia, mkitoka mnasema ni yale yale nasema ole wenu."

"Haki ya nani atanitambua hakuna kupotezeana muda, wiki tatu tumeandaa halafu mtu akitoka hapa aseme yale yale tu ole wako, na anayeona hawezi haya mafunzo aondoke, tumechoka vijana kutokubadilika wala kubadili mtazamo," alisema.

Akizungumzia kuhusu waratibu wa madawati hao, Mhagama alisema baadhi ya mikoa imeshindwa kuleta wawakilishi kwenye mafunzo hayo ikiwamo Dar es Salaam, Pwani, Singida, Njombe, Iringa, na Rukwa.

Alisema kutokana na hali hiyo waratibu wa madawati ambao watabainika wameshindwa kupeleka wawakilishi hao kwa uzembe waondolewe kwenye nafasi zao.

Sambamba na hilo, aliliagiza Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi (NEEC) kuhakikisha linasimamia taasisi za fedha kutengeneza riba rafiki kwa vijana kwa kuwa masharti ya mikopo kwa vijana ni makubwa.

Alisema kumekuwa na changamoto ya kutokuwa na riba rafiki kwa vijana huku wengine wakitakiwa kuweka dhamana ili wapate mikopo wakati uwezo huo hawana.

"NEEC naagiza mhakikishe mnasimamia taasisi za fedha tulizonazo kutengeneza riba rafiki kwa vijana kwa kuwa masharti ya mikopo kwa vijana ni makubwa sana," alisema.

Aidha, alisema yawekwe masharti rafiki kwao lakini na namna ya kuwabana ili kurejesha fedha wanazokopa.

"Kama mnavyojua kukopa ni harusi kulipa ni matanga, sasa hapa lazima nalo mwelewe, tunataka vijana wasimamie wachangie uchumi wa nchi," alisema.



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, akizungumza katika uzinduzi rasmi wa jina jipya la Sekondari ya Fountain Gate Academy, iliyopo eneo la Miyuji, jijini Dodoma jana. Shule hiyo awali ilikuwa ikiitwa Azimio Sekondari. Kushoto ni Mkurugenzi wa shule hizo, Japhet Makau na walimu wa shule hiyo. **PICHA NA IBRAHIM JOSEPH**

# Ugonjwa wa ini unaua 'kimya kimya'

**Na Mwandishi wetu,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa ugonjwa wa homa ya ini ni miongoni mwa magonjwa yanayoua watu kimya kimya, hivyo wananchi wametakiwa kuwa na tabia ya kupima afya zao ili kukabiliana nao.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamini Mkapa(BMH), Dk. Alphonce Chandika, katika maadhimisho ya Siku ya Homa ya Ini iliyokuwa na kauli mbiu, 'Wekeza katika mapambano dhidi ya homa ya ini'.

Alisema ugonjwa huo ni hatari kutokana na dalili zake kutokuwa za wazi jambo ambalo linafanya watu kuchelewa kugundulika hivyo jamii ijenge tabia ya kupima afya zao.

Alibainisha kuwa kambi ya uchunguzi iliyopo hospitalini hapo kati ya watu 400 waliofanyiwa uchunguzi, 13 wamekutwa na ugonjwa wa homa ya ini.

"Sasa tujiulize kwa ndugu au watu wali-ohusiana nao huko kabla ya kujulikana hali zao zikoje na usalama wao ukoje, maana pia kuna changamoto kwenye kuhudumia wagonjwa wa namna hii," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema pamoja na juhudi za serikali za kutoa chanjo ya ugonjwa huo kwa watoto, lakini bado kuna makundi ambayo yanatakiwa kutazamwa na watumishi wake kupewa chanjo ikiwa ni pamoja na watoa huduma za afya na polisi.

"Kuna makundi ambayo yanatakiwa kupewa msukumo kwa kuwapa chanjo watumishi wake kama watoa huduma za afya na polisi ambao wamekuwa wakihudumia maiti na majeruhi mbalimbali bila kujua kama wana ugonjwa huo,"alisema.

Dk. Chandika alisema katika kuunga mkono juhudi za serikali za mapambano na ugonjwa huo, watumishi wa afya 170 wa Hospitali ya Benjamini Mkapa wamepewa chanjo ya ugonjwa huo.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi wa Kinga Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Janneth Mghamba, alisema ugonjwa huo ni mbaya kwa watoto ambapo kati ya asilimia 50 hadi 60 ya watoto walioambukizwa virusi vya homa ya ini wanakabiliwa na magonjwa ya kudumu.

"Ugonjwa huu ni hatari ingawa jamii haitoi msukumo kwa mwaka 2016, kati ya watoto 200, 000 waliopima asilimia 12 kati ya asilimia 50 hadi 60 ya watoto walipata maambukizi ya homa ya ini wanakumbwa na magonjwa ya kudumu," alisema.

Alieleza kuwa kutokana na hatari hiyo serikali imefanya juhudi mbalimbali za kupunguza maambukizi mapya ya homa ya ini kwa asilimia 90 ifikapo mwaka 2030 na kupunguza vifo vinavyotokana na ugonjwa huo kwa asilimia 65.

Naye Mwakilishi wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Dk. Christine Msanu, alisema nchi nyingi ziko nyuma katika uchunguzi na kutibu homa ya ini hivyo kuna haja ya kuongeza juhudi za mpambano.

# Wahitimu itikadi wafunzwa fursa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MJUMBE wa Kamati ya Siasa ya Mkoa wa Magharibi kichama, Ayoub Mohammed Mahmoud, amewataka wahitimu wa madarasa ya itikadi ya Chama Cha Mapinduzi Jimbo la Bububu kutumia mafunzo waliyoyapata kuimarisha umoja na ushirikiano kama moja ya mbinu za kukipatia ushindi chama hicho.

Akihutubia wahitimu hao na viongozi wa ngazi mbalimbali wa ndani na nje ya Wilaya ya Mfenesini, alisema kufanya hivyo kutaongeza uimara wa chama hicho na kupelekea ushindi wa mapema.

Alisema Chama Cha Mapinduzi kimeamua kuwafunza itikadi vijana wanaochipukia ili watambue historia ya nchi yao ili kukuza mapenzi ya chama na viongozi wake hivyo wahitimu hao wanapaswa kuwa mabalozi wazuri kwa kukisemea vyema chama na serikali zao.

Alisema iwapo vijana hao na viongozi wa CCM wa wilaya hiyo watashirikiana kuelezea mafanikio yaliyopatikana kupitia utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya chama hicho, watasaidia kujenga uelewa wa jamii na kuwavutia kuendelea kukiunga mkono.

Aidha, Ayoub ambaye pia ni Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi aliwaasa viongozi wenye watu wa kuwania nafasi za uongozi katika uchaguzi mkuu wa 2020 kuacha kufanya hivyo badala yake washirikiane na viongozi waliopo kutekeleza ilani ya uchaguzi ya 2015 – 2020 na kwamba hatosita kutoa taarifa zao katika vikao halali vya uteuzi wakati utakapofika.

Katika hatua nyengine Ayoub alipongeza ushirikiano uliopo kati ya Chama Cha Mapinduzi wilayani humo na Wilaya ya Kinondoni Dar es Salaam ambao alisema utasaidia kuimarisha Muungano wa Tanzania, lakini kujifunza mbinu na mikakati mbalimbali ya kukiimarisha chama katika wilaya hizo.

Akizungungumza katika hafla hiyo mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kinondoni aliwasihi vijana kuwa na mapenzi ya kweli kwa chama chao na kukipigania ili kiendelee kushika dola katika pande zote mbili za muungano.

Alisema waasisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliweza kupigania uhuru na kuzikomboa nchi mbili hizo kutokana na kuwa na itikadi ya kweli kwa chama na nchi yao jambo linalotakiwa kuendelezwa na kila mwanachama wa CCM bila ya kujali cheo au dhamana aliyonayo.

Akisoma taarifa kuhusu masomo hayo Katibu wa CCM Jimbo la Bububu, Zaituni Tawakal Khairallah, alisema katika mafunzo hayo ya miezi mitatu jumla ya vijana 600 wanawake 420 na wanaume 180 walipatiwa mafunzo ya nadharia na vitendo.

Alisema vijana hao kutoka matawi manane yaliyomo katika jimbo hilo, walifundishwa historia, itikadi na uzalendo jambo lililowaongeza uwezo wa kujitambua, ujasiri na uzalendo kwa nchi na chama chao.

# China yaweka bayana misaada kwa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Watu wa China imesema misaada yake inayotoa inalenga katika kuimarisha uchumi na huduma za jamii kwa wananchi wa Zanzibar.

Hayo yalisemwa na Balozi Mdogo wa China aliyeko Zanzibar, Xie Xiaowu, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika hoteli ya Verder, Mtoni Unguja.

Alisema uhusiano wa China na Zanzibar ulianza baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Januari 12, 1964 ikiwa miongoni mwa nchi za mwanzo kuyatambua mapinduzi hayo matukufu na kusaidia sekta mbalimbali ikiwamo ujenzi wa viwanda.

Balozi huyo alisema uhusiano huo umekuwa ukiendelea katika nyanja mbalimbali ikiwamo China kutoa madaktari bingwa kwa ajili ya kusaidia huduma za afya kwa wananchi wa Zanzibar.

**Uhusiano wa China na Zanzibar ulianza baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Januari 12, 1964 ikiwa miongoni mwa nchi za mwanzo kuyatambua mapinduzi hayo matukufu na kusaidia sekta mbalimbali ikiwamo ujenzi wa viwanda.**

Kwa mujibu wa balozi huyo, ujenzi wa Hospitali ya Abdalla Mzee, mkoani Pemba, ni mfano wa ushirikiano kati ya China na Zanzibar katika sekta ya afya.

Alisema kwa muda wa miaka 55 sasa, China imekuwa ikipeleka madaktari bingwa Zanzibar na kutoa matibabu ya aina mbalimbali na sasa ni awamu ya 29 ya timu ya madaktari 740 kutoa huduma za kiafya visiwani hapa. Alisema timu ya madaktari hao wamewatibu zaidi ya wagonjwa milioni saba, huku wakifanya upasuaji kwa wagonjwa 200,000 pamoja na kuokoa maisha ya wagonjwa 40,000 waliokuwa katika hali mbaya za kiafya.

"Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China itaendelea kushirikiana na Zanzibar katika kuimarisha sekta ya afya ikiwamo mradi wa kupambana na ugonjwa wa kichocho ambao ni hatari kwa afya za watoto na wanafunzi wa shule," alisema.

Aidha, Balozi Xiea alisema ni matarajio yake makubwa kwamba msaada wa jumla ya Sh. bilioni 34 zilizotolewa na nchi hiyo utatumika vizuri kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za madaktari bingwa katika Hospitali ya Abdalla Mzee na uimarishaji wa mitambo ya kurushia matangazo ya vyombo vya habari vya serikali ya Zanzibar.

"Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China tumetoa msaada jumla ya Sh. bilioni 34 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika hospitali ya kisasa ya Abdalla Mzee huko Pemba. Msaada huo pia utatumika kwa ajili ya kuimarisha mawasiliano ya mitambo vya Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC)," alisema.

Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO) Zanzibar, Dk.Juma Mohamed, alisema Zanzibar inathamini misaada mbalimbali inayotolewa na China ambayo imekuwa kichocheo cha kukuza uchumi na mawasiliano.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya TPB, Sabasaba Moshingi (wa pili kulia), akiwa na Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Thobias Mwalapwa (wa tatu kulia), pamoja na viongozi na wanafunzi wa Shule ya Msingi Pande, baada ya kukabidhi msaada wa madawati 50, meza pamoja na viti vitatu vyenye thamani ya Sh. milioni tano, kwa ajili ya shule hiyo, juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Waziri aahidi huduma bora za afya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya Zanzibar, Hamad Rashid Mohammed, amesema serikali itaendelea kutoa huduma bora za matibabu kwa jamii ili kuhakikisha wanapata huduma zinazostahili.

Aliyasema hayo jana wakati akipokea msaada wa vifaa mbalimbali vya tiba kutoka taasisi ya Muzdalifa chini ya ufadhili wa Shirika la Kusaidia Huduma za Jamii Marekani (HHRD) katika hafla iliyofanyika ukumbi wa Wizara ya Afya Mnazi Mmoja.

Alisema hatua hiyo itasaidia upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi ili kuepusha kufuata matibabu nje ya nchi.

Waziri Hamad, alisema ni jambo la faraja kwa taasisi ya Muzdalifa kuunga mkono serikali kwa kuwasogezea huduma za tiba kwa wananchi ili kwenda sambamba na mikakati ya serikali katika kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma bora bila malipo.

Aidha, alisema kuwa kuna baadhi ya taasisi hupata misaada kama hiyo lakini haiwafikii walengwa kwa kujimilikisha wao wenyewe kwa maslahi yao.

Hivyo aliipongeza taasisi hiyo kuwa wasimamizi wazuri ambao wanapokea msaada mbalimbali na kuwafikia walengwa.

Alisema kuwapo na utaratibu maalum wa kuorodhesha mahitaji ya vifaa vya tiba vinavyohitajika ili kuweza kuziba pengo la mahitaji yaliyopo.

"Tusipoorodhesha mahitaji yetu ya vifaa tutasababisha wingi wa vifaa ambavyo hatuvihitaji na kuvitumia kwa fujo," alisema waziri.

Hivyo aliishukuru taasisi hiyo kwa kuwaletea msaada huo na kuahidi kuwafikia walenga na kuwa pamoja na serikali.

Hata hivyo, aliwataka wazee na walemavu kueleza changamoto zao zinazowakabili ili kuweza kufanyiwa kazi na serikali pamoja na taasisi zinazojitolea.

Naye Mwenyekiti wa Taasisi ya Muzdalifa, Shekh Abdalla Ghadhal, alisema taasisi yake itaendelea kushirikiana na serikali kwa kuwapatia vifaa vya matibabu kwa wananchi kila wapatapo misaada kwa wahisani.

Vifaa vyenyewe ni vitanda vya uchunguzi, magongo na viti vya walemavu, pempasi, viti vya kubebea wagonjwa, sabuni, vifaa vya usafi, nguo za wagonjwa, glovu, na vyenginevyo.

# Stiegler's Gorge fursa kwa Dawasa

Na Frank Monyo

OFISA Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (Dawasa), Mhandisi Cyprian Luhemeja, amesema watatumia fursa ya mradi wa kuzalisha umeme katika Mto Rufiji (Stiegler's Gorge) kwa kuangalia namna ya kujenga mtambo na kuanza kuzalisha maji kwa ajili ya kusambaza kwa wananchi.

Pia Dawasa wameweza kuwa moja ya chachu ya mradi huo kwa kukarabati mradi wa maji uliojengwa miaka ya 1970 kwa ajili ya kutoa huduma katika kambi ya ujenzi wa mradi wa uzalishaji umeme wa Rufiji mkoani Pwani ambao utakamilika Juni 2022 na kuzalisha megawati 2115.

**Mradi huo wa maji utawasaidia makandarasi kuwa na miundombinu wezeshi itakayowapatia maji muda wote wa matumizi yao ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi.**

Akizungumza baada ya shughuli za uwekaji jiwe la msingi lililowekwa na Rais Magufuli mwishoni mwa wiki, Mhandisi Luhemeja, alisema lengo la Dawasa ni kutoa maji kutoka maporomoko ya Stieglers Gorge kwenda kwa wananchi na mchakato huo tayari umeanza ikiwamo kuunda timu ya wahandisi wa mradi kufanya usanifu ikiwa ni maandalizi ya kuanza kwa utekelezaji wake huku fedha zitakazotumika zikiwa ni za ndani.

"Utekelezaji wa mradi huu mkubwa utasaidia kuondoa ukosefu wa majisafi na salama kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam na maeneo ya mkoa wa Pwani na kuifanya Dar es Salaam kuwa salama zaidi kwa matumizi ya majisafi na salama," alisema.

Alisema mradi wa maji kutoka maporomoko ya Mto Rufiji (Stiegler's Gorge), umesimamiwa na Dawasa na kugharimu Sh. milioni 604.9 na ulikamilika Agosti mwaka jana ukiwa na uwezo kuzalisha maji lita 209,000 kwa ajili ya matumizi ya kambi ya ujenzi wa mradi wa umeme.

Vile vile, alisema mradi huo wa maji utawasaidia makandarasi kuwa na miundombinu wezeshi itakayowapatia maji muda wote wa matumizi yao ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa na kusaidia mradi wa ujenzi wa bwawa la kufua umeme kukamilika kwa wakati.

"Dawasa walikarabati miundombinu iliyokuwa chakavu ikiwamo ukarabati wa eneo la chanzo pamoja na ufungaji wa pampu moja mpya itakayokuwa na uwezo wa kuchota maji mtoni kiasi cha lita 2.41 kwa sekunde, ulazaji wa mabomba ya kusambazia maji na urefu wa kilomita 1,463 kutoka mahali maji yanapopatikana na mradi huo utapeleka maji kwenye matangi makubwa mawili," alisema Luhemeja na kuongeza:

"Katika ukarabati huo pia kulilazwa bomba la kusafirishia maji (GS pipe) kipenyo cha nchi tatu, ujenzi wa bomba jipya la plastiki (HDPE) la kusafirishia majighafi kutoka Mto Rufiji hadi kwenye tangi na kituo cha kusafisha maji, ukarabati wa kituo cha kusafisha maji, ujenzi wa kituo cha kusukuma maji, ujenzi wa bomba la kusafirishia maji, ukarabati wa matangi mawili ya zamani ya lita 12,500 na 22,500 na ufungaji wa dira za maji, 'air valve 4' na 'gate valve 4'," alisema.



Mmoja ya waanzilishi wa mpango wa "Her Africa", Zena Tenga (kushoto), na mwezeshaji, Erica Zilinde, wakiongea na wanafunzi wa kike wa kidato cha 1 na 2 wa Shule ya Sekondari Chang'ombe, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu fikra potofu na miiko juu ya hedhi kama sehemu ya kampeni ya mpango uitwao "Hedhi yangu, Furaha yangu", inayolenga kuelimisha wasichana juu ya hedhi salama na pia kutoa vifaa vya hedhi kwa wasichana nchini Tanzania. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Mkakati mazalia vimelea vya magonjwa

Na Waandishi Wetu, MAELEZO

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amezindua mkakati wa kudhibiti mbu na wadudu wadhurifu, uliofanyika kitaifa katika Viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki.

Waziri Ummy alisema mkakati huo ni mahsusi kwa ajili ya kudhibiti wadudu wadhurifu wakiwamo mbu, nzi weusi, Mbung'o/Ndorobo, kunguni, kupe, nzi, konokono, viroboto, panya, mende na papasi ambao wanasababisha magonjwa mbalimbali kwa jamii.

Alisema kutokana na wadudu hao kusababisha magonjwa ya aina tofauti, ugonjwa wa malaria umekuwa ukipunguza nguvu kazi ya taifa kwa asilimia kubwa kutokana na kuongezeka kwa mazalia ya mbu katika makazi.

"Kumekuwa na wadudu ambao wamekuwa wakisababisha magonjwa mbalimbali kwa wananchi ambayo ni pamoja na malaria, homa ya dengue, mabusha na matende, oma ya bonde la ufa, chikungunya, homa ya manjano na zika na katika mkakati huu wa kitaifa lengo ni kuwadhibiti kabisa," alisema Waziri Ummy.

Katika kuangamiza wadudu hao, Wakurugenzi wa Manispaa za Dar es Salaam walitoa Sh. milioni 5.5 kwa kununua dawa ya kuua wadudu warukao na watambaao ambao ni wasababishaji wa magonjwa mbalimbali.

Vile vile, Waziri ummy alitoa wito kwa taasisi za umma kushiriki kwa ukamilifu na wadau wa maendeleo kwenye kufanya usafi, kuangamiza mazalia ya mbu, kujikinga na kuumwa na mbu, kunyunyizia viuadudu katika mazalia yao, kuharibu mazalia, kuua wadudu wapevu kwa njia ya kupuliza dawa na viuatilifu.

Alisema serikali imenunua mashine nne za kisasa ambazo zitasaidia kupulizia na kuua wadudu kwa umbali mrefu, mashine hizo ambazo tatu zipo Dar es Salaam na moja mkoani Tanga, zinatarajiwa kuongezewa nguvu na mashine nyingine nne ambazo zitanunuliwa na kugawiwa kwenye mikoa mbalimbali.

Aliwataka wakazi wa Jiji la Dar es Salaam na mikoa mingine nchini kuzunguka katika maeneo yao na kupulizia dawa, ili kuangamiza mazalia yao.

Waziri wa Ofisi ya Rais Tamisemi, Selemani Jafo, alitoa maagizo kwa manispaa zote nchini kuhakikisha ifikapo Januari mwaka 2020, wawe wamenunua mashine za kupulizia dawa katika mazalia ya wadudu, pamoja na kuanzisha kampeni maalum za mtaa kwa mtaa kudhibiti na kutokomeza kabisa wadudu wanaosababisha magonjwa mbalimbali.

# Awacharukia wanaoponda ndege za JPM

Na Marco Maduhu, KISHAPU

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani Shinyanga, Mabala Mlolwa, amelaani kitendo cha watu wachache wanaobeza ndege saba zilizonunuliwa na serikali, kwa madai haziwasaidii chochote.

Mlolwa alibaini hayo juzi wilayani Kishapu wakati akizindua kampeni ya Kishapu ya kijani. ambayo imelenga kuwapatia ushindi wa kishindo wagombea wote wa CCM kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu wa 2020.

Alisema mambo anayoyafanya Rais John Magufuli siyo ya kubezwa bali anapaswa kupongezwa, ikiwa ameliletea maendeleo taifa kwa muda mfupi ikiwamo ujenzi wa barabara, zahanati, vituo vya afya, hospitali, elimu bure, nyumba za maaskari, reli, pamoja na ununuaji wa hizo ndege saba.

"Mimi huwa nawashangaa sana watu ambao wamekuwa wakibeza mambo ambayo anayafanya Rais wetu hasa kwenye ununuaji wa ndege hizi, utawasikia vijiweni na mitandaoni wakisema eti hizo ndege hazina msaada kwetu sisi, wananufaika tu matajiri na wafanyabiashara, lakini sisi wanyonge hatuna faida nazo yaani walaaniwe," alisema Mlolwa.

"Hivi hawajui ndege hizi ndizo zinaongeza pato la taifa, wafanyabiashara na wazungu wanapopanda hizo ndege ndipo serikali inapata fedha, ambazo zitashuka huku kwetu na kutuletea maendeleo, ikiwamo ujenzi wa reli, vituo vya afya, upatikanaji wa dawa, miradi ya maji, barabara, na hizo ndizo faida msiwe mnaongea ongea tu," aliongeza.

Katika hatua nyingine aliwataka wanachama wa CCM na viongozi, pale watakapokuwa wakipiga kura za maoni, wasipitishe wagombea ambao hawana sifa na kutokubalika na wananchi, ili kuwarahisishia kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu mwakani kushinda kwa kishindo.

ITV

JARIDA LA WANAWAKE: SAA 1:00 USIKU

LEO BLANDINA SEMBU ATAKUWA NA MAMA ARERIA MKONGWA ALMAARUFU MAMA KUCHII MFUGAJI WA KUKU WA KIENYEJI AINA YA KUCHI KWA SASA PIA ANATENGENEZA CHAKULA ASILI CHA KUKU AKIWA KANUNUA MASHINE ZA KUTENGENEZA CHAKULA CHA KUKU.

# TANGAZO

China Commercial Bank
中國商業銀行

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 MACHI, 2019
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 30.06.2019 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 31.03.2019 |
|---|---|---|---|
| | **A. MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 432 | 261 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 3,000 | 5,476 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 3,000 | 1,500 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 52 | 18 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 22 | 1 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 1,466 | 1,474 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 477 | 546 |
| 12 | Mali Nyingine | 1,069 | 1,253 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 0 | 0 |
| 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 45 | 140 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **9,563** | **10,669** |
| | **B.DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 0 | 0 |
| 18 | Amana za Wateja | 1,485 | 1,724 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana Maalumu | 0 | 0 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 0 | 0 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 182 | 217 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 167 | 41 |
| 27 | Dhima Nyingine | 1,477 | 1,949 |
| 28 | Madeni | 0 | 0 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **3,311** | **3,931** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29)* | **6,252** | **6,738** |
| | **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 20,881 | 20,881 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 5 | 5 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (13,701) | (13,701) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (1,043) | (557) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 110 | 110 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **6,252** | **6,738** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 8,560 | 8,277 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 328 | 328 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 275 | 187 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 4,630 | 4,630 |
| | **D.BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 65% | 63% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 44% | 45% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 51% | 43% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 5% | 5% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 52% | 33% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -14% | -57% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -10% | -17% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2019
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya mwaka sasa 30-Jun-19 | Robo ya mwaka linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Jun-18 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-19 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Jun-18 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 54 | 340 | 168 | 887 |
| 2 Gharama za Riba | - | (88) | - | (290) |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **54** | **252** | **168** | **596** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | | - | |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (97) | - | (201) | - |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba**: | **142** | **99** | **282** | **181** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha | (3) | 7 | 9 | 10 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 145 | 93 | 267 | 172 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 1 | (2) | 7 | (2) |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **(585)** | **(959)** | **(1,292)** | **(2,035)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 160 | 276 | 337 | 495 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 11 | 26 | 53 | 209 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 414 | 658 | 901 | 1,332 |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(486)** | **(608)** | **(1,043)** | **(1,258)** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | - | - | - | - |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(486)** | **(608)** | **(1,043)** | **(1,258)** |
| 11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| **12 Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(486)** | **(608)** | **(1,043)** | **(1,258)** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 17 | 23 | 17 | 23 |
| 14 Mapato kwa Hisa | -744 | -932 | -1,598 | -1,607 |
| 15 Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| **Baadhi ya viashirio vya Ufanisi** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -5% | -3% | -9% | -1% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -7% | -4% | -16% | -2% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 298% | 273% | 287% | 191% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 1% | 7% | 4% | 6% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho.**

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI, 2019
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya | Mengineyo (bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Robo Mwaka ya sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa Robo mwaka** | **20,881** | **-** | **(14,258)** | **110** | **5** | **-** | **6,738** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (486) | - | - | - | **(486)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa Robo mwaka ya sasa** | **20,881** | **-** | **(14,744)** | **110** | **5** | **-** | **6,252** |
| **Robo Mwaka iliyopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa Robo mwaka** | **20,881** | **-** | **(14,131)** | **110** | **5** | **-** | **6,865** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (557) | - | - | - | **(557)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | 430 | - | - | - | **430** |
| **Salio la mwisho wa mwaka Iliyopita** | **20,881** | - | **(14,258)** | **110** | **5** | **-** | **6,738** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI, 2019
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo Mwaka ya sasa 30-Jun-19 | Robo Mwaka iliyopita 31-Mar-19 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30-Jun-19 | Limbikizo la Mwaka linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Jun-18 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za uendeshaji** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | (486) | (557) | (1,043) | (1,258) |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | 0 | 0 |
| - Hasara Katika Mali | 293 | 299 | 592 | 440 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (26) | 16 | (10) | 332 |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | 0 | (3) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (236) | (2,268) | (2,504) | (1,912) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi | - | - | 0 | 2,830 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (381) | (6) | (387) | 907 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 84 | 176 | 260 | (876) |
| - Kodi Iliyolipwa | (9) | - | (9) | (9) |
| - Mengineyo (bainisha) | - | | | 0 |
| **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(761)** | **(2,340)** | **(3,100)** | **451** |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (1) | (7) | (8) | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | | - | 15 |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | (1,500) | - | (1,500) | (1,500) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(1,501)** | **(7)** | **(1,508)** | **(1,485)** |
| **III Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **-** | **-** | **-** | **-** |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (2,262) | (2,347) | (4,608) | (1,034) |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 5,529 | 7,875 | 7,875 | 10,616 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **3,267** | **5,529** | **3,267** | **9,582** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI, 2019

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| Jina | Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Xiong Zhenglin | Ofisa Mtendaji Mkuu | ............................ | **29.07.2019** |
| Fadhili Sanga | Mkuu wa Fedha | ............................ | **29.07.2019** |
| Victoria Edward | Mkaguzi Mkuu wa Ndani | ............................... | **29.07.2019** |

Sisi tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa Taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathimini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa Taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| Jina | Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Liu Lin | Mwenyekiti wa bodi | ............................ | 29.07.2019 |
| Chao Jiang | Mjumbe wa bodi | ............................ | 29.07.2019 |

## The Banking and Financial Institutions (Disclosures) Regulations, 2014
## MINIMUM DISCLOSURES OF CHARGES AND FEES
## (Made under Regulation 11)

| No. | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | **Current Accounts** | **TZS** | | **USD** | |
| | (a) Required minimum opening balance | | | | |
| | Personal Current Account | TZS | 100,000.00 | $ | 100.00 |
| | Business Account | TZS | 200,000.00 | $ | 200.00 |
| | Imperial Business Account | TZS | 5,000,000.00 | $ | 5,000.00 |
| | Community Account | TZS | 200,000.00 | $ | 200.00 |
| | Call Account | TZS | 10,000,000.00 | $ | 10,000.00 |
| | (b) Monthly service fee (break down per customer type) | | | | |
| | Personal Current Account | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | Business Account | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | Imperial Business Account | TZS | 25,960.00 | $ | 25.96 |
| | Community Account | Free | | Free | |
| | Call Account | Free | | Free | |
| | (c) Cheque withdrawal over the counter | TZS | 1,947.00 | 0.75% of withdrawal amount | |
| | (d) Fees per ATM Withdrawal | | | | |
| | Personal Savings (5 free withdrawals per month) | TZS | 1,300.00 | $ | - |
| | Imperial Savings (5 free withdrawals per month) | TZS | 1,300.00 | $ | - |
| | Student Boom Account | TZS | - | $ | - |
| | Junior Savings Account | TZS | - | $ | - |
| | Senior Savings Account (3 free withdrawals per month) | TZS | 1,300.00 | $ | - |
| | Personal Current Account | TZS | 1,300.00 | $ | - |
| | (e) ATM mini statement | TZS | 300.00 | $ | - |
| | (f) Interim statement (Below 3 months) | TZS | 3,894.00 | $ | 2.60 |
| | (g) Periodic scheduled statement | Free | | Free | |
| | (h) Cheque book (per leaf) | TZS | 519.20 | $ | 0.52 |
| | (i) Dishonoured Cheque | | | | |
| | Inward Unpaid Cheque | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | Outward Unpaid Cheque | TZS | 38,940.00 | $ | 38.94 |
| | (j) Special clearance | | | | |
| | Personal Accounts | TZS | 51,920.00 | $ | 51.92 |
| | Business Accounts | TZS | 64,900.00 | $ | 64.90 |
| | (k) Counter cheque (per leaf) | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | (l) Stop payment (per leaf) | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | (m) Standing order | | | | |
| | Internal | Free | | Free | |
| | External | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | Unpaid | TZS | 6,490.00 | $ | 6.49 |
| | (n) Balance enquiry | Free | | Free | |
| | (o) New ATM card issuance | Free | | Free | |
| | (p) ATM card renewal or replacement | TZS | 12,980.00 | $ | - |
| | (q) Overdrawn Account interest charge | 10% above the Banks Base Lending Rate | | | |
| | (r) Unarranged overdraft | 10% above the Banks Base Lending Rate | | | |
| | (s) Interbank transfer | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | (t) Bill payments through ATM | TZS | 713.90 | $ | - |
| | (u) Deposit fee | Free | | Free | |
| | (v) Other (please specify) | | | | |
| | ATM withdrawal limit per transaction | TZS | 400,000.00 | $ | - |
| | ATM withdrawal daily limit | TZS | 1,000,000.00 | $ | - |
| 2 | **Savings Accounts** | | | | |
| | (a) Required minimum opening balance | | | | |
| | Personal Savings Account | TZS | 50,000.00 | $ | 50.00 |
| | Student Boom | TZS | 20,000.00 | $ | 20.00 |
| | Senior Savings Account | TZS | 50,000.00 | $ | 50.00 |
| | Joint Savings Account | TZS | 50,000.00 | $ | 50.00 |
| | Imperial Savings Account | TZS | 2,000,000.00 | $ | 2,000.00 |
| | Junior Savings Account | TZS | 10,000.00 | $ | 10.00 |
| | (b) Monthly service fee | | | | |
| | Personal Savings Account | TZS | 9,086.00 | $ | 9.09 |
| | Student Boom | Free | | Free | |
| | Senior Savings Account | TZS | 9,086.00 | $ | 9,086.00 |
| | Joint Savings Account | TZS | 9,086.00 | $ | 9,086.00 |
| | Imperial Savings Account | TZS | 19,470.00 | $ | 19.47 |
| | - Imperial Savings Account | TZS | - | $ | - |
| | - Imperial Savings Account | TZS | - | $ | - |
| | - Junior Savings Account | TZS | - | $ | - |
| | (e) Deposit rate (Personal savings accounts) | | 2.5% | $ | 0.01 |
| 3 | **Electronic Banking** | | Free | | Free |
| | (a) Internet Banking monthly fee | | FREE | | FREE |
| | (b) Internet transfers | | FREE | | FREE |
| | (c )SMS Banking | | NA | | NA |
| | (d) Other | | | | |
| | E-Banking Statement request(Self downloaded) | | FREE | | FREE |
| | E-Banking Password resetting | | FREE | | FREE |
| | E-Banking Statement request (printed by the Bank) per page | | TZS 1,298 | | $1.298 |
| 4 | **Foreign Exchange Transaction** | | | | |
| | (a) Purchase/sale of TCs transactions over the counter | | - | | - |
| | (b) Purchase of foreign cheque | | - | | - |
| | (c) Sale/Purchase of cash passport | | - | | - |
| | (d) Telegraphic Transfer (TISS/RTGS) | | | | |
| | Outward TT | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | Inward TT | | Free | | Free |
| | (e) Telex/Swift | | | | |
| | Outward TT | | | $ | 64.90 |
| | Inward TT | | | $ | 12.98 |
| | (f) Transfer from foreign currency denominated Account to local current Account ( within bank and to other bank) | | - | | - |
| 5 | **Loans** | | | | |
| | (a) Processing/Arrangement/Appraisal fee | | | | |
| | (i) Personal loans | 2% of the facility amount | | | |
| | (ii) Overdrafts | 2% of the facility amount | | | |
| | (iii) Mortgage finance | 2% of the facility amount | | | |
| | (iv) Asset finance | 2% of the facility amount | | | |
| | (b) Unpaid loan instalment | 10% above interest rate | | | |
| | (c) Early repayment | 3% of amount to be settled early | | | |
| | (d) Valuation fees | As per service provider rates | | | |
| | (e) Legal Fees | As per service provider rates | | | |
| | (f) Base Lending Rates | | 21% | $ | 0.09 |
| | (g) Maximum Spread Above the Base Lending Rate (BLR) | | 5% | $ | 0.05 |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name | Signature | Designation | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Xiong Zhenglin | | Chief Executive Officer | 29.07.2019 |
| 2 | Joseph Phales | | Ag: Head of Business & Operations | 29.07.2019 |

215350502

# Kabigi kupumzishwa nyumba ya milele leo

**Na Romana Mallya**



MWILI wa mwanahabari mbobezi Agnes Kabigi (53), aliyefariki dunia ghafla Ijumaa iliyopita akiwa kazini Kahama, unatarajiwa kuagwa leo na baadaye kuzikwa kwenye makaburi yaliyopo Bahari Beach kwa Kondo, jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa jana, mwili huo baada ya kuwasili nyumbani kwao Mbezi Beach, kutafanyika ibada na kufuatiwa na salamu za rambirambi kutoka taasisi mbalimbali.

Baadhi ya taasisi ambazo zitatoa salamu za rambirambi ni pamoja na Jukwaa la Fursa, Zanaki, Chama cha Wanahabari Wanawake (Tamwa), Shirika la Kimataifa la AGPAHI, alikokuwa akifanya kazi hadi umauti unamkuta. Ratiba hiyo inaonyesha ibada ya mazishi itaanza saa 6:00 hadi saa 7:30 mchana na kufuatiwa na salama za rambirambi na saa 8:00 hadi saa 9:00 alasiri waombolezaji watatoa heshima za mwisho.

Mwili wa Agnes utaondoka nyumbani saa 9 alasiri kwenda kwenye nyumba yake ya milele.

Agnes alifariki dunia Ijumaa na taarifa za kifo chake zilisambaa kwenye mitandao ya kijamii na baadaye kuthibitishwa na Mkurugenzi wa Shirika la AGPAHI, Dk. Sekele Mwakyusa.

Dk. Mwakyusa aliliambia Nipashe kuwa, Kabigi alifikwa na umauti akiwa mkoani Shinyanga kwa shughuli za kikazi.

Alisema Kabigi alijiunga na shirika hilo Julai, mwaka jana akiwa Meneja Mawasiliano na mwili wake ulisafirishwa kutoka Kahama kwenda Dar es Salaam, Jumamosi.

# NCCR yatangaza safu mpya uongozi

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha NCCR-Mageuzi kimetangaza safu mpya ya uongozi, huku kikimchagua James Mbatia kuendelea na nafasi ya uenyekiti.

Akitangaza uongozi mpya ngazi ya taifa ya chama hicho mbele ya waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mbatia alisema amerudi tena katika nafasi yake hiyo baada ya kuombwa na wanachama wa chama hicho kwa kipindi kirefu.

Mbatia alisema mchakato wa kupata viongozi hao wapya ulichukua muda mrefu kwa kuwa alikuwa amekataa kurudi tena katika nafasi hiyo.

"Tumekaa kimya kwa kipindi kirefu kidogo bila kuchagua viongozi wapya, na moja ya sababu iliyochelewesha ni mimi ambaye nilikuwa nimekataa kurudia tena katika nafasi hii, niliwaomba wanachama wamchague mtu mwingine, lakini baada ya msuguano wa muda mrefu na wanachama wakaendelea kuniomba, nikawakubalia.

"Waliniomba wakasema kutokana na utulivu wa fikra na namna mambo ya siasa yanavyoendelea na changamoto kadha wa kadha tulizopitia na nashukuru tumemaliza hili," Mbatia alisema.

Kiongozi huyo wa NCCR-Mageuzi alisema viongozi hao walichaguliwa katika mkutano mkuu uliofanyika mwishoni mwa wiki.

Alimtaja Makamu Mwenyekiti Bara aliyechaguliwa katika mkutano huo kuwa ni Angelina Mutahiwa na Makamu Mwenyekiti Zanzibar ni Haji Ambar Khamis.

Kwa mujibu wa Mbatia, Katibu Mkuu ni Elizabeth Mhagama, Naibu Katibu Mkuu Bara ni Rehema Kahangwa na Naibu Katibu Mkuu Zanzibar ni Mussa Kombo Mussa na Mweka Hazina ni Mike Karawa.

Katika mkutano huo na waandishi wa habari, Mbatia pia aliomba serikali kuwasikiliza vijana juu ya mawazo waliyonayo kwa sababu ndiyo kundi lenye watu wengi katika taifa.

"Inatubidi pia kuwasikiliza hawa vijana wanataka nini, bila kufanya hivyo ni bomu linalosubiri kupasuka kwa sababu wasiposikilizwa na ujio huu wa mitandao ya kijamii wanaweza kufanya jambo lolote tofauti na watu wenye umri mkubwa, na kabla ya kufikia huko ni vema tuwape nafasi ya kuwasikiliza.

"Ni rai yangu pia kwa jamii, serikali, vyama vya siasa, taasisi za dini na kwa kila Mtanzania kubadilika kifikra kuanza kuwashirikisha na kuwasikiliza vijana badala ya kuwalazimisha kuamini fikra ambazo zimepitwa na wakati, kwa sababu pia ndiyo wapigakura wakubwa," Mbatia alishauri.


**Bank of India (Tanzania) Ltd.**

*Relationships beyond banking*

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)**

**DISCLOSURES MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS, 2014**

**MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)**

| NO. | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE | |
|---|---|---|---|
| | | USD | TSHS |
| 1.0 | **Current Accounts** | | |
| a) | Required minimum opening balance | 500 | 500,000 |
| b) | **Monthly service fee (breakdown per customer)** | | |
| | Folio Charge | 4 | 6,000 |
| c) | Cheque withdrawal over the counter | | |
| | Up to Tshs 25,000,000 a day | - | free |
| | Over 25,000,000 a day | - | 0.15% of withdrawn amount |
| | Up to 5000 USD a day | free | - |
| | Over 5000 USD withdrawal | 0.6% of withdrawn amount | - |
| d) | Fees per ATM withdrawal | - | - |
| e) | ATM mini statement | - | - |
| f) | Interim/additional statement per page | 1.50 | 1500 |
| g) | Periodic scheduled statement | free | free |
| h) | Cheque book **(50 leaves)** | 27 | 42,000 |
| i) | Dishonoured Cheque | 55 | 70,000 |
| j) | Special clearance | | |
| | Within walking distance 1km | 45 | 70,000 |
| | More than 1km | 65 | 95,000 |
| k) | Counter cheque | - | - |
| l) | Inward/Outward cheque collection-USD | 0.60% Min comm. 18 postages USD 90 | - |
| m) | Cancelation of bankers cheque/DD | 15 | 20,000 |
| n) | | | |
| o) | Stop payment | 28 | 35,000 |
| p) | Standing order | - | - |
| q) | Balance enquiry | free | Free |
| r) | Issue of Balance certificate | 7 | 9,000 |
| s) | New ATM card issuance | - | - |
| t) | ATM card renewal or replacement | - | - |
| u) | Overdrawn account interest charge | - | - |
| | Overdrawn in current account | 2% over the TOD rate | 2% over the TOD rate |
| | Overdrawn in loan account | 2% over regular rate | 2% over regular rate |
| | Unarranged overdraft | 2% over the TOD rate | 2% over the TOD rate |
| v) | Interbank transfer | - | - |
| w) | Bill payments through ATM | - | - |
| x) | Deposit fee | - | - |
| | **Savings Accounts** | | - |
| | (Up to USD 5000) | Free | - |
| | (Over USD 5000) | 0.6% of deposited amount | - |
| | Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both below and above USD 5000) | 12% (Min USD 1) of the aggregate of small currency amount | - |
| | **Current account.** | | |
| | (Up to USD 10000) | Free | - |
| | (Over USD 10000) | 0.6% of deposited amount | - |
| | Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both below and above USD 5000) | 12% (Min USD 1) of the aggregate of small currency amount | - |
| v) | Other (please specify) | - | - |

| | | | |
|---|---|---|---|
| b) | Cash withdrawal per day-Free of charge up to amount | 2,000 | 25,000,000 |
| c) | Cash withdrawal charges over USD 2,000 to 5,000 per day | 0.25% of withdrawal amount | |
| d) | Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | 0.60% of withdrawal amount | |
| e) | Cash withdrawal charges over TZS 25,000,000 per day | | 0.15% of withdrawal amount |
| f) | Required minimum opening balance | | |
| | Without Cheque book | 50 | 50,000 |
| | With Cheque book | 200 | 200,000 |
| g) | Monthly service fee | - | - |
| h) | Interim statement | 1.5 per page | 1500per page |
| i) | Cheque book charges 25 leaves | 15 | 20,000 |
| j) | Account closure | 25 | 35,000 |
| k) | **Maintenance of minimum account balance** | | |
| | Without cheque book | 50 | 50,000 |
| | With cheque book | 200 | 200,000 |
| l) | **Minimum balance charges (in case of non maintenance of minimum balance )** | | |
| | Without cheque book | 4 p.m | 900 p.m |
| | With cheque book | 15 p.m | 3,600 p.m |
| 3.0 | **Current Accounts** | | |
| | Ledger folio charges per folio (40lines per folio) | 4 per folio | 6,000 per folio |
| | Cash withdrawal per day-Free of charge up to amount | 5,000 | 25,000,000 |
| | Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | 0.6% of withdrawal amount | - |
| | Cash withdrawal charges over TZS 25.00 Mn per day | | 0.15% of withdrawal amount |
| | Cheque book charges 50 leaves | 27 | 42000 |
| | Account closure charges | 70 | 85,000 |
| | **Maintenance of minimum account balance** | 500 | 500,000 |
| | **Minimum balance charges** | 15 p.m | 20,000 p.m |
| 4.0 | **Electronic Banking** | | |
| a) | Internet banking monthly fee | - | - |
| b) | Internet transfers | - | - |
| c) | SMS banking | - | - |

| | | Minimum SMS Alert Charge ( to be recovered quarterly upfront) | Number of Free SMS on paying SMS Alert charge | SMS Alert charge per SMS beyond the free SMS (To be recovered in monthly basis) |
|---|---|---|---|---|
| d) | SMS Alert facility - | | | |
| | -Individual | USD 3.00 (USD a/c) TZS 5,000 (TZS a/c) | 1st 50 SMS in a Qtr | USD 0.05 per SMS TZS 100 per SMS |
| | -Corporate | USD 10.00 (USD a/c) TZS 15,000 (TZS a/c) | 1st 150 SMS in a Qtr | USD 0.05 per SMS TZS 100 per SMS |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| e) | Others | - | | - |
| 5.0 | **Foreign Exchange Transaction.** | - | | - |
| a) | Purchase/sale of TCs transactions over the counter | - | | - |
| b) | Purchase of foreign Cheque. | - | | - |
| c) | Sale/purchase of cash passport. | - | | - |
| d) | Telegraphic transfer. | | | |
| | Remittances Outward(TISS) | 10 | | 10,000 |
| | Other Outward remittances: | | | |
| | | A/C holder | Non A/C holder | |
| | Up to USD 6,000 | 15 | 40 | -- |
| | USD 6001-10,000 | 30 | | -- |
| | Above USD 10,000 | 0.35%max USD 210 | | -- |
| e) | Telex/SWIFT. | 30 | | - |
| f) | Transfer from foreign currency denominated account to local current account (within bank and to other bank). | | | |
| 6.0 | **Other Charges** | | | |
| a) | Activation of Dormant Accounts - Per Activation | | | |
| | -Individuals | 3 | | 5,000 |
| | -Corporate | 6 | | 12,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 7.0 | **Personal Loans. Charges** | | |
| a) | Processing/Arrangement/Appraisal fee | | |
| i) | Personal loans | 1.50% | 1.50% |
| ii) | Overdrafts | 1.50% | 1.50% |
| iii) | Mortgage finance | 1.50% | 1.50% |
| iv) | Asset finance | 1.50% | 1.50% |
| b) | Unpaid loan instalment | 5.00% Over the applicable rate | |
| c) | Early repayment | 2.5% of prepaid loan amount | |
| d) | Valuation fees | As per actual charges by valuer | |
| e) | **Others** | | |
| i) | Documentation charges | Actuals as per advocate bill | |
| ii) | Document Handling Charges | 0.30% of loan amount | |
| iii) | Inspection Charges | Tshs 30,000 per visit | |
| iv) | Modification charges | 0.25% on the sanctioned limit | |
| 8.0 | **Guarantee (Performance/Financial)** | | |
| | Guarantee Commission | 1.35% per quarter or part there of minimum for one quarter | |
| | Guarantee against 100% cash margin | 50% concession on the above rate | |
| 9.0 | **Imports** | | |
| | LC opening charges | 1.35% per quarter +SWIFT charges USD 30 | |
| | LC against 100% cash margin | 50% concession on the above rate | |
| | LC amendment charges | Per amendment 0.40% of LC mount (minimum USD 60 and maximum USD 325) +SWIFT charges USD 30 (same for LC against 100% cash margin) | |
| | Acceptance of bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 180 | |
| | Retirement of Bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | |
| | Inward Bills for collection | 0.30% of Bill amount minimum USD 150 | |
| 10.0 | **Exports** | | |
| | Negotiation of Bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | |
| | Confirmation of Export LC | 0.90% per quarter +SWIFT charges USD 30 | |
| | LC advising charges | USD 150 | |
| | Export Bills for collection | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | |
| | | | |

No Penalties & Other sanctions have been imposed by Bank of Tanzania (BOT)during the period covered by the disclosure

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name. | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ashwani Kumar Negi | Managing Director | Signed | 08.07.2019 |
| 2. | Poncian Katesigwa | Head of Finance | Signed | 08.07.2019 |
| 3. | Allen Richard | Internal Auditor | Signed | 08.07.2019 |

**OTHER DISCLOSURES (VIAMBATANISHI**

| No. | ITEM/TRANSACTION | USD | TSHS |
|---|---|---|---|
| 1.0 | **Base or Prime Lending rate** | 7.00% p.a. | 15.00% p.a. |
| 2.0 | **Maximum Spread above Base or Prime Lending rate** | 7.00% | 7.00% |
| 4.0 | **Penal interest** | | |
| a) | For Non Compliance of Terms of sanction | 3% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| b) | For Overdrawing/ Excess Drawings due to non – payment of interest/ Instalments/ Charges | 5% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| 5.0 | **Deposit Rate** | | |
| i) | Current Deposit | Nil | Nil |
| ii) | Savings Bank Deposit | 0.50% p.a. | 2.50% p.a. |
| iii) | Fixed/Recurring/QIC/MIC deposit | Up to USD 10,000 | Up to TZS 10,000,000 |
| | 6 months | 2.00% | 6.50% |
| | Over 6 months | 2.50% | 7.50% |
| | | Over USD 10,000 | Over TZS 10,000,000 |
| | 6 months | 2.50% | 7.00% |
| | Over 6 months | 3.00% | 8.00% |
| | * No interest is payable in case of premature withdrawal of fixed deposits | | |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| No. | Name | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ashwani Kumar Negi | Managing Director | Signed | 08.07.2019 |
| 2. | Poncian Katesigwa | Head of Finance | Signed | 08.07.2019 |
| 3. | Allen Richard | Internal Auditor | Signed | 08.07.2019 |

215348302

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ELIMU/ MASOMO

**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA



## CHETI KIMEPOTEA



115347002

**TRIPHONIA D.N. BONGOLE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye **index namba S.0137/0899** kilichotolewa na MKWAWA HIGH SCHOOL mwaka 2000. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **IR/RB/2216/2013.**

## KUPOTEA KWA CHETI




**Edom Adam** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0900-0042 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2004 katika shule ya Sekondari Mwigu na Leaving certificate.

**Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa: IR/RB/3061/2010**

## KUPOTEA KWA CHETI



115347202

**Aman Erasto** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0116/0056 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2000 katika shule ya Sekondari Kantalamba.

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa: SUM/RB/3345/09**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**
**Arusha Mjini**

**Usimamizi wa Mirathi 139/2019**

Ombi la Shamim Ibrahim Kamal ..........kuteuliwa Msimamizi wa mirathi marehemu ............Mohamed Abdulrehman Abood.

Kwa yeyote anayehusika na mirathi hii .
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 14/8/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Tarehe 29/7/2019

115347902

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA KILOSA**

**MAHARI: KILOSA**

**MAOMBI NA ..36..MWAKA 2017**

**SALVANO A.KES.........................................MUOMBAJI**

**FRANSICE A.KISAMO.............................MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA....FRANSICE A.KISAMO**

Mdai/Wadai amefungua/Wamefungua shauri mbele ya baraza la ardhi na nyumba dhidi yako/yenu.Shauri hili limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 27 mwezi 08 mwaka 2019 saa mbili asubuhi/mbele ya my RS Mnyukwa mwenyekiti na Baraza.

Unatakiwa/mnatakiwa ufike/mfike wewe mwenyewe/ninyi wenyewe au wakili wako/wenu mwakilishi wako/wenu pasipo kukosa na ulete /mlete utetezi wako/wenu ndani ya siku ishirini na moja(21) toka tarehe ya kupokea kuitwa shaurini.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/muhuri wa baraza hili leo tarehe....12...mwezi ....06.....mwaka....2019.

115347402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;153/2019**

**Ombi la MUSSA GERVAS NG'ATUNGA**
**Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu**
**PAULINA GERVAS NG'ATUNGA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 06/08/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 24/07/2019

115347502


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311*

**Kwa Habari Motomoto**

**usikose Gazeti lako la**

**Nipashe kila siku**

**NJOO UTANGAZE**

**BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**



OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# TANDAHIMBA COMMUNITY BANK PLC

## UONYESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30/06/2019

(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 30/06/2019 | Robo Mwaka/Uliopita 31/03/2019 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1. | Fedha Taslimu | 93,177 | 467,156 |
| 2. | Salio katika benki kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji katika amana za serikali | - | - |
| 4 | Salio katika benki nyingine na Taasisi za fedha | 369,649 | 1,420,116 |
| 5 | Hundi na miamala ya kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala baina ya matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizofikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za wateja zilizokubalilka | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa benki nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji katika amana nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo halisi iliyopo | 2,520,157 | 2,613,421 |
| 12 | Mali nyingine | 299,536 | 365,954 |
| 13 | Uwekezaji wa hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali zisizohamishika,mitambo na vifaa | 180,945 | 166,023 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | 3,463,464 | 5,032,670 |
| | | - | - |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za benki nyingine na Taasisi za fedha | - | - |
| 18 | Amana za wateja | 815,773 | 1,983,285 |
| 19 | Dhamana ya malipo kwa fedha taslimu | | |
| 20 | Amana Maalum | - | - |
| 21 | Maagizo ya malipo /Fedha kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za kibenki zilizotolewa | - | - |
| 23 | limbiko la kodi na ghalama zitakazolipwa | - | - |
| 24 | Dhima la tozo kwaajili ya usuluhishi baina ya benki na mteja | - | - |
| 25 | Fedha za washirika(MIVARF Grant) | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya kipindi kijacho na tozo nyingine zitakazo lipwa baadaye | - | - |
| 27 | Dhima nyingine | 172,564 | 441,235 |
| 28 | Madeni | 232,703 | 263,128 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **1,221,040** | **2,687,648** |
| **30** | **MALMI /(DHIMA) HALISI(16 kutoa 29)** | **2,242,424** | **2,345,022** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa hisa uliolipwa | 4,487,402 | 4,501,107 |
| 32 | Akiba ya mtaji | (2,410,744) | (2,360,795) |
| 33 | Mapato yaliyobakizwa | (4,100) | 43,208 |
| 34 | Faida(hasara)ya kipindi husika | 154,021 | 145,657 |
| 35 | Akaunti nyingine za mtaji | 15,845 | 15,845 |
| 36 | Stahiki za wenye hisa chache | - | - |
| **37** | **JUIMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **2,242,424** | **2,345,022** |
| 38 | Dhima zisizo dhahiri | - | - |
| 39 | Mikopo chechefu | 132,753 | 63,717 |
| 40 | Tengo kwa ajili ya mikopo chechefu | 56,765 | 65,219 |
| 41 | Mali nyingine chechefu | - | - |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) | Uwiano wa fedha za wanahisa na jumla ya mali | 65% | 47% |
| (ii) | Uwiano wa mikopo chechefu na jumla ya mikopo ghafi | 5% | 2.4% |
| (iii) | Uwiano wa mikopo ghafi na jumla ya amana | 309% | 132% |
| (iv) | Uwiano wa mikopo halisi na jumla ya mali halisi | 73% | 52% |
| (v) | Uwiano wa mali zinazozalisha na jumla ya mali | 83% | 80% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -59% | 82% |
| (vii) | Ongezeko la mali | -31% | 12% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO INAYOISHIA 30/06/2019

(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Robo ya mwaka wa sasa | Robo ya mwaka linganishi(Mwaka uliopita ) | Limbikizo la mwaka wa sasa | Limbikizo la mwaka linganisha (mwaka uliopita) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 30/06/2019 | 30/06/2018 | 30/06/2019 | 30/06/2018 |
| 1. | Mapato yariba | 87,192 | 78,871 | 244,740 | 171,644 |
| 2. | Gharama za riba | (2,858) | (17,432) | (7,440) | (33,291) |
| 3. | Mapato halisi ya riba(1 kutoa 2) | **84,334** | **61,439** | **237,300** | **138,353** |
| 4. | Madeni viza yaliyopitwa | | | | |
| 5. | Punguzo/ongezeko la tengo katika mikopo | 8,454 | (13,975) | 292 | (16,467) |
| **6.** | **Mapato yasiyo ya riba** | **28,544** | **121,052** | **66,789** | **207,560** |
| | 6.1 Faida/(hasara) zitokanazo na miamala ya fedha za kigeni | - | - | - | - |
| | 6.2 Ada na kamisheni | 28,544 | 121,052 | 66,789 | 207,560 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato mengine | - | - | - | - |
| **7.** | **Gharama zisizo na riba** | **(168,640)** | **(164,032)** | **(308,481)** | **(308,363)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (83,715) | (67,711) | (163,528) | (146,516) |
| | 7.2 Ada na kamishani | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama nyingine | (84,925) | (96,321) | (144,953) | (161,847) |
| 8. | **Faida/(Hasara) ya uendeshaji** | **(47,308)** | **4,484** | **(4,100)** | **21,083** |
| 9 | Tengo la kodi ya mapato | - | (1,345) | - | (6,325) |
| **10** | **Faida /(Hasara)Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(47,308)** | **3,139** | **(4,100)** | **14,758** |
| **11** | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa(bainisiha)** | | | | |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | | | | |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 15 | 11 | 15 | 11 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (10.54) | 0 | (1) | 0 |
| 14 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | (I ) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -1.4% | 0.1% | -0.1% | 0.5% |
| | (ii) Uwiano wa Faida Baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -2.1% | 1% | 0% | 1% |
| | (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo na Riba na Mapato Ghafi | 149% | 90% | 101% | 89% |
| | (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 6% | 3% | 16% | 6% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHAKWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30/06/2019

(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Robo mwaka ya sasa | Robo Mwaka iliyopita | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la mwaka Linganishi(Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 30/06/2019 | 31/03/2019 | 30/06/2019 | 30/06/2018 |
| **I:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (4,100) | 43,208 | 39,108 | 21,083 |
| | Marekebisho Kwa Ajili ya: | (1,840) | (1,840) | (3,680) | (26,097) |
| | - Hasara Katika Mali | 8,293 | 7,325 | 15,618 | 32,958 |
| | - Badiliko halisi katika Mikopo | 93,264 | 334,367 | 427,631 | (308,372) |
| | - Faida/Hasara kwenye mauzo ya mali | - | - | - | - |
| | - Mabasiliko halisi katika amana | (1,167,512) | 890,628 | (276,884) | (2,564,783) |
| | - Mabadiliko halisi katika amana za muda mfupi zilizo afikiwa | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | (268,671) | 123,114 | (145,557) | 63,600 |
| | - Mabadiliko halisi katika mali nyingine | 66,418 | (152,317) | (85,899) | (500,971) |
| | - Kodi iliyolipwa | - | - | - | - |
| | - Mengineyo(bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika)kwa shughuli za uendeshaji** | **(1,274,148)** | **1,244,485** | **(29,663)** | **(3,282,582)** |
| **II:** | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | | | |
| | gawio lililopokelewa | - | - | - | |
| | Ununuzi wa mali za kudumu | (16,064) | (3,347) | (19,411) | -34,209 |
| | Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | | | - | |
| | Ununuzi wa amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - | 0 | 0 |
| | Mapato kutokana na mauzo ya amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | |
| | Mengineyo (Bainisha) | | | - | 0 |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji** | **(16,064)** | **(3,347)** | **(19,411)** | **(34,209)** |
| **III:** | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha** | | | | |
| | Ulipaji wa madeni ya muda mrefu | - | - | - | |
| | Mapato kutokana na utoaji wa madeni ya muda mrefu | - | - | - | |
| | Mapato kutokana na utoaji wa mtaji wa hisa | (13,705) | 2,750 | (10,955) | 3,373,092 |
| | Gawio lilololipwa kwa fedha taslilmu | - | - | - | |
| | Mabadiliko halisi katika madeni mengine | (30,424) | (520,337) | (550,761) | (678,867) |
| | Mengnineyo | (90,106) | (12,301) | (102,407) | (56,480) |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(Zilizotumika) kwa shughuli za kifedha** | **(134,235)** | **(529,888)** | **(664,123)** | **2,637,745** |
| **IV:** | **Fedha taslimu na mali zinazo fanana na fedha taslimu** | | | | |
| | Ongezeko/Punguzo halisi kaitka fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslilmu | (1,424,447) | 711,250 | (713,197) | (679,046) |
| | Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa robo mwaka/Mwaka | 1,887,272 | 1,176,022 | 3,063,294 | 2,566,143 |
| | **Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa robo mwaka/Mwaka** | **462,825** | **1,887,272** | **2,350,097** | **1,887,097** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHA 30/06/2019

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | ziada ya kisheria | Tengo la ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Robo Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa Robo mwaka wa sasa | 4,501,108 | 0 | -2,317,588 | 12,116 | 15,845 | 133,541 | 2,345,022 |
| Faida/(hasara) halisi baaada ya kodi ya mapato | | | -4,100 | | | | -4,100 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | | | 0 |
| Miamala na wanahisa | -13,706 | | 0 | | 0 | | -13,706 |
| Gawio lililolipwa | | | 0 | | | | 0 |
| Ziada ya kisheria | | | 0 | 0 | | | 0 |
| Tengo la ziada ya jumla | | | 0 | | 0 | 8,364 | 8,364 |
| Mengineyo | | | -93,156 | | 0 | 0 | -93,156 |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka** | 4,487,402 | 0 | -2,414,844 | 12,116 | 15,845 | 141,905 | 2,242,424 |
| **Robo ya Mwaka iliyopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo mwaka** | 4,498,358 | 0 | -2,363,284 | 2,836 | 27,536 | 143,431 | 2,308,877 |
| Faida/(hasara) halisi baaada ya kodi ya mapato | | | 43,208 | | | | 43,208 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | | | 0 |
| Miamala na wanahisa | 2,750 | | | | 0 | | 2,750 |
| Gawio lililolipwa | | | 0 | | | | 0 |
| Ziada ya kisheria | | | -9,280 | 9,280 | | | 0 |
| Tengo la ziada ya jumla | | | 11,691 | | -11,691 | | 0 |
| Mengineyo | | | 77 | | 0 | -9,890 | -9,813 |
| **Salio la mwisho wa robo mwaka** | 4,501,108 | 0 | -2,317,588 | 12,116 | 15,845 | 133,541 | 2,345,022 |

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha ,sera za uandaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

| | | **Tarehe** |
|---|---|---|
| Mugwagi Steven<br>**Mtendaji Mkuu** | imesainiwa | 30/07/2019 |
| Anthony Bichakila<br>**Mkuu wa fedha** | imesainiwa | 30/07/2019 |

**Sisi,tuliotajwa hapo chini ,wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu ,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006,na zinaonesha hali halisi.**

| | | **Tarehe** |
|---|---|---|
| Said Msomoka<br>Mjumbe wa bodi | imesainiwa | 30/07/19 |
| Elibariki Masuke<br>Mjumbe wa bodi | imesainiwa | 30/07/19 |

215349202

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MAN CITY YAJIANDAA KUMSAJILI OYARZABAL

Lengo ni kuziba pengo la Sane kama atafanikiwa kuondoka klabuni hapo...

**MANCHESTER, Enfgland**

KLABU ya Manchester City itajipanga kuanza mchakato wa kumsajili mshambuliaji wa Real Sociedad, Mikel Oyarzabal kwa dau la Euro milioni 75 ambalo limetajwa katika mkataba wake, kama winga Leroy Sane atafanikiwa kujiunga na Bayern Munich, limeandika gazeti ya AS.

Oyarzabal , ambaye ana umri wa miaka 22 na aliifungia timu yake ya Taifa ya Hispania katika ushindi wa mabao 3-0 , kwenye mechi dhidi ya Sweden ya kuwania tiketi ya kufuzu fainali zijazo za Euro 2020 iliyochezwa Juni mwaka huu, pia akafanya vema akiwa na La Roja U-21 ilipopata ushindi dhidi ya wenzao wa Italia kwenye mashindano ya Ulaya.

Kocha wa City, Pep Guardiola amemtaja moja kwa moja mchezaji huyo tegemeo wa Basque kuwa ndiye chaguo sahihi za kuziba nafasi ya Sane ambaye anaonekana kuwa anaweza kuondoka, huku klabu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu England inajiandaa kumpa kiasi kikubwa cha mshahara.

Licha ya kuonekana usajili huo unawezekana huku La Real yenyewe ikiwa ilijiandaa kuimarisha kikosi chake cha muda mrefu kwa kumpa mkataba mpya kwenye kipindi cha majira ya joto mwaka jana, baada ya kuanza kuwindwa na Athletic Bilbao ambayo ilionyesha nia ya kumnasa mchezaji huyo aliyezaliwa katika mji wa Eibar na kuhamia San Mames.

Kocha wa Bayern, Niko Kovac, amemweleza mtangazaji wa kituo cha habari za michezo cha Ujerumani kiitwacho ZDF mwishoni mwa wiki kuwa, klabu yake ambao ni mabinggwa wa Ligi Kuu wako kimya wakisubiri uamuzi wa dili la kumuuza Sane.

"Tunataka kumsajili mchezaji huyo wa kiwango cha juu," alisema kocha huyo mwenye umri wa miaka 47. "Leroy ni mchezaji mkubwa ambaye kiwango chake kimeonekana ndani ya Ligi Kuu England na pia akiwa na timu yake ya Taifa. Tunamtaka mchezaji huru.

"Idara yetu ya utawala inalifanyia kazi kwa umakini suala la mchezaji huyu. Kama unavyoona sio jambo rahisi, na kama ingekuwa rahisi, tayari usajili wa winga huyo ungekuwa umeshakamilika kabla ya kufikia muda huu. Lakini nina hakika kuwa tunafikiria tutafanikiwa kumnasa."

Wakati huo huo, City imewasilisha maombi mengine kwa Barcelona kwa ajili ya kumwania beki wa kulia wa Timu ya Taifa ya Ureno, Nelson Semedo, limeandika Outlet Sport cha Hispania.

Imeelezwa kuwa, beki huyo mwenye umri wa miaka 25 anatajwa kuwindwa baada ya klabu hiyo kushindwa kunasa saini ya beki mwingine wa kuliwa wa Juventus, Joao Cancelo.

Imefahamika kuwa Barca iliamua kuzikacha ofa mbalimbali zilizowasilishwa kwa ajili ya kumsajili Semedo katika kipindi hiki cha majira ya joto, baada ya kutaka kuona anabakia Camp Nou kutokana na Kocha Ernesto Valverde kuanza kumjumuisha kwenye mipango yake.

## KWA UFUPI

**MADRID YAMBANIA BALE**
RAIS wa Real Madrid, Florentino Perez, amefanya uamuzi wa kusitisha mchakato wa uhamisho wa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Wales, Gaerth Bale, kujiunga na klabu ya Jiangsu Suning ya China. ***(Sun)***

**PALACE YAIGOMEA EVERTON**
CRYSTAL Palace imekacha kupokea ofa ya Everton ambayo inahitaji saini ya winga wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Wilfried Zaha. ***(Mail)***

**BIELIK KUONDOKA ARSENAL**
BEKI wa kati wa Poland, Krystian Bielik (21), anajiandaa kuondoka Arsenal na moja ya klabu ambazo zimetajwa kumwania zinatoka katika Ligi ya Championship. ***(Sportowefakty)***

**EVERTON MTEGONI**
MABOSI wa Crystal Palace wanataka kulipwa zaidi ya pauni milioni 60 na pia kujadiliana kuhusu namna Everton itakavyojipanga kulipa ada hiyo ya uhamisho wa winga raia wa Ivory Coast, Wilfried Zaha. ***(Mirror)***

**EVERTON KUSAJILI WATANO**
ILI kuwa na kikosi imara, Everton itatakiwa kusajili wachezaji wapya watano, huku kiungo wake Msenegal Idrissa Gueye, ambaye ana umri wa miaka 29, anakaribia kujiunga na PSG. ***(Liverpool Echo)***

**PEPE MAMBO SAFI**
WINGA wa Lille, Nicolas Pepe (24), anatarajia kukamilisha uhamisho wake wa kuhamia Arsenal kwa ada ya pauni milioni 72 kati ya kesho au keshokutwa, hata hivyo mabingwa wa Ligi Kuu Ufaransa, Paris St-Germain bado hawajawasilisha ofa yoyote ya kumwania nyota huyo. ***(La Voix Du Nord)***

**SERGEJ, UNITED KIMEELEWEKA**
MANCHESTER United imefikia makubaliano ya kumsajili kiungo wa Lazio na Timu ya Taifa ya Serbia, Sergej Milinkovic-Savic, ambaye ana umri wa miaka 24. ***(Mail)***

**MATUIDI AITAKA UNITED**
KIUNGO wa Juventus, Blaise Matuidi, ambaye ana umri wa miaka 32, ameonyesha nia ya kutaka kujiunga na Manchester United. ***(Corriere di Torino, via Express)***

**SANE APATA MRITHI**
MABOSI wa Manchester City wamemtaja mshambuliaji wa Real Sociedad, Mikel Oyarzabal (22), kuwa ndiye atarithi nafasi itakayoachwa na Sane na wako tayari kulipa ada ya uhamisho ya nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Hispania ambayo ni Euro milioni 75. ***(AS)***

**ADEBAYOR SOKONI**
KLABU ya West Ham United imemweka straika wa zamani wa Arsenal na Tottenham, Emmanuel Adebayor katika orodha ya wachezaji inaowahitaji. Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 35, ambaye ni mchezaji huru, anatajwa kuwaniwa na Watford na Sheffield United.***(Sun)***

**VILLA YAIKATALIA BURNLEY**
KLABU ya Aston Villa haiko tayari kulipa kiasi cha pauni milioni 10 ambacho kinatakiwa na Burnley ili kumuuza golikipa wa Timu ya Taifa ya England, Tom Heaton, ambaye ana umri wa miaka 33. ***(Birmingham Mail)***

**NSOKI KUTUA NEWCASTLE**
BEKI wa kushoto wa Paris St-Germain, Stanley Nsoki (20), anajiandaa kujiunga na Newcastle United, ingawa klabu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu England bado haijatimiza matakwa ya kulipa pauni milioni 13.5, ambazo zinatakiwa na mabingwa hao wa Ufaransa. ***(Newcastle Chronicle)***



## HABARI MICHEZO

# TAIFA STARS KUIFUATA KENYA KWA TAHADHARI

**Na Shufaa Lyimo**

NAHODHA wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), John Bocco, amesema kuwa watakwenda kucheza kwa tahadhari katika mchezo wa marudiano wa kuwania kufuzu fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani ( CHAN) dhidi ya Kenya (Harambee Stars).

Timu hizo zilitoka sare ya bila kufungana katika mchezo wa jana na zinatarajia kurudiana mwishoni mwa wiki jijini Nairobi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Bocco alisema kuwa wataendelea kufanya mazoezi ya "nguvu" ili kuhakikisha wanakwenda kufanya vizuri katika mechi hiyo na hatimaye kusonga mbele.

Bocco alisema kuwa matokeo ya sare waliyopata juzi hawajaridhika nayo, hivyo wanawaomba Watanzania waendelee kuwapa ushirikiano kwa ajili ya kutimiza malengo yao ya kuwafunga wapinzani wao.

"Tutakwenda kucheza kwa tahadhari kubwa huko Kenya, ili wasipate nafasi ya kutufunga, lengo letu ni kusonga mbele. Tunaomba Watanzania wazidi kutuunga mkono ili tutimize malengo yetu na kuipeperusha vema bendera ya Taifa letu," alisema Bocco.

Alisema kuwa mechi ya juzi ilikuwa ngumu na yenye ushindani, lakini pia timu yao ilikosa bahati ya kufunga kutokana na nafasi ilizotengeneza.

"Bado tuna nafasi ya kusonga mbele, tunahitaji kufanya vema katika mechi ya marudiano, tutakuwa ugenini, lakini hilo si tatizo, lolote linawezekana katika soka," Bocco alisema.

Mrundi Etienne Ndayiragije ambaye anashirikiana na Juma Mgunda na Suleiman Matola, ndio wamepewa kikosi hicho kukiongoza.




Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, akizungumza kuhusu maandalizi ya Tamasha la Simba Day litakalofanyika wiki ijayo hapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# Watanzania wanne wapata ulaji CAF

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKISHO la Soka Afrika (CAF), limeteua waamuzi wanne na makamishna wawili kutoka hapa nchini kwa ajili ya kusimamia mechi za kimataifa za Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho, imeelezwa.

Taarifa kutoka CAF imemtaja mwamuzi, Elly Sasii ndiye ameteuliwa kuchezesha mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika kati ya Aigle Noir ya Burundi dhidi ya Gor Mahia ya Kenya utakaochezwa Agosti 11, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Prince Louis Rwagasore nchini Burundi.

Ilisema kuwa Sasii kutoka jijini Dar es Salaam atasaidiwa na Frank Komba (mwamuzi msaidizi namba 1), Ferdinand Chacha (mwamuzi msaidizi namba 2) wa Mwanza na mwamuzi wa akiba ni Emmanuel Mwandembwa kutoka Mbeya.

Kamishna wa mchezo huo ametajwa kuwa ni Gaspard Kayijuka kutoka Burundi.

Pia CAF imeteua Mtanzania, Ahmed Mgoyi, kuwa Kamishna wa mchezo wa marudiano Ligi ya Mabingwa, kati ya Gor Mahia dhidi ya Aigle Noir utakaochezwa kati ya Agosti 23 na 25 mwaka huu nchini Kenya, huku Khalid Abdallah, akiteuliwa kuwa Kamishna wa Mchezo wa Kombe la Shirikisho kati ya Proline FC ya Uganda na Master Security Services ya Malawi utakaochezwa Uwanja wa Kampala Startimes, Uganda.

## Kocha Matu, JKU kimeeleweka

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

LICHA ya kushindwa kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar, uongozi wa JKU umesema kuwa hauna mpango wowote wa kumfukuza kazi kocha mkuu wa timu hiyo, Omar Khamis Matu, imefahamika.

Katibu Mkuu wa JKU, Ujudi Saadu, aliliambia gazeti hili kuwa wataendelea kufanya kazi na kocha huyo katika msimu mpya kwa sababu wanaamini uwezo na uzoefu alionao kwenye kazi hiyo.

Saadu alisema kuwa wamekubali matokeo ya msimu uliopita, na sasa wanajipanga kufanya vema katika msimu ujao ili waweze kulirejesha taji hilo klabuni kwao.

"Kufanya vibaya kwa timu haimaanishi kuwa kocha hafai, ila tatizo linatokana na wachezaji wenyewe kushindwa kuzingatia wanayofundishwa na mwalimu wao, hatuna mpango wa kubadilisha kocha, tutaendelea kuwa na Matu, anafaa kukinoa kikosi cha JKU, kuukosa ubingwa haimaanishi anamapungufu," alisema Saadu.

Katibu huyo aliongeza kuwa kikosi chao kimeshaanza mazoezi kwa ajili ya kujiweka imara kuelekea msimu mpya na wanaamini wataanza ligi kwa kupata matokeo mazuri.

Timu ya JKU ambayo ilishindwa kutetea ubingwa wake na kuambulia nafasi ya nne katika msimu uliopita.

## Mavunde kupeleka makocha Rombo

**Na Mary Mosha, ROMBO**

JUMLA ya timu 47 za vijana zinatarajia kuchuana katika shindano la kuwania Kombe la Rombo (DC Cup) lililopangwa kufanyika kuanzia Julai 28 hadi Septemba 19 mwaka huu kwenye viwanja mbalimbali wilayani Rombo, Kilimanjaro.

Akizindua michuano hiyo, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Antony Mavunde, aliwataka wachezaji watakaoshiriki michuano hiyo kutumia fursa waliyoipata kama kichocheo cha maendeleo katika kujiajiri kwa kutumia vipaji vyao.

Mavunde aliwataka pia vijana wanaoingia kwenye kinyang'anyiro hicho kuwa atawatafutia makocha wenye ujuzi rasmi ili kuwasaidia kunyanyua vipaji vyao na baadaye kusajiliwa katika klabu za Ligi Kuu Bara, nje ya Tanzania hadi kuitwa kwenye Timu ya Taifa (Taifa Stars).

Alisema anataka vijana watumie michuano hiyo kupandisha viwango vyao na kuwavutia mawakala na makocha mbalimbali kufika Rombo kuchagua vipaji vipya.

"Kwanza kabisa ninawaahidi kuwa nitaleta wataalamu mbalimbali wa soka nchini waje kuangalia vipaji vyenu mara mtakapoingia hatua ya 16 bora, pia kwa mshindi wa kwanza nitaongeza Sh. milioni moja kwenye zawadi iliyoandaliwa," alisema Mavunde.

Michezo
Jumanne Julai 30, 2019
Nipashe



City yajiandaa kumsajili Oyarzabal

HABARI UK 30



Kiungo wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Hassan Dilunga (kushoto), akimtoka mchezaji wa Kenya (Harambee Stars) katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), iliyochezwa juzi jijini Dar es Salaam. Timu hizo zilitoka suluhu. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# SIMBA MIPANGO AFRIKA IMEKOLEA

## ●●●Kuwafuata UD Songo na ndege ya kukodi, maandalizi Simba Day...

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI kikosi cha mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kinatarajia kurejea nchini kesho kikitokea kambini Afrika Kusini, uongozi wa timu hiyo umesema kuwa maandalizi kwa ajili ya Wiki ya Simba ambayo kilele chake mwaka huu itakuwa ni Agosti 6, kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, yamekamilika.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori, alisema kuwa kikosi cha timu yao kitarejea nchini kesho usiku na mara baada ya kufika, utafanyika uzinduzi rasmi wa jezi mpya huku pia ikijiandaa kusafiri kwa ndege ya kukodi kuelekea Msumbiji kuwafuata UD Songo kwa ajili ya mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Afrika.

Magori alisema kuwa tamasha la mwaka huu litakuwa bora zaidi kutokana na maandalizi yake na wanatarajia kupata kipimo sahihi cha kuelekea katika mashindano ya kimataifa kwa kucheza na wageni wao Power Dynamo kutoka Zambia.

Alisema kuwa wiki ya Simba Day itaanza kufanyika kesho na Agosti 2 mwaka huu, watazindua kadi za mpya za wanachama za kielektroniki ambazo zitakuwa na punguzo la bei tofauti na zile kadi za kawaida huku siku inayofuata wachezaji wote wa timu hiyo watakwenda kutoa misaada katika hospitali ya Ocean Road, ikiwa pamoja na uzinduzi wa nyimbo yao ya klabu hiyo.

"Tarehe hiyo hiyo (Agosti 3, mwaka huu), pia tutasaini mkataba na wadhamini wetu wa jezi na vifaa vya michezo, ambao watafahamika siku hiyo ikifika," alisema Magori.

Kiongozi huyo aliongeza kuwa pia wanatarajia kutembelea vituo vya watoto yatima hapa jijini na Agosti 5 mwaka huu, wachezaji wa Simba Queens watakwenda katika Shule ya Sekondari Makongo kwa lengo la kutoa hamasa kwa wanafunzi mbinu mbalimbali walizojifunza walipokuwa kwenye ziara yao nchini Ujerumani.

Naye Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Haji Manara, alisema kuwa wanatarajia mchezo wa kirafiki dhidi ya Power Dynamo, ambao utachezwa kuanzia saa 10:00 jioni, utakuwa wa kiwango cha juu huku pia ukitanguliwa na burudani mbalimbali za muziki.

Manara alisema pia mapema mchana, Simba B itacheza mechi ya ufunguzi dhidi ya yoso wenzao kutoka Fountain Gate Academy.

"Kauli mbiu ya Tamasha la Wiki ya Simba mwaka huu ni Iga Ufe This is Next Level# Miaka 10 ya wiki ya Simba, hili ni jambo jema na wengine wameiga," alisema Manara.

Mkurugenzi wa Uendeshaji na Utawala wa SportPesa Tanzania, Abbas Tarimba, alisema kuwa kampuni yao inawapongeza mabingwa hao wa Bara kwa kufanikiwa kufanya shughuli mbalimbali katika kuelekea kilele cha Simba wiki hiyo wao wanasema watashirikiana nao vema ili kuhakikisha manufaa yanapatikana zaidi.

Tarimba alisema pia anafurahi kuona Simba imeingia katika mfumo na utaratibu wa kuuza jezi zake rasmi na klabu yao itafaidika na mauzo hayo.

Aliwataka pia mashabiki na wanachama wa Simba kujitokeza kwa wingi uwanjani kushuhudia siku hiyo ya utambulisho wa wachezaji wao ambao itawatumia katika msimu ujao ambao anaamini ni wenye viwango vya juu.

# Stars, Burundi mtihani mpya

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), imepangwa kucheza na Burundi katika mechi za hatua ya awali ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Dunia zitakazofanyika Qatar mwaka 2022.

Katika kampeni hiyo, Taifa Stars ambayo sasa inanolewa na Kaimu Kocha Mkuu, Etienne Ndayiragije, itaanzia ugenini Burundi kati ya Septemba 2 na 10 na timu itakayopata matokeo mazuri, itasonga mbele na kutinga hatua ya makundi.

Ratiba hiyo inaonyesha pia katika hatua hiyo, Ethiopia itacheza dhidi ya Lesotho wakati Eritrea watawavaa Namibia na Somalia watawakaribisha Zimbabwe huku Botswana watajiandaa kupambana na Malawi.

**Timu ya Djibout yenyewe itaanza kampeni hiyo kwa kuwaalika Eswatini, Gambia watacheza nyumbani dhidi ya Angola, Liberia vs Sierra Leone, Mauritius vs Msumbiji, Sao Tome Principe vs Guinea Bissau, Sudan Kusini vs Equatorila Guinea, Comoro vs Togo, Chad vs Sudan, Shelisheli vs Rwanda.**

Kwa sasa Stars ina kibarua cha kuing'oa Harambee Stars ya Kenya katika mechi ya kusaka tiketi ya kucheza fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >